# Nipashe

Jumanne Septemba 10, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580019

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Mwalimu mbaroni kwa tuhuma kumcharanga mapanga mpenzi

UKURASA 3




UKURASA 13

# Mjadala hukumu ya kesi ya Lissu



• **Wanasheria** watoa ya moyoni, Mbowe asema safari kutafuta haki bado, Spika Ndugai asema jambo...*Ukurasa 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 2**

**JPM AMWAGA BIL. 33.5/- UJENZI HOSPITALI WILAYA**

RAIS John Magufuli ametoa Sh. bilioni 33.5 hospitali mpya 67 za wilaya...

**UKURASA WA 4**

**IMANI ASIA INAVYOMALIZA WANYAMAPORI AFRIKA -2**

WAPO wanaoamini kuwa ukimpa mwanafamilia au rafiki zawadi iliyotengenezwa...

**UKURASA WA 7**

**MAANDAMANO WANAFUNZI YATAWANYWA NA MABOMU**

MILIO ya mabomu ya machozi, jana ilisikika kwa zaidi ya mara 10 nje kidogo...




Wakili Peter Kibatala (kulia), anayemtetea aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, akisalimiana na Mawakili wa Serikali, katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Waenda Qatar kujifunza kulea

UKURASA 23



## Lugola aagiza nabii akamatwe

UKURASA 2

**MICHEZO** **YANGA YASAIDIWA KUIMALIZA ZESCO** UK.32 **MAONI, KATUNI** UK.6



Kaimu Balozi wa Marekani hapa nchini, Dk. Inmi Patterson (wa pili kulia), akionja uji uliotengenezwa kwa kutumia unga wa choroko na karoti na Magdalena Haule Njaidi (kushoto), ambaye ni mmoja wa wahitimu 20 waliopata mafunzo ya wiki 13, kupitia Taasisi ya Wanawake Wajasiriamali (AWE) kwa ufadhili wa serikali ya Marekani, wakati mahafali yao, jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Mkurugenzi wa Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo na za kati wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Consolata Ishebabi. **PICHA: JOHN BADI**

# Mjadala hukumu kesi ya Lissu

**Na Waandishi Wetu**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dar es Salaam imetupilia mbali maombi ya Mbunge wa zamani wa Singida Mashariki, Tundu Lissu ya kibali cha kutaka kufungua kesi kupinga uamuzi wa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kumvua ubunge wa jimbo hilo.

Mahakama hiyo iliyoketi chini ya Jaji Sirilius Matupa, imesema kwamba maombi hayo yangesikilizwa hadi mwisho na Lissu kushinda, Jimbo la Singida Mashariki lingekuwa na wabunge wawili kinyume cha Katiba.

Vile vile, alisema maombi ya Lissu yamechelewa kufunguliwa mahakamani hapo.

Alisema pia maombi ya Lissu hayatekelezeki kwa sababu mleta maombi alitakiwa kufungua kesi ya kupinga uchaguzi, badala yake ameleta maombi ya kutaka kupinga uamuzi wa Spika wa Bunge la Jamhuri na Muungano.

"Katika kupitia maombi haya mahakama yangu imepata wakati mgumu sana kwa sababu kilichotakiwa ni kupinga uchaguzi huo usifanyike, hata hivyo mlalamikaji hajafungua kesi mahakamani," alisema Jaji Matupa.

Akifafanua zaidi katika uamuzi wake, alisema mahakama hiyo ingeruhusu kusikilizwa maombi hayo mpaka mwisho, Jimbo la Singida Mashariki lingekuwa na wabunge wawili kitu ambacho ni kinyume na Katiba ya nchi.

Mbali na Spika Ndugai, mlalamikiwa mwingine ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG).

Mawakili wa walalamikiwa, Vicent Tangoh, Lucas Malunde na Abubakar Mrisha kwa nyakati tofauti walipinga mahakama kukubali ombi la Lissu.

Maombi hayo ya kupinga kuvuliwa ubunge yalifunguliwa na Lissu kupitia mawakili wake Peter Kibatala, Jeremia Mtobesya na Omary Msemo, chini ya hati ya dharura, kupitia kwa kaka yake, Wakili Alute Mughwai, ambaye amempa mamlaka ya kisheria kufanya hivyo.

Kwa mujibu wa ombi namba 18 la mwaka 2019, Lissu aliomba mahakama hiyo, impe kibali cha kufungua kesi ili mahakama hiyo itoe amri ya kumtaka Spika Ndugai ampe (Lissu) taarifa yake ya kumvua ubunge.

Pia aliomba mahakama hiyo itengue na kutupilia mbali uamuzi huo wa Spika Ndugai kumvua ubunge.

Mlalamikaji huyo aliiomba mahakama itoe amri ya kusimamisha kuapishwa kwa Mbunge mteule wa jimbo hilo, Miraji Mtaturu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika hati ya dharura, Lissu aliiomba mahakama hiyo isikilize na kutoa uamuzi wa maombi yake haraka kwa kuwa vinginevyo, Mtaturu ambaye Julai 19, mwaka huu alitangazwa na msimamizi wa uchaguzi wa jimbo hilo kushika wadhifa huo.

Lissu alidai kuwa ameathirika kwa kuwa atapoteza haki zake zote, kinga na maslahi yake yote yanayoambatana na wadhifa wake huo wa ubunge.

Uamuzi wa kumvua ubunge ulitangazwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai, Juni 28, 2019, wakati akiahirisha mkutano wa 15 wa Bunge.

MAONI YA WADAU

Wakizungumza baada ya hukumu hiyo, wadau wa sheria walisema Lissu bado ana haki ya kukata rufani.

INAENDELEA UK. 8

# Lugola aagiza nabii, askofu kukamatwa

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, ameagiza kukamatwa kwa nabii wa kanisa la Pentecostal Power Ministries, Eliya Mahela, pamoja na kumtaka askofu wake Samweli Mahela, kujisalimisha kituo cha polisi baada ya kukaidi agizo la serikali la kuwapigia wananchi kelele.

Nabii huyo amedaiwa kuweka 'flash' ya muziki usiku kanisani na kufungulia kwa sauti kubwa na viongozi wa kanisa na waumini wao kutokuwapo kanisani humo, huku wananchi wakipata usumbufu wa kukosa usingizi.

Lugola alitoa uamuzi huo jana jijini Dar es Salaam, baada ya kufanya ziara katika kanisa hilo lililopo Kimara Temboni, ambalo limekuwa likilalamikiwa kwa muda mrefu na wananchi kwa madai ya kufungulia sauti kubwa ambayo imekuwa kero mtaani hapo.

Alisema wamepokea malalamiko ya muda mrefu dhidi ya kanisa hilo na tayari serikali ilitoa maagizo, lakini limekiuka.

Waziri Lugola alisema haiwezekani mtu mmoja awasumbue wananchi kwa sauti kubwa na kwamba watu wa Mungu ndio wanaopaswa kuheshimu sheria na sio kuzivunja.

Alisema hata katika maandiko matakatifu yanasisisitiza kufuata sheria, haipendezi kuwapo na viongozi wa dini ambao wanakaidi na serikali haiwezi kuwafumbia macho.

"Haiwezekani ibada mnazofanya zisababishe kelele na kuwakera watu wengine, siamini na sitaki kuamini kwamba ukipiga kelele sana ndio mbingu zitafunguka na sitaki kuamini ukipiga kelele sana ndio Mungu atakusikia," alisema Lugola.

Vile vile, alisema siku hizi kumezuka mtindo wa baadhi ya viongozi wa dini kutumia makanisa au misikiti kama kichaka au mwamvuli wa kuvuruga na kuharibu haki ili wakiguswa waseme ni mambo ya kiroho.

"Vyombo vya serikali vilikuja katika kanisa hili na kuacha maelekezo kwa maandishi wameenda hadi polisi, lakini wamekaidi wananchi wameshafika hadi katika hili kanisa wanakuta muziki na mahubiri vinapigwa, lakini hakuna watu ameuacha muziki kwa sauti kubwa na kuendelea kuwakera watu hatuwezi kuwa na mtu mmoja anakaidi mambo ya serikali haiwezekani," alisema.

Aliongeza: "Ulijiona mjanja za mwizi ni arobaini, mtumishi wa Mungu uliwaambia wananchi waende kokote leo hautapona, nataka kujua jeuri yako ilikuwa inatoka wapi

INAENDELEA UK. 8

# JPM amwaga bil. 33.5/- ujenzi hospitali za wilaya

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

RAIS John Magufuli ametoa Sh. bilioni 33.5 hospitali mpya 67 za wilaya zinazoendelea kujengwa nchini ili kujenga wodi za kulaza wagonjwa.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alisema hayo jana wakati wa ziara ya siku moja ya kukagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chamwino inayojengwa kijiji cha Mlowa Barabarani.

Alisema Sh. bilioni 33.5 zinatarajia kutolewa kwa ajili ya kujenga wodi katika hospitali 67 mpya za wilaya zinaoendelea kujengwa na kila moja itapewa Sh. milioni 500.

"Baada ya kukamilika kwa majengo saba yaliyojengwa katika awamu ya kwanza, Rais Magufuli ametoa Sh. milioni 500 zitakazotumika kujenga wodi za kulaza wagonjwa, kama kituo cha afya kilitengewa kiasi kama hicho na kikajenga majengo kati ya matano hadi sita, naamini mtajenga majengo ya idadi hiyo," alisema.

Hata hivyo, alisema fedha hizo hazitatolewa hadi Sh. bilioni 1.5 za awali za ujenzi wa majengo saba kwa kila hospitali, majengo yake yakamilike kwa asilimia 100.

"Najua fedha zikitolewa mapema watu wanaweza 'kuhamisha goli' kuna baadhi wengine wanatumia fedha vibaya watataka kuzitumia hizi. Sasa sitazitoa mpaka majengo ya awali yakamilike kwa asilimia 100," alisisitiza.

Kuhusu ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chamwino, Waziri Jafo alisema ameridhishwa na hatua iliyofikiwa huku akiagiza kuhakikisha ujenzi wake unakamilika kwa wakati.

"Pamoja na kuchelewa hali mliyokuwa nayo nilipokuja awali ilikuwa mbaya na ya aibu. Tusingesimamia kwa karibu mpaka sasa kungekuwa hakuna kitu. Miaka ya nyuma watu ilishazoeleka mradi kama huu ambao tumepanga utekelezwe kwa miezi sita utakuta unafanywa kwa miaka mitatu," alisema.

Jafo alimtaka mhandisi mshauri kuhakikisha anasimamia kwa karibu umaliziaji ili kusiwe na kasoro.

Naye Mkuu wa Mkoa wa

INAENDELEA UK. 8

## Mugabe kuagwa kwa sherehe Jumamosi

**HARARE, Zimbabwe**

RAIS wa zamani wa Zimbabwe, Robert Mugabe (95), anayetarajiwa kuzikwa Jumapili hii (Septemba 14) nchini humo, ataagwa kwa sherehe.

Kwa mujibu wa taarifa zilizoripotiwa jana na vyombo vya habari mbalimbali vya kimataifa, kabla ya maziko, kutatanguliwa na sherehe za kumuaga zitakazofanyika Jumamosi.

Mwili wa kiongozi huyo wa kwanza wa Zimbabwe unatarajiwa kurejeshwa nchini humo kesho kutoka Singapore, alipokuwa akipatiwa matibabu.

Kwa mujibu wa mpwa wa marehemu Mugabe, familia haijafahamu kiongozi huyo wa zamani atazikwa wapi ingawa wanaamini mazishi yatafanyika katika makaburi ya Mashujaa ya Taifa, kama ilivyopangwa kabla ya kutimuliwa kwake madarakani.

Alisema tangu kuondolewa madarakani shujaa huyo wa zamani wa uhuru mwaka 2017, hali yake ya afya iliendelea kudhoofika.

Katika makaburi hayo ndipo alipozikwa mke wake wa kwanza, Sally Mugabe, eneo ambalo lilijengwa kwa msaada wa Korea Kaskazini.

Sally, alikuwa mmoja wa wanaharakati wa ukombozi wa Zimbabwe, aliyetazamwa na wengi hadi kifo chake kama Mama wa Taifa la Zimbabwe.

Taarifa zinaeleza baadhi ya ndugu zake wanataka azikwe kijijini alikozaliwa cha Kutama, kilichopo katika Jimbo la Magharibi la Mashonaland, kilomita 80 magharibi mwa mji mkuu, Harare.

Ijumaa iliyopita, Rais wa Zimbabwe, Emmerson Mnangagwa, alimtangaza Mugabe kuwa ni shujaa wa taifa na kutangaza siku za maombolezo kabla ya kuzikwa.

# Mwalimu mbaroni tuhuma za kumcharanga mapanga mpenzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MWALIMU Joseph Msafiri anayefundisha Shule ya Msingi Namagubu iliyopo Ukerewe mkoani Mwanza, anashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, kwa tuhuma za kumkata mapanga mpenzi wake, Neema Kabulu (19) mkazi wa Ukerewe na kumjeruhi vibaya.

Tukio hilo lilitokea juzi usiku maeneo ya Old Shinyanga mjini hapa, wakati mwalimu huyo, ambaye ni mkazi wa Kata ya Iselamagazi Shinyanga Vijijini akiwa na mpenzi wake wamelala kwenye nyumba ya wageni ili kesho yake kwenda kumtambulisha ukweni Iselamagazi Shinyanga Vijijini, ndipo ukatokea ugomvi kati yao.

Kamanda wa Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, Richard Abwao, alisema kwamba mwalimu huyo alimkata mapanga mpenzi wake maeneo ya usoni, tumboni, na mkono wa kulia, hivyo kukimbizwa kupatiwa matibabu kwenye hospitali ya rufani ya mkoa huo, na kuwa hali yake si ya kuridhisha.

Abwao alisema Mwalimu Msafiri alikwenda na mpenzi wake kwa ajili ya kumtambulisha kwa wazazi wake, lakini ukatokea ugomvi kati yao.

"Kwenye eneo la tukio yalipotokea mapigano hayo, tulikuta panga lililokuwa limetumika kumshambulia mwanamke huyo pamoja na nguo zenye damu," alisema Abwao.

Alisema chanzo cha ugomvi huo ni wivu wa kimapenzi, kutokana na mwalimu huyo kumtuhumu mpenzi wake kuwa siyo mwaninifu kwenye mahusiano yao.

Aidha, alisema Jeshi la Polisi mkoani humo linamshikilia mwalimu huyo na kwamba taratibu zingine zikishakamilika atafikishwa mahakamani.

## Ujerumani yamwaga bil. 33/- kuboresha afya

**Na Gwamaka Alipipi**

BENKI ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) imeipatia Serikali ya Tanzania msaada wa Euro milioni 13 (Sh. bilioni 32.74) zitakazosaidia kuboresha afya ya uzazi na watoto wachanga pamoja na kukinga maambukizo ya virusi vya Ukimwi VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto katika mikoa mitano.

Hafla ya kutiwa saini kwa mkataba huo ilifanyika jana jijini Dar es Salaam kati ya Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Doto James na Mkurugenzi wa KfW Tanzania, Annika Calov.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa halfa hiyo, James alisema mradi huo ulianza mwaka 2012 kwa KfW kutoa Euro milioni 13 (Sh. bilioni 25.5, awamu ya pili ilianza mwaka 2016 kwa kutoa Euro milioni 20 ( Sh. bilioni 48.2).

James alisema jumla ya msaada uliotolewa na serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani tangu mradi ulipoanza hadi sasa ni Euro milioni 46 (Sh. bilioni 115.86).

Mkurugenzi wa KfW, Colov, alisema wanafahamu umuhimu wa kuokoa maisha ya mama na mtoto ndiyo sababu wametoa msaada wa kiasi hicho cha fedha.

Alisema serikali ya Ujerumani imekuwa ikitoa misaada kwa serikali ya Tanzania tangu zamani katika nyanja za elimu, afya, nishati na maliasili.




# Imani Asia inavyoangamiza wanyamapori Afrika -2

**Na Salome Kitomari**,

aliyekuwa THAILAND

**IMANI na utamaduni wa watu wa Bara la Asia imedaiwa kuwa kichocheo kikubwa cha biashara ya bidhaa za malighafi zitokanazo na wanyamapori ambazo nyingi hutolewa bara la Afrika, ikiwamo Tanzania. Katika sehemu ya kwanza ya ripoti hii, ilieleza mambo yanayochangia. Leo tunaendelea na sehemu ya pili na ya mwisho...**



Mnunuzi wa bidhaa za wanyamapori akipima uhalisia wa bidhaa hizo kama alivyokutwa na mpiga picha wetu katika soko la Amulet, lililopo Jiji la Bangkok, Thailand. Soko hilo ni maarufu kwa bidhaa haramu na halali za wanyamapori na hutembelewa na maelfu ya watalii kutoka Asia. .

## ZAWADI

Wapo wanaoamini kuwa ukimpa mwanafamilia au rafiki zawadi iliyotengenezwa na mazao ya wanyama hao kama ngozi, meno, pembe au mfupa, ni kuashiria thamani na utajiri.

Vile vile, wengine hutumia magamba ya kakakuona kutengeneza urembo, huku tiger (mnyama aina ya chui) wakitumia kwenye nyumba za matajiri na kifalme kuonyesha ukuu wao.

Kwenye makazi ya watu mbalimbali wanapamba vinyago vilivyotengenezwa kwa kutumia meno ya tembo na pembe za faru, ambavyo huuzwa kwa fedha nyingi, na wenye kuhitaji hununua kwa gharama yoyote katika masoko halali na haramu.

## UTAFITI KWA WALAJI

Utafiti wa walaji wa mwaka 2018, kati ya watu kumi waliohojiwa ambao ni wanunuaji na watumiaji kwa miezi 12 iliyopita, ulibainisha kuwa nchini China watumiaji wa bidhaa za tembo asilimia 4.01 ni vya tofauti, asilimia 3.86 waliamini katika imani za kiroho na asilimia 3.79 waliamini katika urembo.

Kwa pembe za faru, asilimia 3.49 wanaamini inaleta afya njema na maisha mazuri, asilimia 3.40 inaponya kutoka kwenye maradhi mbalimbali na asilimia 2.95 waliamini kwenye utajiri, mafanikio na kupata nafasi kubwa.

Kwa upande wa kakakuona, asilimia 4.14 waliamini inaponya maradhi mbalimbali, 3.72 inaleta afya njema na maisha mazuri na asilimia 2.74 inaongeza nguvu za kiume.

Kwa upande wa tiger (chui), asilimia 4.78 wanaamini ni kitu cha tofauti, asilimia 4.25 wanatumia kwa ajili ya kuponya maradhi na asilimia 3.95 kupata afya njema.

## VIETNAM

Upande wa bidhaa zinazotokana na tembo, asilimia 3.77 waliamini ni uzuri au urembo, asilimia 2.65 wanaamini ni bidhaa adimu na asilimia 3.58 wanaamini ni nzuri kununua kwa kuwa ni zawadi ya thamani nzuri kutumia nyakati za likizo.

Kwa pembe za faru, asilimia 3.85 wanaamini ni bidhaa adimu, asilimia 3.51 wanaamini inajenga uhusiano mzuri wa kibiashara na asilimia 3.41 wanaamini inasafisha mwili.

Kwa upande wa kakakuona, asilimia 3.40 wanaamini inaongeza ubora wa dawa nyingine, asilimia 3.38 inaleta afya njema na asilimia 3.37 wanaamini nyama ya kakakuona inaongeza afya njema.

## THAILAND

Waliohojiwa asilimia 94 walisema wanatumia bidhaa za meno ya tembo kwa kuwa ni kitu cha tofauti na thamani kubwa, asilimia 88 walisema inaleta matumaini na bahati na asilimia 79 walisema inawalinda dhidi ya adui na majanga.

Kwa upande wa tiger, asilimia 91 walisema bidhaa zake ni adimu na za thamani, asilimia 83 walisema zinatoa ulinzi dhidi ya adui na asilimia 80 walisema inawapa matumani na bahati kwenye maisha.

## ZINAZOONGOZA KWA MATUMIZI

Oranop anasema nchi zinazoongoza kwa matumizi ya bidhaa haramu za wanyamapori kama tembo, tiger (chui), kakakuona na faru ni China, Vietnam na Thailand.

USAID Wildlife Asia imebaini kuwa Thailand ndiyo njia kuu ya kupitisha bidhaa hizo za tembo, tiger, kakakuona na faru zikielekea nchi za Vietnam na China, huku kukiwa na matumizi makubwa ya bidhaa hizo.

Anasema uchambuzi wa mwaka 2017 uliofanywa na USAID Wildlife Asia, ulibaini kuwa wananchi wa nchi hizo ndiyo wanafanya masoko ya bidhaa hizo kuendelea kuwapo licha ya serikali kupiga marufuu, lakini zinafanyika kwa njia haramu.

Mtaalamu wa Mawasiliano ya kupunguza mahitaji ya walaji kupitia kubadilisha tabia, Wanweena Tangsathianraphp, akiwasilisha mada ya matumizi na mahitaji ya bidhaa zitokanazo na wanyamapori bara la Asia, anasema uchambuzi wa mwaka 2017 umebainisha asilimia ya wanunuzi na watumiaji wa bidhaa hizo kwa kila nchi.

Uchambuzi huo umebainisha kuwa nchi ya China inaongoza kwa uhitaji na matumizi ya bidhaa hizo, akitaja viwango kwa kila bidhaa kuwa ni tembo (asilimia 16), faru (asilimia 16), kakakuona (14) na tiger (asilimia 12).

Watumiaji wa bidhaa hizo ni tembo (asilimia 10), faru (asilimia 8), kakakuona (asilimia 7) na tiger (asilimia 4), huku wanunuzi ikiwa ni tembo (asilimia 18), faru (asilimia 13), kakakuona (asilimia 13) na tiger (asilimia 13).

Kwa Thailand, watumiaji wa tembo ni asilimia mbili na tiger asilimia moja, huku wanunuzi ikiwa ni asilimia tatu kwa kila mnyama.

Vietnam matumizi ya tembo ni asilimia 18, faru asilimia 10 na kakakuona asilimia 8, huku watumiaji ni asilimia 13 ya tembo, asilimia 5.7 ya faru na asilimia 5.9 ya kakakuona, pamoja na waliotaka kununua ni tembo asilimia 12, faru asilimia nane na kakakuona asilimia saba.

Alisema USAID Wildlife Asia imesaidia kupunguza matumizi kwa kutumia mawasiliano, kuhamasisha na uraghibishi, wa namna ya kubadilisha matumizi na kujenga desturi mpya za matumizi ya bidhaa za wanyamapori.

Alisema licha ya sheria kupiga marufuku matumizi na biashara haramu ya bidhaa za wanyamapori, lakini inafanyika kwa usiri mkubwa nchini Thailand, huku China kukiwa na maeneo ambayo yameruhusiwa kuuza bidhaa hizo.

## MBINU KUBADILI IMANI

"Kubadili imani, utamaduni na maisha ya watu waliyoyazoea siyo kazi rahisi, tunatumia mbinu mbalimbali kuwasiliana nao kupitia ujumbe kwa simu na mitandao mingine, mabango na mikutano, tunaamini ni mabadiliko ya taratibu kwa kuwa wamezaliwa na kukuta zinatumika na wanaendelea kutumia hadi sasa," alifafanua.

Tangsathianraphap anasema mbinu zinazotumika kwenye mpango wa kubadilisha tabia kwa kuchambua kinachowasukuma kutumia bidhaa hizo, historia, hatua za mabadiliko ya tabia, thamani na uelewa wa wanachotumia na kisha kuweka uelewa mpya kwa ajili ya kuleta mabadiliko kwenye tabia za awali.

Anasema USAID Asia imekuja na muundo huo baada ya kubaini kuwa wanaharakati wamejikita zaidi kwenye usambazaji na usimamizi wa mazao ya wanyamapori, lakini hawajazungumza kwa kina mzizi wa watumiaji au walaji ambao wanasababisha soko kuendelea kuwapo.

Anasema kampeni inayofanyika inalenga kuelewesha wananchi kwa kuwa uchambuzi wa USAID Asia mwaka 2017, umebaini kuwa biashara hiyo inaendelea kwa kuwa wanunuzi na walaji halisi hawajafikiwa.

Anasema utafiti wa mwaka 2018 kuhusu walaji wa bidhaa za wanyamapori, ulionyesha kuwa elimu ya uhifadhi haikuwafikia watumiaji wa bidhaa hizo na hivyo kuendelea kuongeza uhitaji sokoni.

Pia wanatumia mitandao ya kijamii na teknolojia kuwafikia wananchi wengi kwa wakati mmoja kuhusu umuhimu wa kuacha kutumia bidhaa hizo.

Takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la udhibiti wa dawa za kulevya na uhalifu (UNODC) za mwaka 2017, kwa Bara la Asia zimeonyesha kulikuwa na tiger 100,000 katika karne ya 20 na sasa wamebakia 4,000 kati yake 200 wapo Thailand.

Katika karne hiyo kulikuwa na tembo 300,000, lakini kwa sasa wamebaki 3,000 na kwa imani za ukanda huo wanyama hao hutumiwa kwa shughuli za kibinadamu na wananchi wanaruhusiwa kuwafuga.

Mwakilishi wa Shirika la Kudhibiti Usafirishaji wa Wanyamapori Asia (Traffic), Monica Zavagli, alisema biashara ya wanyamapori inahusisha watu wenye mtandao mkubwa na wenye fedha nyingi ambazo huzitumia kununua nyara hizo.

"Ni biashara kubwa ambayo inatumia zaidi ya Dola za Marekani bilioni tisa hadi 30 kwa mwaka, mtandao huu unatumia taasisi za kifedha kuhamisha fedha na benki zina uwezo wa kuchunguza kwamba fedha hizo zinatokana na nini kama zinahusisha ujangili," alisema.

Alisema Tanzania imefanya vizuri kuwa na sheria kali, lakini jitihada zaidi zinahitajika katika kushirikisha taasisi za fedha, kwa kufuatilia mali na mienendo yao kama fedha hizo zinahusisha biashara hiyo itasaidia kumaliza mtandao huo," alisema.

Mkuu wa USAID Asia, Craig Karkpatrick, alisema ripoti ya polisi wa kimataifa imeonyesha kuwa biashara haramu ya mazao ya wanyamapori ipo na inafanyika kwa kiasi kikubwa.

"Biashara hii haramu inaharibu wanyamapori na vizazi vyao, inapunguza idadi yao, inaharibu uoto wa asili na ikolojia, ni uhalifu wa mazingira, inaharibu utawala wa sheria, inachangia ongezeko la rushwa na utakatishaji fedha, ina kuza mitandao ya kihalifu duniani, ni eneo muhimu sana linalohitaji kuunganisha nguvu kupambana nalo," alisema.

## HABARI KITAIFA

# PM awavutia Cuba kuwekeza Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewakaribisha wawekezaji kutoka Cuba kuja nchini kuwekeza kwenye kilimo cha miwa.

Majaliwa alisema hayo jana katika ofisi yake, Bungenio mjini Dodoma, alipokutana na kufanya mazungumzo na Naibu Waziri wa Kwanza wa Mambo ya Nje wa Jamhuri ya Cuba, Marcelino Medina Gonzalez.

Katika mazungumzo hayo, Waziri Mkuu aliishukuru serikali ya Cuba kwa ushirikiano mzuri inaoutoa kwa serikali ya Tanzania katika kuboresha maendeleo ya jamii.

Waziri Mkuu alisema serikali ya Cuba imepiga hatua kubwa katika uzalishaji wa sukari, hivyo akawakaribisha Wacuba kuja nchini washirikiane na serikali ya Tanzania katika kuongeza uzalishaji wa sukari kwa kuboresha kilimo cha miwa na kuanzisha viwanda vya bidhaa hiyo.

Kadhalika, Waziri Mkuu alisema serikali itaendelea kuimarisha ushirikiano uliopo kati yake na Cuba kwa kuwa nchi hiyo ni moja ya nchi zenye ushirikiano wa muda mrefu na Tanzania katika masuala ya kisiasa, kijamii, kiafya na kiuchumi.

"Mfano katika sekta ya afya, madaktari wengi kutoka Cuba wamekuwa wakija Tanzania kutibu wagonja waliokuwa na maradhi makubwa na pia serikali ya Cuba imekuwa ikitoa fursa kwa Watanzania kwenda kusomea fani ya udaktari," alisema.

Majaliwa pia aliwakaribisha Wacuba kuja kuwekeza katika sekta ya utalii hususani wa fukwe kwa sababu Tanzania ina fukwe nzuri. Alisema mji mmoja wa Varadero wa nchini Cuba unaingiza zaidi ya watalii milioni moja kwa mwaka na unategemea kivutio kikubwa kimoja tu cha ufukwe ambao una urefu wa kilomita 22.

Kuhusu ofisi ya ubalozi wa Tanzania iliyofunguliwa nchini Cuba, Waziri Mkuu alisema imesaidia kurahisisha mawasiliano kwa sababu awali kulikuwa na balozi mmoja tu ambaye alikuwa akiwakilisha nchi ya Cuba nchini Tanzania.

Gonzalez kwa upande wake alisema serikali ya Cuba itahakikisha uhusiano wake na Tanzania unakuwa endelevu.

Pia alipongeza jitihada zinazofanywa na serikali katika kuboresha maendeleo pamoja na kukuza uchumi.



Mwendesha guta akiwa amesheheni mzigo mkubwa uliokuwa ukisababisha usumbufu kwa watumiaji wengine wa barabara katika eneo la Mburahati, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Malipo kodi ardhi sasa kwa Airtel Money

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amezindua huduma ya ulipaji kodi ya pango la ardhi kwa kutumia mtandao wa simu ya mkononi kupitia Airtel Money.

Uzinduzi wa ulipaji kodi unarahisisha huduma hiyo kwa wamiliki wa kufanya malipo kupitia mtandao huo wa simu bila kwenda ofisi za ardhi.

Akizungumza jana jijini Dodoma wakati wa kuzindua huduma hiyo, Waziri Lukuvi alisema ubunifu wa serikali kufanya malipo ya ankara za serikali kwa kutumia mfumo wa GePG umerahisisha malipo ya tozo mbalimbali za serikali ikiwamo kodi ya pango la ardhi.

Alisema mfumo huo wa malipo ya serikali umeibuka na faida nyingi kama vile kuweka kumbukumbu vizuri, kulipa kwa muda, kupunguza upotevu wa mapato ya serikali, kuondoa mianya ya rushwa na kuongeza mapato ya serikali.

"Tunayo furaha kubwa kwa mara nyingine kutangaza kuwa kampuni ya simu ya mkononi ya Airtel imerahisisha malipo ya kodi ya pango la ardhi kupitia Airtel Money. Hii ni huduma rahisi na itapunguza kero nyingi wakati wa kufanya malipo" alisema Lukuvi.

Aliitaka Airtel kusaidia kuhimiza wananchi wanaotumia mtandao wa simu wa kampuni hiyo kulipia tozo mbalimbali za serikali ikiwamo kodi ya pango la ardhi kwa Airtel Money kwa kuwa inarahisisha kufanya malipo mahali popote.

Waziri Lukuvi alisema lengo la wizara yake kwa sasa ni kutaka kutumia kampuni za simu kuwakumbusha wananchi kulipia kodi ya pango la ardhi kupitia ujumbe wa simu badala ya utaratibu uliopo sasa wa kuwafuata wadaiwa.

"Sasa ofisi za ardhi za kulipia kodi ya pango la ardhi ziko viganjani mwenu. Mnaweza kulipia bila kwenda katika ofisi za ardhi," alisema Lukuvi.

Mkurugenzi wa Mawasiliano wa Airtel, Beatrice Singano, alisema kuunga mkono juhudi za serikali ni moja ya ajenda kubwa ya Airtel na kubainisha kuwa kampuni hiyo inaelewa umuhimu wa kukusanya kodi na kulipa malipo ya serikali kwa kuwa ndiyo njia pekee ya kuleta maendeleo.



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mil. 500/- zichochee ujenzi wa hospitali

**KATIKA** toleo letu la leo tumechapisha habari ikieleza kuwa ujenzi wa hospitali za wilaya 67 zinazoendelea kujengwa, umeongezewa nguvu, baada ya Rais John Magufuli kutoa fedha za ziada kwa ajili ya kuzikamilisha.

Katika kuchochea na kuharakisha ujenzi huo, Rais Magufuli ametoa Sh. milioni 500 kwa kila hospitali hizo mpya za wilaya zinazoendelea kujengwa nchini ili kujenga wodi za kulaza wagonjwa.

Hayo yalibainishwa jana na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, alipofanya ziara ya kukagua ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Chamwino inayojengwa kijiji cha Mlowa Barabarani mkoani Dodoma.

Jafo alisema jumla ya Sh. bilioni 33.5 zinatarajia kutolewa kwa ajili ya kujenga wodi katika hospitali hizo mpya za wilaya zinaoendelea kujengwa ambapo kila mmoja itapewa Sh. milioni 500.

Kwa mujibu wa Waziri Jafo, baada ya kukamilika kwa majengo saba yaliyojengwa katika awamu ya kwanza, Rais Magufuli ametoa kiasi hicho cha fedha zinakazotumika kujenga wodi za kulaza wagonjwa.

Hata hivyo, alisema fedha hizo hazitatolewa hadi zile za awali za ujenzi wa majengo saba ambazo zilitolewa Sh. bilioni 1.5 kwa kila hospitali, majengo yake yakamilike kwa asilimia 100.

Utoaji wa fedha hizo kwa ajili ya kujenga wodi za wagonjwa ni hatua nzuri na muhimu katika suala zima la uboreshaji wa sekta ya afya nchini. Umuhimu huo unatokana na sababu kuwa haiwezekani hospitali ikajengwa na kuonekana imekamilika bila kuwa na wodi za kulaza wagonjwa.

Kwa lugha nyingine tunaweza kusema kuwa ili kuwa na hadhi ya kuitwa hospitali, lazima mambo ya msingi yakamilishwe ikiwamo wodi za kulaza wagonjwa, maabara, vifaa tiba na dawa pamoja na miundombinu nyingine.

Kutolewa kwa kiasi hicho kikubwa cha fedha, tunaamini kuwa kutachochea kwa kiasi kikubwa kukamilika kwa ujenzi wa hospitali hizo ambazo zina umuhimu na tegemezi kwa wananchi wengi katika ngazi ya wilaya.

Tunasema hivyo kutokana na wananchi wengi kuzitegemea zaidi hospitali za wilaya kwa huduma kubwa za matibabu ambazo haziwezi kupatikana katika zahanati na vituo vya afya ngazi ya vijiji na kata.

Sekta nyingine muhimu za jamii pia zina mahitaji makubwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wananchi, hivyo Rais Magufuli amefanya hivyo kwa kuthamini umuhimu wa sekta ya afya.

Kutokana na hilo, kuna kila sababu kwa wahusika na wenye dhamana kuhakikisha kwamba wanazifuatilia na kuzisimamia fedha hizo ili zitumike kwa lengo lililokusudiwa la kukamilisha ujenzi wa hospitali hizo 67 za wilaya.

Kumekuwapo na matukio ya ufujaji, wizi na ubadhirifu wa fedha za miradi kadhaa ya jamii nchini ikiwamo ya sekta ya afya, hivyo wakuu wa wilaya, wakurugenzi na wakuu wa mikoa husika watatimiza wajibu wao kwa kuhakikisha kuwa hakuna hata senti moja itakayochakachuliwa katika ujenzi wa hospitali hizo. Kwa watakaodiriki kuzichakachua wasionewe aibu badala yake wakamatwe na kushtakiwa kwa makosa ya kuhujumu uchumi.

Ni matarajio yetu kwamba fedha zilizotolewa na Rais Magufuli zitasaidia kuchochea ujenzi wa hospitali hizo ili zitoe huduma za afya kwa wananchi wengi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Idara ya Matangazo:** 0745 700710
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Serikali isimamie maagizo yake magari ya wanafunzi

Na Salome Kitomari

**KWA** muda sasa, serikali iliagiza magari yote yanayobeba wanafunzi yapakwe rangi ya njano ili kutambulisha na kuwezesha wanafunzi kusafiri kwa urahisi.

Utekelezaji wa jambo hilo ulianza baada ya kutokea ajali ya wanafunzi 32 wa Luck Vicent mkoani Arusha, waliofariki baada ya gari lao kupata ajali wakielekea Manyara, kufanya mtihani wa kujipima.

Toka wakati huo, serikali ilielekeza magari ya wanafunzi kupakwa rangi ya njano kwa mujibu wa sheria.

Hiyo ilitokana na wengi kutumia magari ya kawaida kama 'Noah' na daladala ambazo hukodishwa kwa muda mfupi kubeba wanafunzi.

Magari hayo ya kukodishwa huendeshwa na madereva wasio na utaalamu wa kuendesha wanafunzi, jambo ambalo kimsingi ni la hatari.

Baada ya maelekezo hayo mabadiliko yalitokea kwa magari kupakwa rangi na hivyo kutambulika kirahisi kuwa ni ya kubeba wanafunzi.

Hata hivyo, bado kuna magari ya kawaida yanayotumiwa kubeba wanafunzi kwa baadhi ya shule.

Hivi sasa shule zimefungwa kwa wiki mbili, matarajio ni kufanya marekebisho mbalimbali kwenye shule, ikiwamo kuhakikisha kunakuwa na magari na madereva waliofundishwa namna ya kuendesha magari ya wanafunzi.

Ni vyema serikali ikafuatilia kwa karibu utekelezaji wa maagizo yake likiwamo la shule kuwa na magari yake ya kubeba wanafunzi, kuliko kila shule kujiamulia itakavyo.

Kuna changamoto kubwa ya wanafunzi kubanana kupita kiasi katika baadhi ya magari, kutokana na uhaba wa magari hayo kwa baadhi ya shule licha ya wazazi kulipa viwango vikubwa vya ada, ambavyo huongezwa kila wakati.

Wazazi hukubaliana na ongezeko la fedha za usafiri au ada kwenye shule binafsi kwa sababu wanataka watoto wao wapate kilicho bora, ikiwamo kusafiri vizuri na kufikishwa shuleni kwa wakati.

Tofauti na matarajio ya wazazi, shule huwa na malengo ya kufanya biashara, na ndiyo mwanzo wa wanafunzi kujazwa kwenye mabasi au 'Noah.'

Tatizo jingine ni ubovu wa magari hayo kwani kwa shule ambazo zimejitahidi kuwa na magari yao, mengine ni yaliyokuwa yanatumika kwenye usafiri wa umma na sasa yamegeuzwa kubeba wanafunzi.

Matokeo yake huharibika mara kwa mara na kusababisha wanafunzi kuteseka njiani.

Kutokana na adha hiyo wanafunzi wanachelewa kuchukuliwa vituoni, kufika shuleni na kurudishwa nyumbani.

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na shule binafsi lakini eneo la usafirishaji limesahaulika na ambalo ni muhimu sana kwa maslahi ya wanafunzi.

Ni vyema shule zikajipanga kuhakikisha suala la usafiri halina ubabaishaji. Serikali ifanye ufuatiliaji wa mara kwa mara ili kuondoa usumbufu kwa wazazi na wanafunzi.

Kasi ya kutoa maelekezo na kufuatilia ajali inapotokea inapaswa kwenda sambamba na ufuatiliaji wa utekelezaji wa maagizo hayo, kwamba magari yote yanayobeba wanafunzi yamepakwa rangi ya njano na kutambulisha kisheria na yanakaguliwa mara kwa mara.

Ukaguzi wa mara kwa mara utaondoa usumbufu au uwezekano wa kutokea ajali, kwani kutakuwa na magari sahihi ya kusafirishia wanafunzi na siyo kuwa na magari yenye uhakika wa kuondoka lakini hakuna uhakika wa kufika.

Aidha, ni muhimu kukawa na marufuku kwa ya magari mengine kutumika kubeba wanafunzi, kwa sababu madereva wa kubeba wanafunzi wanapaswa kuwa na maadili na waliofundishwa kwa ajili ya kazi hiyo.

Kutumia magari ya daladala mathalani si jambo jema kwa sababu ya lugha isyo ya staha inayotumiwa na madereva ama makondakta wao lakini aina ya muziki unaopigwa pia kwenye magari hayo unawafanya wanafunzi wadogo kuigiza mambo yasiyo sahihi kwa umri wao.

Ikiwa gari asubuhi na jioni linapiga nyimbo ambazo pengine zimekataliwa na serikali, upo uwezekano wa wanafunzi kukariri hilo.

Hata hivyo, kwa madereva na makondakta waliofunzwa maalumu kwa kazi hiyo hawawezi kuweka nyimbo hizo au kutumia lugha mbaya.

**HABARI KITAIFA**

## Balozi ataka wanawake kuchangamkia fursa

**Na Rahma Kisilwa**

KAIMU Balozi wa Marekani, Dk. Inmi Patterson, amewataka wanawake kuchangamkia fursa za kiuchumi kwa kushiriki katika mafunzo ya ujasiriamali yatakayowawezesha kufikia malengo yao.

Wito huo aliutoa jana jijini Dar es Salaam, wakati akizungumza na wajasiriamali wanawake 20 waliomaliza mafunzo ya miezi mitatu ya ujasiriamali yaliyoandaliwa na Taasisi ya Wanawake Wajasiriamali (AWE) chini ya Ubalozi wa Marekani.

Aidha, aliwataka wanawake walionufaika na mafunzo hayo kuwa mabalozi wa kutoa elimu kwa wajasiriamali wenzao ili kufikia lengo la kuwa na wanawake wenye ujuzi wa kutosha.

Alisema wanawake wana nguvu ya kuleta mabadiliko ya kiuchumi kwenye jamii kwa sababu wanapofanikiwa wanainua jamii na familia.

"Kipato cha mwanamke aliyefanikiwa kinanufaisha jamii, kulipa ada za watoto na huduma za afya, hivyo manufaa ya mafanikio yao kiuchumi yatasaidia vizazi vijavyo," Dk. Patterson alisema.

Mgeni rasmi katika hafla hiyo ambaye ni Mkurugenzi wa Viwanda Vidogo na Biashara kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, Consolatha Ishebabi, alisema AWE imedhamiria kuwapatia wanawake ujuzi, kupitia mtandao na kuwaonyesha njia wanazohitaji kugeuza mawazo yao kuwa uhalisi.

Jumla ya wahitimu watano katika mafunzo hayo ambao walifaulu vizuri walipatiwa Dola za Marekani 1,000 kila mmoja.

Baadhi ya wahitimu hao, waliishukuru AWE kwa kuwasaidia kupata mafunzo hayo na kwamba imewasaidia kukutana na wanawake wajasiriamali mbalimbali na kukuza biashara zao.

Taasisi ya AWE inasimamiwa na Serikali ya Marekani na kuwapatia wanawake wajasiriamali duniani kote rasilimali na maarifa muhimu ili kutimiza ndoto zao za kiuchumi.



Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein (katikati), akimzawadia mwanafunzi Ahmad Khamis Kassim wa Shule ya Sekondari ya Lumumba katika hafla ya kuwapongeza wanafunzi waliofaulu mitihani ya taifa ya kidato cha nne na sita pamoja kuwaandalia chakula cha mchana, katika viwanja vya Ikulu Mjini Zanzibar jana.. **PICHA: IKULU ZANZIBAR .**

# Maandamano ya wanafunzi yatawanywa kwa mabomu

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MILIO ya mabomu ya machozi, jana ilisikika kwa zaidi ya mara 10 nje kidogo ya mji wa Bomang'ombe, baada ya Jeshi la Polisi kutumia nguvu kuzima maandamano ya wanafunzi 400 wa Chuo cha Ualimu Moshi, zamani Mong'are.

Maandamano hayo yaliyokuwa yakitokea chuoni hapo kwenda katikati ya mji hadi Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, yalitumia takribani saa tatu, huku wanafunzi hao wakifunga barabara kwa mawe na kuzuia shughuli mbalimbali za kiuchumi ikiwamo usafirishaji, kushinikiza kurejeshewa zaidi ya Sh. milioni 78.1 za malipo ya ada.

Katika maandamano hayo, wanafunzi 12 waliokuwa wakishiriki kushinikiza kurejeshewa fedha hizo, walikamatwa na kushikiliwa na Polisi kwa saa kadhaa, hadi Mkuu wa Wilaya alipofika eneo hilo na kutoa amri waachiwe na kusikilizwa.

Polisi wakiwa na mabomu ya machozi na silaha za moto, walifika katika Kijiji cha Kambi ya Nyuki, Kata ya Bondeni, wakiwa na magari namba PT 3753 na lori aina ya Ashok Leyland na kukamata baadhi ya wanafunzi.

Wanafunzi hao waligomea kuingia katika vyumba vya mitihani ya kuhitimu masomo yao na wengine ambao walikuwa wanafanya mitihani ya muhula iliyokuwa inaanza jana hadi Septemba 12, mwaka huu.

Katika kushinikiza huko, wanafunzi hao walikwenda barabarani na kulala chini, wengine kupanga mawe na wengine kuzuia magari kupita, wakitaka serikali kuingilia kati na kuweleza hatima ya fedha zao.

Wanafunzi wanaodaiwa kulizwa fedha hizo na mhasibu wa chuo hicho, wamo wale wanaotarajia kufanya mitihani ya taifa ya kada hiyo ngazi ya cheti ya 'Grade IIIA.

Akizungumza wakati wa maandamano hayo, kabla ya kutawanywa kwa mabomu, Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Ualimu Moshi (Urom), Herman Tarimo, alisema walibaini kuwapo kwa udanganyifu huo baada ya kufanyika ukaguzi wa ndani Novemba, mwaka jana katika miamala 487 ya kibenki.

"Hizo 'bankslip' (stakabadhi za malipo benki) ni za benki ya CRDB zilizotolewa na Chama cha Akiba na Mikopo (Saccos) cha Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) ambazo zilizozalishwa na mashine ya wakala yaani KKKT Saccos, chini ya CRDB ambazo zinaonekana kuwa katika makundi fulani ya mfanano.

"Kuna kiasi cha Sh. 78,165,000 zilizopelekwa benki na wanachuo hao katika mwaka mmoja ila fedha zilizoingizwa benki ni Sh. 5,650,000. Katika fedha hizo Saccos ya Kanisa la KKKT waliingiza katika akaunti ya chuo Sh. 540,000,000 kwa kufuata kanuni za miamala walizopewa na benki ya CRDB."

Alisema chuo kimejaribu kuwasaidia wanachuo hao

INAENDELEA UK. 8

# Mafuta ya nywele yashusha mfumuko bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za vyakula ikiwamo mafuta ya nywele kwa kipindi cha mwaka ulioshia Agosti 2019, kumechangia kupungua kwa mfumuko wa bei wa Taifa hadi asilimia 3.6.

Bidhaa zingine zilizochangia kupungua huko ni mafuta ya taa, petroli, majiko ya gesi, gharama za kufanya ukarabati wa nyumba, bidhaa za usafi binafsi kama mafuta ya nywele.

Hayo yalielezwa jana na Kaimu Mkurugenzi wa Sensa ya Watu na Takwimu za Jamii kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu(NBS), Ruth Davison, alipokuwa akizungumzia mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Agosti, 2019.

Alisema mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Agosti 2019 umepungua hadi asilimia 3.6 kutoka asilimia 3.7 kwa mwaka ulioishia Julai, 2019.

"Hii inamaanisha kasi ya mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma kwa mwaka ulioishia Agosti 2019 imepungua ikilinganishwa na kasi iliyokuwapo kwa mwaka ulioishia Julai 2019," alisema.

Alibainisha kupungua kwa mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Agosti 2019 kumechangiwa hasa na kupungua kwa mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za vyakula kwa kipindi kilichoishia Agosti 2019 zikilinganishwa na bei za Agosti 2018.

Alitaja baadhi ya bidhaa zisizo za vyakula zilizopungua bei kwa Agosti 2019 zikilinganishwa na bei za Agosti 2018 ni na mafuta ya taa kwa asilimia 2.6.

Pia alisema petroli kwa asilimia 4.3, majiko ya gesi kwa asilimia 1.4, gharama za kufanya ukarabati wa nyumba kwa asilimia 1.7 na bidhaa za usafi binafsi kama mafuta ya nywele kwa asilimia 1.3. Davison alisema mfumuko wa bei wa bidhaa za vyakula baridi kwa Agosti 2019 umeongezeka hadi asilimia 3.7 kutoka asilimia 2.9 Julai, 2019.

Akizungumzia hali ya mfumuko wa bei kwa nchi za Afrika Mashariki kwa kipindi hicho, alisema kwa Kenya kwa mwaka ulioshia Agosti 2019 umepungua kwa asilimia 5 kutoka asilimia 6.27 kwa kipindi cha Julai, 2019.

"Kwa Uganda mfumuko wa bei kwa mwaka ulioishia Agosti 2019 umepungua hadi asilimia 2.1 kutoka asilimia 2.6 kwa mwaka ulioishia Julai 2019," alisema.

# Lugola aagiza nabii, askofu kukamatwa

INATOKA UK.2

na uhakika hii jeuri haitoki kwa Mungu, wewe hii jeuri umeipata wapi? Au unatumia kivuli cha kanisa na hili kanisa halijasajiliwa, hapo tu hujasajiliwa unakuwa hivyo ukisajiliwa si utapeleka spika kwenye nyumba za watu," alisema Lugola.

Waziri alimwagiza OCD kumkamata Nabii Mahela pamoja na kumtaka Askofu wake Samwel Mahela, kujisalimisha kituo cha polisi ili hatua zichukuliwe.

"Huyu nabii ni jeuri, OCD upo wapi kamata huyu mpeleke kituoni na kwa sababu ya heshima ya hawa waumini ningelifunga hili kanisa. Mtaendelea kusali hapa bila kuwa na vyombo vya muziki vya kizungu, mtaendelea kutumia vyombo vya asili mpaka mtakapopatiwa maelekezo na huyo askofu wenu Mahela ajisalimishe Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Kimara, aje kutoa maelezo," alisema.

Alisema agizo hilo la kulinda maslahi ya sauti ni la nchi nzima, hivyo kila mmoja anatakiwa kuweka nidhamu kwa wananchi na sio kuwasababishia kelele hadi wanashindwa kulala.

Wakati huo huo, Waziri Lugola, ametangaza kiama kwa wakuu wa polisi wa wilaya nchini ambao watashindwa kudhibiti kelele zinazolalamikiwa na wananchi.

Alitangaza hatua hiyo wakati alipofanya ziara kwenye baa ya Buscar LaVida, iliyopo Mbezi Chini, ambayo inalalamikiwa kusababisha kelele kwa wananchi nyakati za usiku na kushindwa kulala.

Waziri alisema amesikia kilio cha wananchi hao na kwamba tatizo hilo lipo katika maeneo mengi nchini.

Alisema amegundua tatizo hilo linasababishwa na OCD (Mkuu wa Polisi wa wilaya) kwa kuacha kuchukua hatua, huku wananchi wakiendelea kupata shida.

"Kuanzia sasa naanza kufa na ma-OCD wa wilaya, nikipatiwa taarifa na wananchi sehemu fulani ina kelele OCD ama zako, nasema tena ama zako nataka JPM awakute Watanzania roho zao zipo safi na sio kulalamika ama wanakosa amani."

Lugola aliwaomba wananchi wampe taarifa za watu wanaowapigia kelele na kuahidi kuchukua hatua kwa OCD ambaye atashindwa kutatua kero hiyo.

Mwanasheria wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Heche Suguta, alisema baa hiyo imejengwa katika eneo linalolindwa dhidi ya kelele na kwamba kufanya hivyo ni ukiukwaji wa sheria.

Alisena mmiliki wa baa hiyo hatakiwi kuongeza kiwango cha sauti cha juu kwa mujibu wa sheria.

Saguta akitoa maelekezo kwa kanisa, aliwataka kuacha mara moja kutumia vyombo vinavyosababisha sauti kutoka nje na kuwakera wananchi.

Alionya kwa yeyote atakayebainika kufanya kosa hilo adhabu yake ni kwenda jela kuanzia kifungo cha miaka miwili hadi saba au kulipa faini ya Sh. milioni mbili hadi Sh. milioni 10.

# Mjadala hukumu kesi ya Lissu

INATOKA UK. 2

Rais wa Chama cha Wanasheria Tanganyika (TLS), Dk. Rugemeleza Nshala, alisema wanakubali maamuzi ya mahakama lakini, Lissu bado ana haki ya kukata rufani kwa sababu hukumu inapotolewa na mtu akiwa hajaridhishwa nayo, ipo haki hiyo.

Mratibu wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, alisema lazima watu waelewe kwa nini kuna mihimili ya Mahakama, Bunge na Serikali.

"Lengo ni kuhakikisha kuna kuwa na check and balance (mgawanyo wa madaraka), chombo kikifanya sivyo, chombo kingine kije kusawazisha na chombo kilichopewa dhamana hiyo ni Mahakama ambayo inaweza kuingilia mahali popote," alisema.

Kuhusu hoja kuwa mahakama haiwezi kuingilia maamuzi ya Bunge, Olengurumwa alisema, hiyo ni hoja dhaifu kwa sababu muhimili huo ndiyo wenye kuweza kuingilia mahali popote.

"Yule ni Mbunge wa wananchi hajachaguliwa na Spika, wala Bunge, mahakama leo inasema haina mamlaka ya kutengua hoja ya Spika, sasa mtu akiona ameonewa aende wapi? Kwa sababu Mahakama ndiyo imepewa mamlaka ya kuingilia mahali popote ili kutenda haki.

"Kama hali ndiyo hii ina maana Mahakama siyo sehemu sahihi ya kwenda kudai haki kwa sababu inatuonyesha wazi kuwa inaogopa kuingia migogoro na mamlaka nyingine ambazo ni Bunge na Serikali," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema hukumu hiyo iliyotolewa ni kama imejichanganya.

"Hukumu imetolewa kama vile Lissu wakati akifungua kesi yake uchaguzi katika jimbo ulikuwa umeshafanyika, kwa sababu inasema kama Lissu anapinga, apinge uchaguzi wakati yeye alipinga kuvuliwa ubunge na baadaye alipinga kuapishwa kwa Mtaturu," alisema.

Kuhusu mahakama kutoingilia Bunge, Henga alisema Jaji amesahau kuwa mhimili huo unategemea mahakama.

"Mahakama ilikuwa na jukumu la kutenda haki, uamuzi umeamuliwa bila kufuata kesi ya msingi ilikuwa inasemaje," alihoji.

**MBOWE ANENA**

Akizungumza nje ya Mahakama jana baada ya hukumu hiyo, Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Freeman Mbowe, alisema Chadema na Lissu watarejea mahakamani haraka iwezekanavyo baada ya mashauriano yanayofanyika.

"Utaratibu ambao utakubalika baada ya mashauriano yatakayofanyika, Chadema kitatumia mfumo wa kisheria katika ngazi mbalimbali za mahakama kupigania haki kwenye suala la Lissu.

"Itoshe kusema...katika Mahakama kuna ngazi mbalimbali za kupata haki ile, kwa hiyo tutaendelea kutumia kila mfumo wa kimahakama kuhakikisha kwamba haki hiyo inaendelea kupiganiwa na kutafutwa.

Hivyo ni wazi kuwa Chama pamoja na Lissu, watarejea mahakamani, haraka iwezekanavyo, iwe kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa leo au kufungua kesi nyingine ya uchaguzi.

**SPIKA NDUGAI**

Bungeni jijini Dodoma, Spika Job Ndugai wakati ukiahirisha kikao cha jana cha Bunge, alilizungumzia suala hilo, akiwataka wabunge kuheshimu mamlaka na kuzingatia taratibu zilizowekwa.

Alisema waliokuwa na shaka kuhusu ubunge wa Miraji Mtaturu, sasa watambue ni Mbunge halali wa Singida Mashariki.

"Mambo haya ukiheshimu mamlaka, ukashirikiana na mamlaka huwezi kupata matatizo haya. Bahati mbaya Spika hawezi kutokeza kila wakati kujibu kila mtu anayeweka kwenye mitandao huko, na mimi ningekuwa najibu kila kinachosemwa huko sijui wangeweka wapi nyuso zao kwa sababu majibu yapo.

"Katika Bunge kama hili linaloendelea wewe una hali ya kawaida, si kwamba unaumwa sana, ni suala la kumjulisha tu Spika kwamba mimi niko hospitali naendelea na matibabu hivyo siwezi kuhudhuria mkutano huu wa 16 wa Bunge na cheti cha daktari wako unanitumia.

Hata ukipiga simu, hapo si taarifa umetoa, hata ukiandika meseji tu, hapo si taarifa umetoa! Kwa hiyo, hayo mengine yote unafanya, lakini kumwambia Spika tu hapana, nakuona tu huku huko, wapi. Mengine yote unafanya, lakini kuwasiliana na huyu hufanyi, haiwezekani.

"Itafika mahali watu wataruka na wewe, utaanza kupiga kelele ooh imekuwa, imekuwa, si uliyataka mwenyewe, taratibu unazijua, ni lazima waheshimiwa wabunge tufuate taratibu," Spika Ndugai alisema.

Alisema fomu za maadili ni lazima zijazwe na wabunge kwa sababu ni wajibu wa kisheria na kueleza kuwa hata Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, akiwa gerezani, alimwandikia kututaarifu kuwa asingeweza kuzijaza kwa kuwa alikuwa gerezani na alipotoka alizijaza, lakini Lissu hakufanya hivyo.

"Wewe unapuyanya na yako, huandiki, huwasilishi, huwasiliani, ukitoka una yako, unamtandika huyo huyo unayetakiwa kuripoti kwake, mambo hayaendi hivyo, katiba inakwambia mpe Spika nakala mbili," alisema.

Alisema kwa maoni yake, kilichomkuta Lissu ni cha kajitakia na hajaonewa na mtu bali amekiuka taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema kosa la Lissu linafanana na aliyekuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki, Joshua Nassari (Chadema) akibainisha kuwa hata chama chao hakikumpa taarifa kuhusu maendeleo ya afya yake na sababu za kutojaza fomu za maadili.

***Taarifa hii imeandaliwa na Hellen Mwango, Romana Mallya na Sanula Athanas, Dodoma**

# JPM amwaga bil. 33.5/- ujenzi hospitali za wilaya

INATOKA UK. 2

Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, alisema Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) linatarajia kuingiza umeme katika majengo hayo kuanzia wiki ijayo.

Awali, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Chamwino, Athuman Masasi, alisema walipokea Sh. bilioni 1.5 na mpaka sasa wametumia Sh. bilioni 1.438 tangu kuanza ujenzi huo Februari, mwaka huu.

"Hadi sasa fedha iliyobaki ni Sh. milioni 61 na ujenzi wa majengo haya umefikia zaidi ya asilimia 80 na tuko katika hatua za umaliziaji," alisema.

Alibainisha walishindwa kumaliza kwa wakati kwa sababu mfumo wa malipo ulifungwa, lakini kwa sasa umefunguliwa baada ya kufanyika kwa usuluhishi wa kibenki.

# Maandamano ya wanafunzi yatawanywa kwa mabomu

INATOKA UK. 7

kufuatilia kwa njia mbalimbali ikiwamo mahakamani lakini wanaona kuwa pia haki yao imechelewa na wanahisi kwamba hata watuhumiwa wakitiwa hatiani, fedha zao hawatazipata.

Baadhi ya wanafunzi waliozungumza na Nipashe, Barnabas Inyasi na Aron Alex kwa nyakati tofauti walieleza hawatakubali kuingia kwenye vyumba vya mitihani mpaka hapo watakapojua hatima yao, kwa kuwa watakapokuja kudai vyeti vyao vya taaluma watakwama kuvipata.

Baada ya Polisi kuzima maandamano hayo na kamati ya ulinzi na usalama ya Wilaya ya Hai kufika eneo hilo, mmiliki wa chuo hicho, Joseph Msaki, alimweleza Ole Sabaya kwamba wanafunzi hao waligoma jana asubuhi kuingia katika vyumba vya mitihani wakitaka kujua hatima yao kwa sababu watakapoondoka baada ya kumaliza mitihani, wakirejea wanajua watauliza ada. Kutokana na hali hiyo, Msaki alimwomba Mkuu huyo wa Wilaya kuwasaidia wanafunzi hao kupata fedha zao na awasihi warejee madarasani kuendelea na utaratibu wa mitihani.

Mkuu wa chuo hicho, Federick Akyoo, alimweleza Ole Sabaya kuwa wanafunzi hao ni kweli walimpa fedha mkononi mhasibu wao waliyemtaja kwa jina la Sarafina Septemba, mwaka jana na baadaye waligundua kutokuwapo kwa fedha hizo katika akaunti ya chuo Desemba, mwaka jana.

Baada ya maelezo hayo na kuwasikiliza wanafunzi hao, Ole Sabaya aliagiza kuitwa kwa maofisa wa CRDB na Chama cha Akiba na Mikopo kinachotuhumiwa ili wajibu maswali ya wanachuo hao lakini aliyeweza kutokea alikuwa ni Meneja wa CRDB, Tawi la Bomang'ombe, Philemon Pindapinda.

"Naagiza DAS (Katibu Tawala wa Wilaya), hawa ELCT Saccos kutoka Moshi waitwe na waje hapa chuoni kesho wao pamoja na CRDB katika kikao cha kamati ya ulinzi na usalama na tutatoa majibu hapa hapa baada ya kikao. Tunataka wanafunzi hawa wajue hatma yao kesho (leo). OCD (Mkuu wa Polisi wa Wilaya) msaidie DAS watu hao waje,"aliagiza Ole Sabaya.

HABARI MIKOANI

# Vigogo 14 wa polisi kuja Dar kuhudhuria mkutano

**Na Romana Mallya**

WAKUU 14 wa Jeshi la Polisi wanatarajia kuja nchini kuhudhuria mkutano mkuu wa mwaka wa 21 wa Wakuu wa Polisi Mashariki mwa Afrika (EAPCCO) utakaofanyika kwa siku sita.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, aliyasema hayo na kueleza kuwa mkutano huo ambao utafanyika jijini Arusha utaanza Septemba 15 hadi Septemba 20 na unatarajia kufunguliwa na Rais John Magufuli.

Misime alitaja nchi ambazo wakuu wa polisi watakaohudhuria kuwa ni kutoka Burundi, Comoro, Djibouti, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC), Eritrea, Ethiopia, Kenya, Rwanda, Shelisheli, Sudan Kusini, Tanzania na Uganda.

"Mkutano huu utaongozwa na kauli mbiu isemayo, 'Kuimarisha ushirikiano na ubunifu katika kupambana na ubunifu na uhalifu ndani na nje ya mipaka yetu," alisema.

Alisema katika mkutano huo, Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, (IGP) Simon Sirro, atakabidhiwa uenyekiti wa kuongoza Shirikisho la Wakuu wa Majeshi ya Polisi Mashariki mwa Afrika.

"Mkuu wa Jeshi la Polisi Sudan, Adil Bashair, ndiye atakayemkabidhi IGP Sirro uenyekiti baada ya muda wake wa kuongoza mwaka mmoja ulioanzia mwezi Septemba mwaka jana kuisha," alisema.

Alisema Septemba 15 kutafanyika kikao cha wakuu wa vitengo vya Interpol kutoka katika nchi hizo.

"Kwa siku mbili zitakazoanzia Septemba 16, vitafanyika vikao vya kamati tendaji ambavyo vinajumuisha kikao cha wakurugenzi wa upelelezi wa makosa ya jinai kutoka nchi hizo. Septemba 19 ndipo ufunguzi wa mkutano wa wakuu wa majeshi ya polisi utafanyika na siku itakayofuata kutakuwa na vikao vya mawaziri wa Wizara za Mambo ya Ndani," alisema.

Misime alisema Jeshi la Polisi limejiandaa katika maandalizi yote ya mkutano huo na kuwataka wananchi watakapoona viashiria vyovyote vya uhalifu wapige simu 0787668306.



Wananchi wakichagua sendozi zilizokuwa zikiuzwa kando ya Barabara ya Uhuru, eneo la Mnazi Mmoja, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# Watakiwa kufuatilia matumizi ya rasilimali

**Na Christina Haule,** MOROGORO

MKURUGENZI wa shirika lisilokuwa la kiserikali linalojishughulisha na masuala ya kutoa elimu kwa jamii Dira ya mkoani Morogoro, Erasmo Tullo, amewataka wakazi wilayani Kilosa kutambua kuwa kila mwananchi anapaswa kufuatilia na kusimamia kikamilifu matumizi ya rasilimali za umma (PETS).

Tullo alisema hayo kwenye mkutano wa hadhara mbele ya wakazi wa kijiji cha Mbamba kilichopo kata ya Kilangali wilayani Kilosa mkoani hapa, wakati shirika hilo likitoa elimu ya ufuatiliaji na usimamizi wa matumizi ya rasilimali za umma sekta ya elimu ya msingi sambamba na sekondari katika shule zilizopo ndani ya kata tano za wilaya hiyo kupitia ufadhili wa The Foundation For Civil Society (FCS).

Alisema kila mwenye dhamana ya kushikilia rasilimali za umma anapaswa kuwa muwazi ili kuwezesha taarifa hizo kujulikana kwa kila mwananchi.

Aidha, Tullo alisisitiza jamii kuzingatia uwepo wa uwazi, ushirikishwaji na uwajibikaji kwa lengo la kupatikana huduma bora katika maeneo yao.

Hata hivyo, Tullo aliwashauri wananchi wa wilaya hiyo, watapokuwa wanakaa kujadiliana na kuchangia masuala ya maendeleo ya sekta ya elimu wanapaswa kuangalia kama matumizi yanaendana na uhalisia wa fedha iliyokusanywa ili kuondokana na changamoto ya ubadhirifu inayorudisha nyuma maendeleo ya sehemu yoyote.

Tullo alisema, ikiwa watajenga nidhamu ya kukiheshimu walichochangia watajikuta wanaongeza kasi ya maendeleo kwenye vijiji vyao ikiwamo kuboresha madarasa chakavu, kuhakikisha chakula kinapatikana shuleni, kumalizia miradi viporo, kujenga vyoo vipya, madarasa na pengine nyumba za walimu vyote vikiwa katika hali ya ubora.

Msafiri Makau, mkazi wa kijiji cha Mbamba aliwataka wanakijiji wenzake kuona haja ya kuamka na kufuata elimu waliyopewa na Dira kwani kufanya hivyo kutawasaidia kupunguza au kumaliza kabisa changamoto za elimu kijiji kwao.

Shirika la Dira linaendesha mradi wa kufuatilia na kusimamia matumizi ya rasilimali za umma ukijikita kwenye sekta ya elimu ya msingi sambamba na sekondari katika kata tano za Wilaya ya Kilosa ambazo Kilangali, Zombo, Mabwerembere, Ulaya na Tindiga.

# TIC kupanua wigo mwakani

**Na Anthony Gervas,** MWANZA

KITUO cha Uwekezaji Tanzania Kanda ya Ziwa (TIC) kinatarajia kupanua zaidi wigo wake wa uwekezaji katika maonyesho ya biashara ya Afrika Mashariki mwakani.

Meneja wa Kanda ya Ziwa, Fanuel Lukwano, alisema hayo juzi wakati wa kufunga maonyesho hayo yaliyofanyika siku kumi katika viwanja vya Rock City Mall jijini hapa.

"TIC mwaka huo tumefanya vizuri hadi tukapata vikombe vya ushindi katika maonyesho haya ya biashara ya Afrika Mashariki, sasa tunatarajia kupanua wigo zaidi wa uwekezaji katika maonyesho ya biashara yajayo ya Afrika Mashariki 2020," alisema Lukwano.

Alisema TIC ni kituo cha uwekezaji na wakala wa kuratibu na kusimamia shughuli zote za uwekezaji pamoja na kuishauri serikali masuala yote yahusuyo uwekezaji.

Lukwaro alisema mojawapo ya shughuli zingine inazotakiwa kuzifanya ni kushirikiana na halmashauri zote kuibua na kutangaza fursa za uwekezaji zilizopo katika kila halmashauri, yakiwamo maeneo ya uwekezaji hususani ardhi ya kuwekeza.

# Ujerumani yasaidia vifaa wenye ulemavu

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI ya Ujerumani kupitia mradi wa kusaidia walemavu uitwao Bundesministerium fuer wirtschaftliche Zusammenarbeit und Entwicklung (BMZ), imetoa msaada wa vifaa mbalimbali kwa walemavu wa kata kumi katika Jimbo la Musoma Vijijini mkoani Mara.

Msaada huo ni huduma za matibabu bure katika Hospitali Teule ya Wilaya ya Rorya, KMT Shirati, vifaa maalum vya kujimudu kama fimbo nyeupe, baiskeli, vifaa vya kuongeza usikivu na vya shule kwa wanafunzi.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Musoma Vijijini, Charles Magoma, aliliambia gazeti hili kwa njia ya simu kuwa siyo mara ya kwanza BMZ kusaidia walemavu katika kata mbalimbali za halmashauri hiyo.

"Safari hii wamesaidiwa walemavu kutoka kata kumi ambazo ni Suguti, Bukima, Nyamrandirira, Bwasi, Murangi, Kiriba, Nyambono, Bugwema Makojo na Bugoji," alisema Magoma.

Magoma alisema mbali na msaada huo wa BMZ, halmashauri nayo imekuwa ikitoa mikopo kwa vikundi vya watu wenye ulemavu ili waendeshe miradi yao kwa ajili ya kujikimu kimaisha.

# Mbunge ataka matokeo ukamataji waendesha pikipiki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeelezwa kuwa moja ya chanzo cha ajali za barabarani ni waendesha pikipiki.

Hayo yalielezwa jana Bungeni na Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Yusuf Hamad Masauni, alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tabora (CCM), Emmanuel Mwakasaka.

Katika swali lake, alihoji waendesha pikipiki nchini wamekuwa wakikamatwa na askari wa usalama barabarani mara kwa mara kwa tuhuma za makosa mbalimbali, ukamataji wa waendesha pikipiki umefanikiwa kwa kiasi gani.

Akijibu swali hilo, Masauni alisema mwaka 2016 nchini kote kulitokea jumla ya ajali za pikipiki 2,544 zilizosababisha vifo vya watu 890 na majeruhi 2,128.




"Mwaka 2017 zilitokea ajali za pikipiki 1,459 zilizosababisha vifo vya watu 728 na majeruhi 1,090. Mwaka 2018 zilitokea ajali za pikipiki 876 zilizosababisha vifo vya watu 366 na majeruhi 694," alisema.

Alieleza kuwa katika kipindi cha Januari hadi Juni 2019 kumetokea ajali za pikipiki 334, zilizosababisha vifo 176 na majeruhi 289, ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha Januari hadi Juni 2018.

"Kwa kipindi cha Januari na Juni 2018 zilitokea ajali 408 zilizosababisha vifo 165 na majeruhi 344 utaona kupungua kwa ajali za pikipiki sawa na asilimia 18 kuongezeka vifo 11 sawa na asilimia 6.6 na kupungua kwa majeruhi 55 sawa na asilimia 16," alisema.

Alibainisha kuwa takwimu hizo zinathibitisha kupungua kwa ajali za pikipiki barabarani zinazotokana na waendesha pikipiki kutozingatia sheria.

"Kupungua kwa ajali hizi ni mafanikio yanayopatikana kutokana na usimamizi wa sheria ya usalama barabarani kwa kukamata waendesha pikipiki wanaokiuka sheria na kuwachukulia hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kuwafikisha mahakamani," alisema.



Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani (wa tatu kulia), akipata maelezo ya ujenzi wa handaki, uliokamilika kwa asilimia 100, alipokagua maendeleo ya ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme wa Julius Nyerere Rufiji mkoani Pwani juzi. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Wakulima wa korosho wapewa matumaini malipo

WIZARA ya Kilimo imesema madai ya wakulima wa korosho ambao bado wanadai yatalipwa kabla ya msimu ujao kuanza.

Hayo yalielezwa jana bungeni na Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba, alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Ndanda (Chadema), Cecil Mwambe.

Katika swali lake, Mwambe alihoji mwaka jana serikali ilichukua uamuzi wa kukusanya korosho yote kwa wakulima, kutangaza bei na kwamba watawalipa wakulima wote.

Hata hivyo, alisema kumekuwa na sintofahamu kwa wakulima hao kwa kuwa mpaka sasa serikali haijakamilisha malipo kama ilivyoahidi.

"Rais alisema serikali imeshatenga fedha na zinatakiwa kulipwa kwa wakulima kwa asilimia 100, naomba kujua kauli ya serikali ni lini hasa malipo ya wakulima wa korosho yatakamilishwa," alihoji.

Akijibu swali hilo, Mgumba alisema serikali ina fedha za kuwalipa na kwamba katika ununuzi wa korosho hizo iliielekeza Bodi ya Nafaka mchanganyiko kununua korosho zote kutoka kwa wakulima.

Alibainisha kuwa taasisi hiyo ilienda kukopa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) na kilichotokea hadi kutokamilisha malipo hayo ni kutokana na ukomo wa fedha walizopangiwa.

"Hii imetokana na limit (ukomo) ambayo walipangiwa wameshafikia, hivyo ilikuwa ni lazima kuuza korosho kwanza ili wapunguze gap (tofauti) wauze tena, tumeshauza korosho na kabla ya msimu ujao kuanza wakulima watalipwa fedha zao," alisisitiza.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Ubungo (Chadema), Saed Kubenea, alihoji kitendo cha kutoa kibali kwa viwanda vya sukari kuagiza sukari kutoka nje siyo kuua kabisa kilimo cha zao la miwa, ambacho wakulima wanategemea kuuza kwenye viwanda vya ndani.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Mgumba alisema serikali kupitia Bodi ya Sukari imekuwa ikifanya tathmini ya mahitaji ya sukari nchini kwa mwaka kwa kuzingatia matumizi ya kawaida na matumizi ya viwandani.

Alisema tathmini hiyo hufanyika sambamba na kujua uwezo wa viwanda vya kuzalisha sukari hapa nchini na nakisi kati ya uzalishaji na mahitaji ndio kiasi cha sukari inayohitajika kuagizwa kutoka nje ya nchi.

"Tathmini ya mahitaji ya sukari kwa miaka miwili iliyopita 2017/18 na 2018/19 ilibaini kuwapo na utengamano wa soko la ndani kwa bei na upatikanaji wa sukari nchini," alisema.

Mgumba alisema utengamano huo ni matokeo ya uamuzi ya serikali ya kutumia mfumo wa kuwapa leseni wazalishaji wa ndani kuagiza sukari kutokana na mahitaji badala ya mfumo wa kutumia wafanyabiashara.

"Mfumo huo umedhibiti uingizaji wa sukari ya ziada nchini kwa kuwa wazalishaji huagiza kulingana na kiasi kilichoainishwa kwenye leseni husika," alisema.

Alisema kabla ya utaratibu wa kuwapata vibali wenye viwanda kuagiza sukari, nakisi ya sukari ilikuwa ni zaidi ya tani 130,000, lakini baada ya utaratibu wa wenye viwanda kuagiza upungufu umepungua hadi kufikia tani 38,000.

Kadhalika, alisema katika kipindi hicho uzalishaji wa miwa kwa wazalishaji wadogo umeongezeka kutoka tani 568,083 msimu wa 2017/18 hadi tani 708,460 msimu wa 2018/19.

"Ongezeko la uzalishaji wa miwa kwa wakulima wadogo limekwenda sambamba na ongezeko la kipato cha mkulima na mapato ghafi kwa wakulima wa Kilombero yamefikia thamani ya Sh. bilioni 68.7 msimu 2018/19 kutoka Sh. bilioni 48.1, msimu wa mwaka 2017/18," alisema.

Alibainisha kuwa kutokana na ongezeko la uzalishaji wa miwa kwa wakulima wadogo, uzalishaji wa sukari nchini umeongezeka kwa asilimia 16.8 kutoka wastani wa tani 307, 431.26 hadi tani 359,219.25 katika miaka hiyo.

# Aomba ATM maalum kwa wenye ulemavu

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Amina Mollel, amehoji serikali ina mikakati gani kuweka mazingira rafiki kwa watu wenye ulemavu pindi wanapoenda kupata huduma za kibenki hususani wanapotoa fedha kwenye mashine za ATM.

Akiuliza maswali bungeni jana, Mollel alihoji mpango wa serikali wa kuhakikisha ATM za benki zinawekewa mifumo inayokidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu.

"ATM za benki nyingi hapa nchini hazikidhi mahitaji ya watu wenye ulemavu," alisema.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, aliagiza benki zote nchini kuhakikisha zinaweka mazingira rafiki ya kuhudumia wenye ulemavu hususani wa miguu kulingana na uhitaji wao kwenye mfumo wa miamala kwa njia ya mashine za kutolea fedha ATM.

Dk. Kijaji alisema kuwa benki zote nchini zinawajibu wa kuhakikisha kuwa huduma za kibenki zinakuwa na mazingira yatakayowezesha wenye ulemavu wa miguu kupata huduma hiyo kwa urahisi.

Alisema changamoto ya uduni wa baadhi ya miundombinu kwa watu wenye ulemavu, hususani wenye ulemavu wa miguu imetatuliwa kwa sehemu kubwa na hivyo kuwa rafiki katika maeneo mengi yanayotoa huduma za kibenki kwa kutumia mashine za ATM.

Alilihakikishia Bunge kuwa serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu suala hilo ili kuhakikisha kuwa mifumo ya miamala kwa njia ya ATM inakuwa rafiki kwa makundi yote wakiwamo watu wenye ulemavu.

Awali alifafanua kuwa tangu serikali ilipoanza maboresho ya mifumo ya malipo nchini mwaka 1996, Benki Kuu ya Tanzania imeendelea kusimamia usimikaji wa mifumo ya kisasa, mahiri na salama ili kuendana na mahitaji ya soko na mabadiliko ya teknolojia.

Alieleza kuwa maboresho hayo ya mifumo yanalenga pamoja na mambo mengine kukidhi mahitaji ya makundi mbalimbali katika jamii wakiwamo watu wenye mahitaji maalum hususani wenye ulemavu.

Alibainisha kuwa Mei mwaka 2007, Benki Kuu ilitoa mwongozo wa mfumo wa malipo kwa njia ya mtandao ikiwa ni mpango wa serikali wa kuhakikisha kuwa huduma za malipo kwa njia ya mtandao yanafanyika kwa usalama na kukidhi mahitaji ya makundi yote katika jamii.

Alisema miongoni mwa vipengele muhimu na nyeti hususani kwa watu wenye ulamavu vilivyoainishwa kwenye mwongozo huo ni alama za utambuzi, usalama wa mifumo na uwezo wa mifumo wa kutunza siri za wateja.

Dk. Kijaji alisema pamoja na serikali kutoa mwongozo huo, benki zote nchini hazijafanikiwa kusimika ATM maalum na rafiki kwa watu wenye ulemavu hususani wenye ulemavu wa macho na inatokana na ukweli kwamba teknolojia ya ATM kwa watu wenye ulemavu wa macho ni ngeni, pia ina mfumo au mahitaji ya ziada ikilinganishwa na ATM za kawaida.

# Watakiwa kuchangamkia fursa za kifedha

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WANANCHI wametakiwa kuchangamkia fursa za huduma za kifedha zinazotolewa na Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) kwa njia ya mtandao wa kidigtali ulioongezwa thamani na kumwezesha mteja kupata huduma za kifedha ndani na nje ya nchi.

Akizungumza juzi kwenye halfa ya chakula cha jioni kilichoandaliwa na NBC jijini Arusha kwa lengo la kuwakutanisha wateja wao, Mkuu Wilaya ya Arusha, Gabriel Daqarro, alisema huduma hiyo itawasaidia wananchi hususani walioko ofisini kupata huduma za kifedha popote walipo.

Dagarro aliwapongeza wafanyabiashara wanaotumia benki hiyo ambayo imekuwa ikiwahudumia wateja wake kwa zaidi ya miaka 50 na katika hali ya usalama wa uhakika wa fedha zao.

"Benki hii ina mafanikio makubwa kwa misingi ya utoaji wa huduma bora kwa jamii zitakazosaidia kutengeneza faida na mnyororo wa thamani kuongezeka," alisema.

Alisema benki hiyo imekuwa ikisaidia kwa kurudisha faida kwa jamii ili kukuza maendeleo ya nchi, jambo hilo limesaidia sana ukuaji wa kiuchumi.

"Ni jambo jema sana kwa benki hii kuwakutanisha wateja na kuzungumza nao kuhusiana na uboreshaji uliofanyika. Nasi serikali kama wadau wa benki hii tumeendelea kutoa huduma ya usalama kwa ajili ya maendeleo ya benki na taasisi zingine kuiga mfano huu," alisema.

Mkurugenzi wa Wateja Wakubwa wa NBC, Linde Kapya, alisema changamoto mbalimbali wanaendelea kuziboresha, kuhakikisha wanapanua wigo wa upatikanaji wa huduma za kibenki ili kumrahisisha mteja

kupata huduma akiwa ofisini kwake.

Awali Meneja wa NBC Tawi la Arusha, Miraji Msuya, alisema ni muhimu sana kwa benki hiyo kukaa na wateja kwa lengo la kuwashukuru kwa kuendelea kutumia huduma zao ikiwamo wateja wakubwa wakati na wadogo na kupata changamoto mbalimbali katika kuboresha huduma za kibenki.

Alisema benki hiyo imejikita zaidi kujua mahitaji ya mteja ili kukua na kufikia malengo yake na kuwataka wananchi kungana nayo kwa kuwa ni benki kongwe na ina uzoefu wa zaidi ya miaka 50 katika utoaji wa huduma za kibenki.

Naye Meneja Bidhaa na Teknolojia wa NBC, Christophe Msangule, alisema huduma zao zimejikita zaidi kidigitali na wamekuwa wakiziongezea thamani kwa kuwa wana mifumo mbalimbali mipya ya kibenki ambayo mteja ana uwezo wa kupeleka fedha nje akiwa ndani ya ofisi yake.

Baadhi ya wateja wa benki hiyo Pasenshe Charles kutoka kampuni ya Utalii ya Wanyama Tours & Safari alisema NBC imewanufaisha kutokana na huduma zake kwa kuwa mbali na mikopo mizuri ya kifedha wamekuwa wakipata ushauri wa kibiashara na akaunti za malengo kwa wanawake.



Baadhi ya wakazi wa eneo la Haydom, wilayani Mbulu Mkoa wa Manyara, wakisubiri kuchota maji, ambayo upatikanaji wake ni shida katika eneo hilo juzi. **PICHA: GIFT THADEY**.

# Wananchi Odonyowas waiangukia serikali

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

WANANCHI wa kijiji cha Odonyowas wilayani Arumeru, wameiomba serikali kuweka bei elekezi kwa wafanyabiashara wa vyakula ili kuwawezesha kuvinunua na kujikinga na njaa.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti, wananchi hao walisema hali ya ukame inayowakabili inawapa wasiwasi mkubwa wa kukosa chakula kwa kuwa wamepanda mazao mbalimbali lakini wameshindwa kavuna.

Lomayani Sanare alisema kwa sasa vyakula vimeanza kupanda bei, hivyo wanaomba serikali iwawekee bei elekezi ambayo itamwezesha kila mwananchi kununua chakula na kuweka ndani ili kukitumia baadaye.

"Tunahofia sana kukumbwa na baa la njaa kutokana na hali ya hewa mbaya. Tulilima mazao mengi kwa ajili ya chakula lakini yalikauka shambani, hivyo tunaomba serikali itusaidie kutuangalia sisi wanyonge katika hili," alisema Peter Seuri.

Diwani wa Odonyowas, Elisante Nassary, aliiomba serikali kujipanga kwa ajili ya kutoa elimu kwa wafugaji kupunguza mifugo yao kutokana na ukame unaokuja kwa kuwa wengi wao hawana elimu ya kutosha, inayohusiana na ufugaji bora wa ng'ombe wachache.

"Unajua si binadamu tu tunahofia kufa njaa, bali hata mifugo yetu imeanza kudhoofika. Tunaiomba serikali kuja kutoa elimu kwa hawa wafugaji ili kuuza mifugo yao baadhi na wanunue vyakula kabla ya njaa hii haijafika," alisema.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Jerry Muro, akizungumzia suala hilo, alisema wilaya haina njaa wala ukame na inachakula cha kutosha kwa sababu maeneo mengi yamelimwa na pia kuna shughuli mbalimbali za maendeleo zinaendelea, hivyo wana imani hakuna njaa itakayowapata.

Alisema kuna baadhi ya vijiji kama Odonyowas, Losikito na Lengijave ambavyo mvua hazikuwa nyingi lakini chakula cha kutosha cha kutumia sasa na vya akiba kwa ajili ya kipindi kijacho.

# TAEC yafurahia utafiti zao la mpunga

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

TUME ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) imesema utafiti wa mbegu ya mpunga kwa kutumia teknolojia ya nyuklia ya kununurisha vinasaba (viasili), umeleta matokeo chanya ya kupata mbegu bora ya Super BC ambayo inatoa mavuno mengi zaidi visiwani Zanzibar.

Akizungumza jana na Nipashe ofisini kwake, Mtafiti Mwandamizi wa Teknolojia ya Nyuklia, Simon Mdoe, alisema utafiti huo ulianza mwaka 2009.

Mdoe alisema tangu kuanza kwake, umefanikisha matokeo chanya mara saba zaidi kwa mavuno ya mbegu ya Super BC ikilinganishwa na awali.

Mdoe alisema utafiti wa mbegu hiyo uliofanywa na Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha Zanzibar (Zari) pamoja na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA), unaratibiwa na TAEC kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki (IAEA).

Katika utafiti huo, alisema walinunurisha (kupitisha mionzi kitaalamu kwenye mbegu) ambayo ilibadilisha vinasaba na kuwa bora zaidi, hivyo kuzalisha mara saba ya mazao yaliyokuwa awali.

"Katika utafiti wetu tulichukua mbegu za mmea wa mpunga na kupitisha miale ya nyuklia kwa hatua sita, huku kila hatua moja tukihamishia mbegu shambani na kupata matokeo tofauti. Mara ya mwisho tulipata matokeo mazuri zaidi kuliko hatua zingine tano na kugundua kuwa mavuno yamefikia mara saba ya kawaida ya mbegu hizo," alisema.

Alitoa mfano kuwa mkulima kabla ya uvumbuzi huo kufanyika, alikuwa akivuna magunia 12 kama ambavyo imezoeleka kwa mbegu za zamani na alipotumia mbegu za super BC alipata magunia 70, jambo ambalo linamtoa mkulima katika umaskini na kupata tija kwa kilimo.

Mtaalamu huyo alisema baada ya matokeo ya utafiti ushirikishwaji ulifanyika kwa mashirika ya mbegu za Super BC zilitawanywa kwenye maduka ya mbegu visiwani Zanzibar na wakulima walipata matokeo hayo hayo mazuri mara saba zaidi tofauti na awali.

Alisema kabla ya utafiti, asilimia 80 ya wakulima Zanzibar wanapendelea kutumia mbegu hiyo.

Mdoe alisema pia matokeo mengine ya utafiti na kuboreshwa kwa mbegu kupitia mionzi ya nyuklia, yamebaini kuongezeka kwa ladha ya mchele uliotokana na mpunga wa Super Bc pamoja na harufu nzuri kwa walaji.

# TPDC yakutanisha wadau bomba la mafuta

**Na Juster Prudence,** TUDARCo

SHIRIKA la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), limesema lipo katika majadiliano na washirika wa mradi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima-Uganda hadi Tanga-Tanzania yatakayowezesha mradi huo kuendelea.

Ujenzi huo ulitarajiwa kukamilika 2020, lakini hivi karibuni moja ya kampuni inayoshiriki kutoa mtaji za Total Oils ya Ufaransa, ilitangaza uwezekano wa kujitoa kwenye mradi huo.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa kwenye moja ya magazeti (siyo Nipashe), TPDC ilisema kuwa majadiliano hayo yatahitimishwa na makubaliano yatakayowezesha mradi kuendelea.

"Katika kipindi chote TPDC imeendelea kusimamia utekelezaji wa mradi huo kwa ufanisi mkubwa, hivi karibuni kumekuwapo na taarifa za kuchelewesha kwa mpango wa mradi kutokana na washirika kuchukua muda mrefu kukubaliana na masuala ya fedha," ilisema taarifa hiyo iliyotolewa na Mkurugenzi Mtendaji.

Kwa mujibu wa TPDC, washirika bado wana nia ya dhati ya kuendelea na utekelezaji wa mradi huo kwa kushirikiana kwa karibu na Serikali ya Tanzania na Uganda kuona mradi unakamilika kwa ufanisi.

Vile vile, TPDC iliuhakikishia kwamba changamoto za namna hiyo kwenye miradi mikubwa ya kisekta na kimkakati ni ya kawaida.

Uzinduzi wa mradi huo ulifanywa na marais wa nchi za Uganda na Tanzania mwaka 2017 baada ya kusaini mkataba wa ujenzi wa bomba hilo lenye urefu wa kilomita 1,120, ambalo litaweza kutoa ajira zaidi za ya 15,000.

Septemba 6, wakati wa kongamano la biashara kati ya Tanzania na Uganda, Rais John Magufuli, alieleza kukerwa na ucheleweshaji wa mradi huo unaofanywa na baadhi ya watendaji wa Serikali ya Uganda, huku akimshauri Rais wa Uganda, kuchukua hatua dhidi ya wahusika.

Ujenzi wa bomba hilo unatarajiwa kugharimu zaidi ya Dola za Marekani Sh. bilioni nne na tayari Serikali ya Tanzania ilishaanza kulipa fidia kwa wananchi wa vijiji vitakavyopitiwa na mradi huo.

Shughuli zitakazotoa ajira ni ujenzi wa tangi za mafuta, usafirishaji, mawakala mbalimbali wa mafuta watakaokuwapo mkoani Tanga na Uganda.

# Wakulima wazidi kulilia mfumo stakabadhi ghalani

**Na Mwandishi Wetu,** MOROGORO

MUUNGANO wa vikundi vya wakulima nchini (MVIWATA), umelalamikia uamuzi wa kusitishwa kwa shughuli za ushirika, ukisema hatua hiyo ni sawa na kuisaliti ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Hayo yamebainishwa na Mkurugenzi Mtendaji wa MVIWATA, Veronika Sophu, alipoongea na Nipashe kuhusu hali ya sekta ya kilimo nchini na changamoto zinazowakabili wakulima, mjini Morogoro.

Alisema MVIWATA imesikitishwa na hatua kusitisha mfumo wa ushirika (stakabadhi ghalani) kwa mazao ya dengu, choroko, soya, ufuta na mbaazi.

Sophu alisema, mazingira ndani ya Ilani ya CCM ya mwaka 2015-2010 ibara ya 22 (g) na (w), ziliwekwa mahususi kwa ajili ya kuuinua mfumo wa ushirika na kumsaidia mkulima.

"Sasa haiwezekani mambo yaliyopigiwa debe na wakubwa serikalini, yanakuja kusitishwa kwa utashi wa watu wachache, hilo sio jambo la kulikalia kimya hata kidogo," alisema Sophu.

Alisema uamuzi uliofanywa dhidi ya mfumo huo haukubaliki na kumwomba Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, kuwafikishia wakulima kilio chao kwa Rais John Magufuli.

Mfumo huo ulisitishwa rasmi Septemba 3, mwaka huu.



Kijana wa mtaani akiosha kioo cha gari katika Barabara ya Bibi Titi Mohamed, jijini Dar es Salaam jana, bila ya kuruhusiwa kitendo ambacho husababisha usumbufu kwa madereva. **PICHA: MIRAJI MSALA**.

# Serikali yaendelea kuwalipa waliokuwa wafanyakazi Mutex

**Peter Haule na Farida Ramadhani,** **WFM, DODOMA**

SERIKALI kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina inaendelea na taratibu za kuwalipa waliokuwa wafanyakazi wa Kiwanda cha Nguo cha Musoma (Musoma Textile Mills Limited Mutex) kwa mwaka wa fedha 2019/20, baada ya uhakiki kukamilika mwezi Juni, 2019.

Hayo yameelezwa bungeni jijini Dodoma na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dk. Ashatu Kijaji alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum, Joyce Sokombi, aliyetaka kujua utofauti wa malipo kwa waliokuwa wafanyakazi wa kiwanda hicho baada ya kufungwa mwaka 1984.

Dk. Kijaji alisema, serikali inafuatilia kwa karibu malalamiko yote yanayohusu tofauti ya kiwango cha malipo yaliyofanyika hivi karibuni ikilinganishwa na kiwango kilichoidhinishwa kwenye kikao cha pamoja kati ya mfilisi wa kiwanda hicho, wadau na serikali ili kuona kama yana ukweli.

"Baada ya serikali kupokea maombi ya malipo kutoka kwa wafanyakazi hao mwaka 2018, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanya uhakiki wa wafanyakazi hao ili kujiridhisha na hatimaye kufanya malipo," alieleza Dk. Kijaji.

Alisema, awali jumla ya wafanyakazi 219 walijitokeza na wasimamizi wa mirathi 14 na hivyo kulipwa jumla ya Sh. milioni 44.5, pia Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifanya tena uhakiki mwezi Juni, 2019 kwa wafanyakazi ambao hawakujitokeza katika uhakiki wa awali na jumla ya wafanyakazi 115 walijitokeza pamoja na wasimamizi wa mirathi 22 ambao kwa ujumla wanastahili kulipwa Sh. milioni 20.7.

Dk. Kijaji alisema serikali ilisimamisha uzalishaji katika kiwanda cha Mutex mwaka 1994 baada ya kukabiliwa na changamoto ya ukosefu wa mtaji na ongezeko kubwa la madeni kutoka taasisi iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Alisema kiwanda hicho kilifilisiwa na hatimaye kuuzwa mwezi Machi, 1998 kwa Kampuni ya LALAGO Cotton Ginnery and Oil Mills, kisha wadai, serikali na mfilisi waliridhia mapendekezo ya kulipa kiasi cha Sh. milioni 161.3 kwa wafanyakazi 935 waliokuwapo kiwandani baada ya kikao kilichofanyika Septemba 23, 2005.

Alisema kuwa baada ya zoezi la ufilisi kukamilika, wafanyakazi 512 pekee ndio walioijitokeza kuchukua mafao yao na wengine 423 waligoma kupokea mafao yao kwa madai kwamba nauli ya familia na gharama za kusafirisha mizigo ni ndogo.

Wafanyakazi hao 423 walifungua kesi katika Mahakama ya Kazi ya Tanzania na baadaye Mahakama hiyo ilitoa tuzo Juni 10, 2008 na ilitupilia mbali shauri hilo na kuamuliwa wadai waende kwa mufilisi kuchukua stahili zao.

Pia wadai hao walifungua shauri jingine la maombi ya marejeo na Februari, 2010 mahakama hiyo iliamua tena wadai waliogoma kuchukua mafao yao waende kwa Mufilisi kama ilivyoridhiwa katika kikao cha wadau.

Nipashe
# TESA
Jumanne Septemba 10, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Ukurasa 14




## MICHEZO YA EAPCCO 2019 YAMALIZIKA

Ukurasa 18



## JE, WAJUA?

Jogoo mwenye kelele ashinda kesi dhidi ya jirani zake



Ukurasa 17

## JIELIMISHE

Wanasayansi kuchunguza shimo jeusi lililo angani



# Simulizi ya aliyenusurika kuozeshwa ndoa ya utotoni

Ukurasa 15

ELIMU KUTOKA POLISI

# Michezo ya EAPCCO 2019 yamalizika jijini Nairobi



Wanamichezo kutoka Jeshi la Polisi Tanzania wakipita kutoa heshima kwa mgeni rasmi wakati wa ufunguzi wa michezo ya Wakuu wa Majeshi ya Polisi ya Nchi za Kanda ya Afrika Mashariki (EAPCCO GAMES 2019) yaliyomalizika jijini Nairobi nchini Kenya, Agosti 31.



Askari wa Jeshi la Polisi Tanzania na Jeshi la Polisi Kenya (katikati), wakiwa na medali zao walizotunukiwa baada ya mashindano ya ulengaji wa shabaha kwa silaha ya SMG AK 47 wakati wa mashindano hayo



Askari kutoka nchi za Tanzania, Uganda, Rwanda, Kenya na Burundi wakiwa katika ulengaji wa shabaha kwa timu za askari wa kike kwenye mashindano ya michezo ya Wakuu wa Majeshi ya Polisi ya Nchi za Kanda ya Afrika Mashariki (EAPCCO GAMES 2019). **PICHA ZOTE: JESHI LA POLISI**

MICHEZO ni miongoni mwa mikakati ambayo hutumika na vyombo vya ulinzi na usalama katika kujenga umoja, kuimarisha uhusiano na ushirikiano pamoja na kubadilishana taarifa za kiintelijensia ambazo husaidia katika mapambano dhidi ya uhalifu na wahalifu hususani makosa yanayovuka mipaka na yale yanayofanyika kwa njia ya mtandao.

Katika kutekeleza malengo ya mapambano ya uhalifu unaopangwa ndani na nje ya nchi, Wakuu wa Majeshi ya Polisi kwa nchi za Kanda ya Afrika Mashariki na kati waliamua kuanzisha umoja wao ambao pamoja na mambo mengine kujadili masuala ya uhalifu ndani ya nchi wanachama.

Walianzisha michezo ya Wakuu wa Majeshi ya Polisi kwa nchi za kanda ya Afrika mashariki na kati inayojulikana kwa jina la EAPCCO GAMES likiwa na lengo mahususi la kuwaleta pamoja askari majeshi ya Polisi kwa nchi wanachama wa umoja huo katika kupambana na wahalifu na uhalifu unaovuka mipaka.

Akifunga michezo ya wakuu wa majeshi kwa nchi za kanda ya Afrika Mashariki na Kati iliyofanyika viwanja wa Kasarani Jijini Nairobi nchini Kenya, Waziri wa Ulinzi wa nchi hiyo Recho Omamo aliwaeleza askari wa Majeshi ya Polisi wa Kanda hiyo kutumia michezo katika kubadilishana uzoefu wa namna ya kupambana na uhalifu na wahalifu ndani na Nje ya Kanda hiyo.

Michezo hiyo ya Wakuu wa Majeshi ya Polisi kwa nchi za kanda ya Afrika Mashariki (EAPCCO 2019) inajumuisha nchi 14 ambapo kati ya hizo nchi 7 tu ndizo zilizoshiriki ambazo ni Tanzania, Uganda, Rwanda, Burundi, Sudani, Sudani ya Kusini pamoja na nchi ya Kenya ambayo ilikuwa mwenyeji wa michezo hiyo.

Katika mashindano hayo askari kutoka katika nchi hizo wanachama wa umoja huo walipata fursa ya kushiriki katika michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu, mpira kikapu, taekwondo, Judo, Karate, kuvuta kamba, riadha mbio ndefu na mbio fupi, kurusha vishale, mpira wa wavu pamoja na kulenga shabaha.

Katika michezo hiyo Timu za Jeshi la Polisi Tanzania zilizoshiriki katika michezo ya Wakuu wa Majeshi ya Polisi kwa nchi za Kanda ya Afrika Mashariki (EAPCCO 2019), zimefanikiwa kupata jumla ya Medali 39 Katika medali hizo dhahabu 3, Silva 9 pamoja na Medali 27 za Shaba.

***Imetolewa na:***
***Dawati la Habari EAPCCO Games 2019,***
***Ofisi ya Uhusiano,***
***Makao makuu ya Polisi (TZ)***



TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Upotoshwaji wa maneno ya Kiswahili

SHAKA (hali ya kuwa na wasiwasi juu ya jambo) yangu ni jinsi Kiswahili kinavyoborongwa (haribu kazi kwa kasi; atili, bananga) na waandishi wa magazeti yetu ya Kiswahili!

Matokeo yake sasa hata kuandika sentensi zenye mtiririko unaoeleweka zawashinda waandishi. Kwa muktadha huu, 'maana' ni dhana inayowakilishwa na neno; ufafanuzi wa kitu au jambo. Kinyume chake ni upotoshaji yaani kitendo cha kufanya mtu mwingine afanye jambo lisilokuwa sahihi.

Ingawa yapo baadhi ya maneno yenye maana zaidi ya moja, sioni sababu ya waandishi kupotosha maana halisi ya maneno ilhali yapo maneno sahihi lakini hawayatumii. Badala yake hutumia maneno yaliyo tofauti na maudhui (wazo kuu linaloelezwa katika maandishi au katika kusema) ya kazi zao.

'Mwisho' ni ukomo wa jambo; kikomo, hitimisho; hali ya kumalizika, tamati. Kwa hiyo isemwapo "mwisho wa siku" maana yake ni mwisho wa siku husika. Soma sentensi ifuatayo:

"Akizungumza na ... (jina la gazeti) jana, Katibu Mkuu wa Klabu ya Lipuli, Julius Leo, alisema walikuwa wamemtengea dau Boban na alikubali kwenda kusaini mkataba, lakini mwisho wa siku wakasikia amechukuliwa na Yanga."

"Mwisho wa siku" hutumiwa na watu wengi kiasi cha kuonekana ni maneno sahihi kumbe siyo. Badala ya kuandika "mwisho wa siku" ingeandikwa 'mwishowe' au 'hatimaye.'

"Makambo alifunga bao lake la tisa msimu huu wakati Yanga ikipata ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Ruvu Shooting katika pambano lililopigwa Uwanja wa Taifa ambapo msemaji wake, Masau Bwire aliamua kuchomoa bastora ili kuwatawanya mashabiki wa Yanga waliokuwa wakimzonga mara baada ya pambano hilo kali."

Waandishi wa michezo wamezoea sana kuandika "pambano lilipigwa ...". Pambano 'halipigwi' bali hufanywa au huchezwa. Kosa la pili la mwandishi ni kuandika kuwa Masau Bwire alichomoa 'bastora', neno lisilokuwa na maana yoyote kwa Kiswahili! Neno sahihi ni 'bastola' yaani bunduki ndogo fupi ambayo aghalabu hufichwa mwilini bila ya kuonekana.

"Simba yazidi kutetema Bara" ni kichwa cha habari kwenye gazeti mashuhuri la michezo nchini. Je, ni kweli kuwa Simba ilitetema? Maana ya 'tetema' ni kitendo cha kutikisika, harakaharaka; tetemeka. Ingeeleweka kama ingeandikwa "Simba yatetemesha Ligi Kuu."

Kichwa kingine cha gazeti hilohilo kiliandikwa: "Kitendo cha mashabiki kuvamia uwanjani lidhibitiwe mapema." Mwandishi angeandika "Kitendo cha mashabiki kuvamia uwanja kidhibitiwe mapema" badala ya "kitendo ... lidhibitiwe." 'Kitendo' ni kundi la maneno yanayotaja matendo kama vile lala, tembea, pumua n.k.

Waandishi wanavyoharibu maneno: "Mara baada ya kuanza kwa Ligi Kuu Bara kikosi cha Yanga hakikuwa kikipewa nafasi kubwa ya kutamba kutokana na kuwa na wachezaji wengi wa kawaida, huku mafundi wakiwa ni wachache mno." Sentensi ya maneno 31 yaliyoandikwa shelabela (hali ya kukosa mpango maalumu)!

Ingeandikwa: "Ligi Kuu ya Bara ilipoanza, Yanga haikupewa nafasi kubwa ya kufanya vizuri kwani wachezaji wengi walikuwa wa kawaida wakati mahiri wakiwa wachache." (Maneno 22). 'Mahiri' ni -enye uhodari wa jambo fulani.

Sentensi ya mwisho ya habari hiyo haikumalizika; kwa hiyo haikueleweka! "Mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba, wanashika nafasi ya tatu baada ya kujikusanyia pointi 27 kutokana na" (Mwandishi alikomea hapo bila kueleza ni kutokana na nini.) Haraka haraka haina baraka! Wanaodurusu (wanaopitia maandiko ili kusahihisha) hawakuwa makini katika kazi yao.

"Kikosi changu ni kizuri na tunatambua tunaenda kucheza na timu nzuri lakini mara nyingi huwa kikosi cha ushindi katika timu yoyote hakibadilikagi," alisema Aussems ambaye alichukua mikoba ya kukinoa kikosi cha Simba kutoka kwa Pierre Lechantre. (Maneno 36 katika sentensi moja).

'Hakibadilikagi' si Kiswahili sanifu (-enye kufuata vigezo vilivyokubalika.) 'Mikoba' ni wingi wa 'mkoba' na maana yake ni chombo cha kusukwa au kushonwa cha kutilia vitu; mkoba wa kuili. Pia ni mfuko wa mganga wa kuwekea zana zake za kazi. Ina maana kocha wa Simba alikabidhiwa mikoba ya uchawi!?

Ingeandikwa: "Kikosi changu ni kizuri na tunakwenda kupambana na timu nzuri. Hata hivyo, mara nyingi kikosi cha ushindi hakibadiliki," alisema Aussems aliyechukua nafasi ya Pierre Lechantre.

"Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' alisema beki wao kisiki Juuko amebadilika si kinizamu yaani nje ya uwanja na hata ndani katika kushindania namba anapokuwa mazoezini."

**Methali: Pauliwapo nyoka hapaachi ndombezi.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Simulizi ya aliyenusurika kuozeshwa ndoa ya utotoni

• Baba yake alishapokea mahari ya ng'ombe watano na Sh. 300,000

MTOTO Nchambi mwenye umri wa miaka 17 (si jina lake halisi), mkazi wa Kata ya Maganzo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, amesimulia alivyonusurika kuozeshwa ndoa ya utotoni na Baba yake mzazi kwa mahari ya ng'ombe watano pamoja na fedha taslimu Sh. 300,000 kwa mwanamume ambaye hata hamjui.

Akielezea tukio hilo Septemba 5, mwaka huu kwa mwandishi wa makala haya anasema aliona ng'ombe watano wameletwa nyumbani kwao, akajua kwamba baba yake amewanunua, kumbe haikuwa hivyo bali ni mahari iliyotolewa ili yeye aolewe.

Anasema ng'ombe hao waliletwa kwao Juni mwaka huu na baada ya kupita takribani mwezi mmoja, ndipo siku moja akaitwa na wazazi wake na kuelezwa kwa nini ng'ombe hao wako kwao.

Alijulishwa na Baba yake mzazi kwamba amechukua mifugo hiyo kama malipo ya mahari yake, hivyo anapaswa kuolewa ili familia yao ipate mali (mifugo).

Anafafanua kuwa aligoma kuolewa, tena na mwanamume ambaye hata hamjui, kwani nia yake ni kuendelea na masomo baada ya kuwa amemaliza elimu ya msingi mwaka 2017.

"Baada ya kugoma, wazazi walianza kunishawishi nikubali tu kuolewa, na kwamba endapo nitakataa, nitaleta mkosi kwenye familia yetu kwa kuwa kwa mujibu wa mila na desturi za kabila letu la Kisukuma, muoaji huwa hakatiliwi," anasema.

Nchambi anabainisha kwamba wamezaliwa mapacha kwa wazazi wao na mwenzake alifaulu kuendelea na masomo ya Sekondari, na sasa yuko kidato cha pili wakati yeye hakufaulu. Anasema kila alipowaeleza wazazi wake wampeleke chuo akasome hata kozi ya ufundi cherehani, wamekuwa wakimueleza kwamba hawana uwezo.

"Hivyo niliamua kukaa tu nyumbani, lakini kumbe ninavyoendelea kubaki nyumbani naonekana kero kwa wazazi wangu, na ndipo wakaamua kunitafutia mwanamume wa kunioa," anasema na kuongeza:

"Mimi bado mdogo, siwezi kumudu masuala ya ndoa...vilevile nafahamu madhara ya kuolewa katika umri mdogo kutokana na elimu tuliyokuwa tukipewa shuleni."

Anasema wazazi wake waliendelea kumrubuni ili akubali kuolewa kwa kuwa tayari wameshachukua mahari hiyo na kwamba endapo ataendelea kugoma kwa kutotii amri yao, watakosa mali hizo, hivyo kutouepuka umaskini walionao.



Mtoto Nchambi (si jina lake halisi) mkazi wa Kata ya Maganzo wilayani Kishapu Mkoani Shinyanga, akisimulia namna alivyotaka kuozeshwa ndoa ya utotoni na wazazi wake, ambao tayari walikuwa wamechukua mahari ya ng'ombe watano na Sh.300,000 ili kumuozesha kwa mwanaume ambaye hata hakuwa anamjua. **PICHA: MARCO MADUHU.**

> "Hatua hiyo iliniokoa kwani wazazi waliamua kusitisha suala la kuniozesha na wakaamua kurudisha ng'ombe za watu walizochukua kama mahari yangu.

### ASAIDIWA

Nchambi anafafanua kuwa wakati mvutano ukiendelea nyumbani kwao na kuonekana kama mkosi ndani ya familia, ndipo siku moja akaona wanakuja wasaidizi wa kisheria nyumbani kwao.

Wasaidizi hao wanatoka Shirika la PACESH linalojishughulisha na masuala ya kijamii.

"Wasaidizi hao waliwaelimisha juu ya Sheria ya Mtoto na madhara ya ndoa za utotoni...waliwaelimisha pia kuhusiana na madhara ya kumuozesha mtoto mdogo, kwani ni ukiukaji wa Sheria ya Mtoto.

"Hatua hiyo iliniokoa kwani wazazi waliamua kusitisha suala la kuniozesha na wakaamua kurudisha ng'ombe za watu walizochukua kama mahari yangu," anasema.

### BABA MZAZI

Naye Baba mzazi wa mtoto huyo, Lyuba Seif, anakiri kutaka kumuozesha binti yake huyo, kwa madai amekaa nyumbani kwa muda mrefu baada ya kufeli masomo yake ya elimu ya msingi.

"Tatizo sina uwezo wa kifedha wa kumsomesha hata kwenye vyuo vya ufundi, na ndiyo maana nilichukua uamuzi wa kumtafutia mwanamume ili aolewe, nipate mali," anasema.

Seif anabainisha kwamba kutokana na binti yake kukaa nyumbani kwa muda mrefu, anahofia asije kupata ujauzito na hivyo kuzalia nyumbani, kitendo ambacho ni mkosi kwenye familia, pamoja na kuwakosesha utajiri (mifugo), hivyo kuendelea kuwa maskini.

"Nilishapanga kumuozesha binti yangu huyu kwenye kijiji cha jirani, ambapo tayari nilishachukua mahari ya ng'ombe watano pamoja na pesa taslimu Sh. 300,000 ili kujihami asije akapewa ujauzito akiwa nyumbani, na kutuletea mkosi kwenye familia," anasema.

### ATOA OMBI

Mzazi huyu anaomba wadau wajitokeze kumsomesha binti yake huyo chuo chochote cha ufundi ili apate kutimiza ndoto zake, kutokana na yeye kutokuwa na uwezo wa kifedha.

Anabainisha kwamba endapo atakosekana mtu wa kumsaidia, itabidi mwakani amuozeshe kwenye familia hiyohiyo, kwa sababu atakuwa ameshafikisha umri wa miaka 18.

"Ieleweke nimeahirisha suala hili la kumuoza binti yangu baada ya kubanwa tu na hawa wasaidizi wa kisheria... tayari nimesharudisha ng'ombe za watu, lakini nina deni la Sh. 300,000 ambazo nilizitumia," anasema na kuongeza:

"Ninasubiri mwakani atakapofikisha miaka 18, umri wa mtu mzima kama atakuwa hajapatikana msamaria mwema wa kumlipia masomo ya chuo, basi nitampleleka akaolewe huko huko nilikochukua pesa ya watu."

### PACESH

Kwa upande wake msaidizi wa kisheria kutoka Shirika hilo la PACESH Maganzo wilayani Kishapu, Fatuma Katabalo, anasema taarifa za kuozeshwa kwa binti huyo ndoa ya utotoni walizipata kwa majirani zao.

"Ndipo tulipoamua kwenda kwenye familia hiyo kuwapatia elimu ya sheria ya mtoto na madhara ya kuozesha mtoto mdogo," anasema.

Fatuma anabainisha kwamba baada ya kufika kwenye familia hiyo walikaa na wazazi wa binti huyo, na kuwaeleza kwamba kitendo hicho wanachotaka kukifanya ni ukiukwaji wa sheria ya mtoto.

### MENEJA

Meneja Mradi wa Huduma na Msaada wa Kisheria kutoka Shirika hilo la PACESH Mkoani Shinyanga, John Shija, anakubaliana na uamuzi wa wazazi wa mtoto huyo wa kusitisha ndoa hiyo.

"Ninatoa ahadi ya kumsomesha binti yao huyo chuo cha ufundi ili apate kutimiza ndoto zake alizonazo za kielimu," anasema.

Anabainisha kwamba tatizo la mimba na ndoa za utotoni mkoani Shinyanga haliwezi kwisha, endapo wazazi wenyewe watashindwa kujitambua, na kuacha kuendekeza mila potofu za kutomthamini mtoto wa kike, kwa kumchukulia kama kitega uchumi kwenye familia.

Anatoa wito kwa wazazi mkoani humo kuacha tabia ya kuwaozesha mabinti wakiwa katika umri mdogo.

### TAKWIMU

Takwimu za kitaifa za mwaka 2012 zinaonyesha kwamba mkoa wa Shinyanga unaongoza Tanzania kwa tatizo la mimba na ndoa za utotoni kwa asilimia 59, ukifuatiwa na Tabora asilimia 58 na Mara asilimia 55, ambapo watoto wa kike wamekuwa wakiolewa chini ya umri wa miaka 18.

ELIMU

NA JALIWASON JASSON, BABATI

# Unajua Chekechea ilivyobeba siri mahali elimu inakosusasua nchini?

***"...mchango mkubwa katika ukuaji ubongo wa mwanafunzi, kwani matumizi yake yanamsaidia kujenga kumbukumbu ya kudumu, pia yanamjenga milango yote ya fahamu na inawasaidia wanafunzi kulipenda somo husika..."***

• Kila zana darasani, sawa maneno maelfu • NGO Manyara yawaletea mapya wafugaji • Majaribio tu, wasiojua kusoma nao adimu • Mwalimu 'afunguka' mazito yake darasani



Wanafunzi wa madarasa ya awali, wakiendesha taaluma kutoka Shule ya Msingi Dudumer, katika Halmshauri ya Dudumera, iliyopo Babati. **PICHA ZOTE: JALIWASON JASSON**

KATIKA mustakabali wa sera za kitaaluma, ubora wa elimu unaanzia ngazi ya awali.

Hiyo iko bayana na ndio maana kuna wakati serikali ilitoa mwongozo wa ulazima wa elimu kuanzia ngazi ya awali. Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, kuna wakati ilitoa maelekezo kwa shule za msingi nchini kujiboresha katika eneo hilo.

Msingi wake kufanikisha hayo ni kwamba elimu katika ngazi hiyo ya awali inaboreshwa kwa kuwa na walimu makini, wanaokuwa chachu ya kuwatengeneza vyema, kuanza darasa la kwanza wakimudu kinachoitwa 'KKK' kwa maana ya; Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

Hitaji hilo ndilo linaloibua changamoto mpya ya kuwa na zana sahihi za kufundishia, ili iwe rahisi kuelewa kwa mtoto anayejifunza.

### KUTOKA BABATI

Ofisa Elimu Taaluma wa Halmashauri ya Wilaya Babati mkoani Manyara, Joyce Oronu, anasema sera ya elimu ya zamani ilimhitaji mwanafunzi wa darasa la awali awe mwenye umri kati ya miaka mitano hadi sita.

Anaeleza mabadiliko kwamba, hivi sasa mahitaji ni miaka minne, kwa maana ya kusoma miaka miwili, kwani anapofikisha umri wa miaka sita, anapaswa kuanza darasa la kwanza.

Oronu anasema katika kuhakikisha walimu wa awali wanatumia zana sahihi, mkoani Manyara, kuna asasi ya Literacy and Numeracy Education Support Programme (LANES) waliwapa mafunzo ya kutumia zana za kufundishia watoto awali.

Hiyo ilitoa mwanya kwa walimu wa awali 138 katika halmashauri hiyo, kila shule kukiwapo mwalimu mmoja aliyepatiwa mafunzo hayo, ili kumsaidia kuandaa zana na kuzitumia kuwafundisha watoto wa awali.

Anafafanua kwamba, zana zinatakiwa ziendane na umri wa mwanafunzi, pia nyenzo za mwalimu ziendane na somo analofundisha kukidhi vigezo vya kufundisha darasa la awali.

Mtaalamu Oronu, anaziweka zana tajwa kwenye makundi matatu: Zana za kutengeneza, mfano kiti, meza, jembe; jingine, zana za kununua kama mpira na kikombe, ambazo mwalimu anaweza kuwaagiza wanafunzi kuja nazo kutoka nyumbani; mwisho ni zana za kuunda kama vile vyungu na midori, ambavyo wanafunzi wanaweza kutengeneza kwa udongo wa mfinyanzi.

"watoto hao washauriwe kutembea kwa makundi, ili kukwepa uovu dhidi yao na anaelekeza wito kwa walimu na walezi kuwajibika kwa hilo ipasavyo.



Picha ya zana za kufundishia.

### ZINAWASAIDIAJE?

Ofisa mtaalamu huyo, anasema hizo zina mchango mkubwa katika ukuaji ubongo wa mwanafunzi, kwani matumizi yake yanamsaidia kujenga kumbukumbu ya kudumu, pia yanamjenga milango yote ya fahamu na inawasaidia wanafunzi kulipenda somo husika.

Pia, anataja manufaa ya kumrahisishia mwalimu kufundisha, huku mwanafunzi akiwa mbunifu, anayejiamini na kujielekeza.

Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Wilaya Babati, Getrude Kavishe, anasema walimu wanaotumia zana katika kuwajulisha watoto kujua kusoma, kuhesabu na kuandika, kunawapa uhakika wanajifunza kwa vitendo.

Getrude anasema katika mwaka wa kwanza wa darasa la awali, mwanafunzi zaidi anajifunza mazingira na kiasi kidogo cha masomo, kwani kwa asilimia kubwa wanakuwa wametawaliwa na michezo na hawajielewi

Anataja baadhi ya mambo wanayojifunza katika ngazi ya awali ni nyimbo, michezo mazingira ya shule.

"Mwaka wa pili unamuandaa mwanafunzi wa awali kuingia darasa la kwanza na kujifunza kwa michezo na nyimbo . Kwao ni vizuri zaidi na inamjenga mtoto aweze kujiamini na kuwa mbunifu," anasema Getrude.

"Kwanza watoto wale wanatakiwa wapewe ule upendo, hivyo kwenye michezo mwalimu anawapa upendo na anatakiwa kucheza nao michezo yao na shule ni mahali pazuri pa watoto kuchezea na kujifunza,"anasisitiza

Anafafanua kuwa mwalimu wa awali anatakiwa awe rafiki wa watoto na kushiriki kila mchezo wao na darasa likitawaliwa na vitu mbalimbali vya mchezo.

### KUWAPO VIBOKO?

Getrude anaendelea: "Yule mtoto wa awali ukimpiga atachukia shule, hataipenda tena, lakini ukijenga naye urafiki, mtoto huyo atakupenda na atakuwa rafiki wa mwalimu, mpaka kuja shule anakuwa hasukumwi na mtu yeyote na ukimzuia, lazima achukie."

Anasema, mwalimu wa ngazi hiyo hapaswi kuwaelekeza wanafunzi darasani kwa fimbo, akisema inamuogopesha na kumuondolea upendo.

Kuhusu mustakabali wa ulinzi na usalama wa wanafunzi hao wa awali wanapotoka na kwenda shuleni, Getrude anasema ni jukumu la jamii nzima kuhakikisha usalama na haki zao za kisheria.

Anasema, watoto hao washauriwe kutembea kwa makundi, ili kukwepa uovu dhidi yao na anaelekeza wito kwa walimu na walezi kuwajibika kwa hilo ipasavyo.

Sambamba na asasi ya Lanes, shirika la kimataifa la World Vision, nalo limeungana kubeba jukumu la kutoa mafunzo ya kuandaa zana za kufundishia watoto wa awali. Kila mwezi walimu wawili kutoka tarafa ya Mbugwe wanapewa mafunzo.

Oronu anafafanua, mafunzo hayo yana msaada mkubwa, kwa kuongeza idadi ya watoto wanaojua kusoma, kuandika na kuhesabu na World Vision, imekuwa ikisaidia kununua vifaa vya kutengeneza zana kwa shule za ukanda wa Mbugwe.

### WALIMU

Mwalimu wa darasa la awali katika Shule ya Msingi Dudumera, Jemima Njidile, kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Babati, ni mnufaika wa mafunzo ya ualimu wa darasa la awali.

Anashauri darasa hilo kutochanganywa na eneo jingine la shule, maana watoto hao hawatakiwi kuchanganywa na wenzao wa shule ya msingi.

"Wakichanganywa watoto hawa na wanafunzi wa shule ya msingi, wanashindwa kufanya vitu vinavyoendana na mtaala wao," anasema Jemima.

Anaeleza kwamba umuhimu wa zana za kufundishia, ndizo zinamfurahisha na kumtengenezea mtoto kumbukumbu na atapenda mazingira ya kufundishia.

Analimwagia sifa shirika la World Vision, kuwa mafunzo yaliyomsaidia kutengeneza zana zinazomtosheleza kufanya vizuri.

### HULKA YA UFUNDISHAJI

Kuhusu hili Jemima anaeleza: "Mwalimu wa awali inabidi awe anawapenda watoto na asitumie lugha ya ukali badala yake atumie lugha ya upole."

Anaongeza mfano: "Siku moja mtoto alimpiga mwenzake mpaka akatokwa na damu. Sikumpiga, ila nilimwambia atafute maji amnawishe mwenzake, ili wenyewe wapeane msamaha."

Mwalimu Jemima anasema, mbadala wa adhabu kwa mwanafunzi anayekosa anatumia mbinu ya kuwaelekeza na walio wasumbufu zaidi, anawaita wazazi wao kushauriana cha kufanya ili wajirekebishe.

Pia, anazungumzia mzigo wa wingi wa wanafunzi alio nao kwamba, darasa lake lina wanafunzi 95, hivyo fursa ya kumpitia kila mwanafunzi ni ngumu.

Mwalimu Jemima anasema kati ya Januari hadi Juni, huwa anawafundisha kucheza, kuimba na matendo, akiwachanganya mwaka wa kwanza na wa pili.

Anasema, kuanzia Julai hadi Desemba, ndipo anapoanza kuwafundisha 'namba matendo' akimaanisha kujumlisha na kutoa na kadri muda unavyosonga, anawachambua wanaoelewa kuingia darasa la kwanza.

Je zana zinamsaidiaje mtoto kujua kusoma, kuhesabu na kuandika? Mwalimu anafafanua kwa kauli "zaidi ya asilimia 90 inampa wepesi mwanafunzi."

### CHANGAMOTO

Anataja changamoto inayomkabili katika shule yake yuko peke yake kwa darasa hilo na ndio maana analazimika kuwachanganya wanafunzi wa mwaka wa kwanza na pili.

Anasema hata kipindi anapotaka kwenda likizo inakuwa changamoto, kwani mwalimu mkuu huteua mwingine kufundisha darasa hilo, wakati hana mafunzo ya kufundisha wanafunzi wa awali.

Ni hoja ambayo Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Dudumera, Mussa Mkumbo, anakiri mapungufu kwa shule hiyo iliyoanzishwa mwaka 1956, akieleza darasani pia wanafunzi wanalazimika kuandika wakiwa wamesimama, kutokana na urefu ukubwa wa madawati.

Anaainisha shule yake yenye wanafunzi 578, ina uhaba wa walimu. Kwamba mbali na mmoja wa darasa la awali, katika shule ya msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la saba, wapo walimu 10, kati yao saba wa kike na watatu wanaume.

Jemima anataja changamoto nyingine, ni ufinyu wa eneo la kuweka zana nyingi alizo nazo.

Anaiomba serikali kutenga maeneo ya kutosha kwa wanafunzi wa awali ili wafunzwe tofauti kimazingira, akitaja mfano wa aina za mahitaji yao ya kipekee; hisabati inayojumuisha vifaa vyake kama vile 'vihesabio' na picha za namba kuanzia moja mpaka tisa.

Jingine ni 'kona ya sayansi' anayosema inatakiwa kuwe na michoro, mfano mbwa, ndizi au machungwa; vivyo hivyo sanaa inayojumuisha ngoma na filimbi; 'kona nyumbani' inayojumuisha kitanda, jiko, chupa ya chai, mdoli, fagio, sahani, sabuni na kitana.

Pia, anazitaja 'kona ya michezo' mfano mpira, kamba, bembea; mwisho ni 'kona ya dukani' mfano chumvi, sukari, viberiti, madaftari, juice na kalamu anazosema zinahitaji maeneo yake, ili walimu wa awali wafundishe vizuri.

Wakichanganywa watoto hawa na wanafunzi wa shule ya msingi, wanashindwa kufanya vitu vinavyoendana na mtaala wao.

Mwalimu Mkuu Mkumbo, anashukuru msaada wa World Vision kuwezesha wanafunzi wake kumudu haraka kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na imekuwa vigumu kumkuta mwanafunzi darasa la tatu asiyejua kusoma na walimu wanafanya kazi kwa kujiamini.

### WANAVYONENA WADAU

Mratibu wa Mradi wa Magugu Area Programu kutoka Shirika la World Vision, Majid Mfinanga, anasema wanatekeleza mradi katika kata tano za Tarafa ya Mbugwe iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati, katika vijiji 22.

Mtaalamu huyo anayejitambulisha, aliwahi kuwa mkufunzi wa vyuo vya ualimu nchini, anasema matumizi ya zana za kufundishia yanasaidia kujenga kumbukumbu ya kudumu kwa kutumia milango ya fahamu na yanamfanya mwanafunzi kuelewa haraka.

"Mwalimu akitumia zana, anapunguza maneno na matumizi ya zana moja, inawakilisha maneno 10,000 ambayo mwalimu angezungumza...akitumia zana ni rahisi mwanafunzi kuelewa na zana ni mbadala wa yale maneno ya mwalimu,"anasema.

---

JIELIMISHE

# Wanasayansi kuchunguza shimo jeusi angani

KUNDI moja la Wanasayansi lililopiga picha za kwanza za shimo jeusi lililo angani, limetangaza mipango ya kuchukua video yenye uasili wa shimo hilo linalopatikana katikati ya anga.

Setilaiti itazinduliwa kusaidia mfumo wa darubini nane zitakazotumika kuchukua filamu hiyo.

Watafiti wanasema kwamba uimarikaji wa mfumo huo utawezesha kuona jinsi shimo hilo linavyovuta na kuingiza ndani vitu vilivyo karibu yake.

Kundi hilo tayari limetuzwa tuzo ya ufanisi. Profesa Heino Falcke, kutoka Chuo Kikuu cha Raboud nchini Uholanzi ambaye alipendekeza wazo hilo la darubini, ameiambia BBC kwamba, hatua ya pili ni kuona vitendo vya shimo hilo.

Kama vile sayari, shimo hilo jeusi pia huzunguka, lakini lina maajabu ya kuizungusha anga, elimu ambayo inatakiwa sasa ifuatiliwe. La kushangaza zaidi ni hatua ya kuchukua picha za rangi ya kitu ambacho uwezo wake ni mkubwa sana, kwamba hata mwanga hauwezi kuepuka.

Mapema mwaka huu kundi hilo la Wanasayansi lilichapisha picha za shimo kubwa jeusi lililokuwa katika sayari moja iliyo umbali wa kilomita bilioni 40, ikiwa ni mara tatu zaidi ya ukubwa wa dunia.

Picha hiyo inaonyesha gesi ya moto ikianguka kwenye shimo hilo katika rangi tofauti za machungwa.

Hata hivyo, ukweli ni kwamba shimo hilo jeusi halina rangi. Lakini kile ambacho wataalam wa angani wanaona ni vile vitu vinavyoingia ndani yake na kubadilika kuwa gesi ya moto.

Gesi hiyo inaonekana kubadilika rangi inapokaribia shimo hilo jeusi.



Profesa Heino Falcke ambaye mradi wa shimo jeusi ni pendekezo lake. **PICHA: MTANDAO**

Kama jua linapokuwa nyuma ya mawingu jioni, mwanga kutoka kwa vitu hivyo vilivyobadilika na kuwa gesi moto unalazimika kusafiri kupitia gesi zaidi kuelekea duniani.

Hivyo basi, athari yake itakuwa kubadili rangi na umbo la vitu hivyo karibu na shimo hilo.

Kundi hilo la wataalam linatarajia kuongeza darubini katika eneo la Greenland, Ufaransa na maeneo kadhaa ya bara Afrika na tayari limewasilisha ufadhili kutoka kwa wakfu wa wanasayansi wa kitaifa nchini Marekani (NSF) kutuma setilaiti tatu ndogo angani ili kusaidia uchunguzi huo utakaofanyika kutoka ardhini.

Kulingana na Profesa Falcke, hatua hiyo itasaidia kujenga darubini kubwa yenye ukubwa zaidi ya dunia, itakayoweza kuchukua picha asili ya shimo hilo lililo katikati ya sayari. Profesa Falcke ameiambia BBC News kuhusu mpango wa kundi hilo unaojulikana kama EHT, lenye wanasayansi 347 baada ya kupokea Dola za Marekani milioni tatu, kama tuzo kufuatia ufanisi wake.

Ijapokuwa Profesa Falcke ndiye aliyependekeza wazo hilo na kupigania kupata ufadhili, anasema kwamba tuzo hiyo inatambua juhudi zilizofanywa na kundi lote la wanasayansi hao.

Kundi hilo linashirikisha wanasayansi kutoka Ulaya, China, Afrika Kusini, Japan na Taiwan. **BBC**

UTAFITI

# Jogoo mwenye kelele ashinda kesi dhidi ya jirani zake



Jogoo Maurice hatanyamazishwa tena baada ya Mahakama kumuunga mkono. **PICHA: MTANDAO.**

MAHAKAMA ya Ufaransa, imetoa hukumu ikimuunga mkono mmiliki wa jogoo mmoja baada ya kelele za alfajiri za kuku huyo kuwakera majirani.

Kuku huyo ajulikanaye kwa jina la Maurice kutoka kisiwa cha Oleron katika pwani ya Atlantic, alituhumiwa kwa kuwakera wanandoa waliostaafu wanaomiliki nyumba ya likizo kwenye eneo hilo.

Habari za matatizo yaliyomkabili zilisambaa kote duniani na kupata mashabiki chungu nzima.

Mmiliki wake, Crinne Fesseau amefurahia uamuzi wa kesi hiyo.

"Ni ushindi wa kila mtu aliye katika hali yangu... natumaini uamuzi huo utakuwa wa kuigwa," alinukuliwa na gazeti la AFP akisema.

Wakati wa kusikizwa kwa kesi hiyo mwezi Julai, mawakili wake walisema kwamba malalamiko hayo ni hafifu kwa kuwa kuwika kwa kuku huyo ni hali ya kawaida ya maisha ya taifa hilo.

Fesseau ambaye aliishi kwenye kisiwa hicho cha Oleron kwa miaka 35 katika pwani ya Atlantic, angelazimika kuondoka eneo hilo ama kumnyamazisha kuku wake iwapo Jaji angetoa hukumu dhidi ya jogoo huyo.

Sasa atalipwa Yuro 1000 kama malipo ya kumpotezea wakati wake, mawakili wake walisema Alhamisi wiki iliyopita. Kesi hiyo iliungwa mkono na watu 140,000 katika mitandao ya kijamii waliowasilisha ombi la kupinga.

Jogoo huyo mwenye umri wa miaka minne amekuwa maarufu nchini Ufaransa, ambapo katika nembo ya taifa kuna jogoo. Biashara zimefanywa kwa niaba yake huku barua za kumuunga mkono zikitoka umbali wa hadi Marekani, kulingana chombo cha reuters.

Kesi hiyo iliyopata umaarufu imezua wasiwasi mkubwa kati ya wakazi wanaoishi vijijini nchini Ufaransa na wale wanaohamia maeneo hao ili kuepuka maisha ya mijini.

"Huu ndio uvumilivu, lazima ukubali mila za mitaani," anasema Christophe Sueur, Meya katika kijiji cha Fesseau.

Meya wa mji mwingine, Bruno Dionis du Sejour, aliandika katika barua ya wazi mwezi Mei akitaka kelele za maisha ya vijijini, zikiwemo zile za ng'ombe na kengele za kanisani, ziandikwe kwenye orodha ya urithi wa Ufaransa ili kuwalinda dhidi ya malalamiko kama hayo. **BBC**

> "Sasa atalipwa Yuro 1000 kama malipo ya kumpotezea wakati wake, mawakili wake walisema Alhamisi wiki iliyopita. Kesi hiyo iliungwa mkono na watu 140,000 katika mitandao ya kijamii waliowasilisha ombi la kuipinga.

JE, WAJUA?

# Mimea ya maajabu inayokula wadudu yapandwa Uingereza

MIMEA inayokula nyama iliyo hatarini kuangamia (Watch a carnivorous plant devouring an insect), imeanza kupandwa tena kwenye maeneo kadhaa ya Uingereza katika jaribio la kupunguza kuangamia kwake.

Wataalam wa mimea wanasema kwamba mimea hiyo iliyo na umbo la kuvutia, imetoweka katika sehemu nyingi kutokana na uhaba wa maeneo yenye ardhi zenye unyevu.

Ikiwa na mikono inayoshika na kula wadudu, mimea hiyo ni miongoni mwa makumi ya mimea inayokula nyama nchini Uingereza.

Charles Darwin alifurahishwa sana na aina ya mimea hiyo, na hivyo basi kukusanya picha na vipimo katika kitabu chake kwa jina Insectivorous Plants, kilichochapishwa 1876.

Anasema kwamba aliupendelea sana mmea kwa jina la Drosera, unaofahamika kama Dawy kwa lugha ya Latin, ikilinganishwa na kitovu cha aina zote duniani.

Ni aina iliyo nadra kupatikana kulingana na Joshua Styles kutoka Chuo Kikuu cha Cheshire, ambaye alianzisha hisani yake ya hifadhi kwa jina North West Rare Plant Initiative, kwa lengo la kuhifadhi mazingira.

Nchini Uingereza, mmea huo umeorodheshwa kama ulioangamia na hupatikana chini ya maeneo 20.

"Hivyo basi kutopatikana kwake na hali yake kulinishawishi kutaka kuupanda tena," anasema Joshua Styles.

**JE MMEA HUO UNAPATIKANA WAPI?**

Ulikuwa ukipatikana kwa wingi nchini Uingereza na ulianza kuangamia katika karne iliyopita.

Mabadiliko ya matumizi ya ardhi yamesababisha kukauka kwake katika maeneo yenye ardhi zilizo na unyevu. Hata hivyo, Styles amefanikiwa kupanda mmea huo kutokana na majani yaliyokatwa na yaliyotoka katika mimea michache iliyosalia, ambayo imeweza kustahimili mazingira magumu kwenye eneo la Cumbria.

Alizindua mimea aina 10 katika eneo la Rsley Moss karibu na Warington, akishirikiana na wakfu wa Chesser na ule wa wanyama pori wa Lancashire.

Mmea huo unaokula nyama umestahimili katika mazingira hayo na kuanza kuzaana.

"Kila mwaka wakati unapotoa maua, unatoa makumi ya maelfu ya mbegu ndogo ndogo zinazofanana na vumbi," anasema.

Unapopanda 10 haionekani kama ni mingi, bali idadi ya mbegu zinazotolewa...ninatumaini kupata mbegu nyingi mwaka ujao," anasema.

**MMEA WA SUNDEW (DROSERA ANGLICA)**

Kawaida mimea hujipatia chakula kutoka kwenye mchanga kupitia mizizi yake, lakini mimea inayokula nyama imepiga hatua ya kula protini za wanyama.

Mmojawapo ya mimea hiyo ni wa Sundew ambao una 'mikono' mingi midogo midogo inayotoa maji yenye harufu tamu, ambayo huwavutia wadudu.

Mikono hiyo midogo baadaye huwashika wadudu hao na kuwakamua ndani ya majimaji hayo yanayonata.

Enzymes za mwilini hujitokeza polepole na kuwavunja wadudu hao kuwa chakula chenye virutubishi.

Mtunzaji mdogo kabisa wa bustani alivutiwa na utaalamu wa mimea akiwa na umri wa miaka saba, na amekuwa akisoma mimea tangu hapo.

Anasema ni muhimu kuhifadhi mimea ya kula nyama kwa faida yao kwa mazingira na viumbe hai, na kwa faida ya baadaye, kama vile chanzo kinachoweza kutengeneza dawa mpya. **BBC**



Wadudu huvutiwa na majani ya mmea huo.**PICHA: MTANDAO**

SHERIA

**NA CHRIS TOMASSO**

UCHAMBUZI WA KITABU

# LAW of ATTRACTION HABITS (Sheria za tabia za mvutano)

**MCHAMBUZI: Dk. Raymond Mgeni**



Ustawi wa vijana kama hawa unategemea sana mawazo yao ambayo nayo huibua hisia kisha hatua kuchukuliwa. **PICHA: MTANDAO**

MAISHA yako yalipo sasa ni matokeo ya mambo ambayo umeamua kuyavuta mwenyewe kuanzia katika fikra na hisia unazoruhusu ziwe ndani yako.

Vitabu vingi vimeandika juu ya sheria za asili, na sheria ya mvutano ni moja ya sheria muhimu inayofanya wajuao kuitumia iwavutie kwenye maisha wanayotaka.

Hivi umewahi jiuliza kwanini nina aina hii ya maisha.?

Hili swali linaweza kukufanya uone kuna mambo ambayo hukutaka yawe katika maisha yako lakini yametokea. Jibu la swali hili lipo katika tabia za uvutano zinazoongozwa na sheria mama ya uvutano.

Mtu ni matokeo ya tabia. Tabia huzaliwa na mrudiano wa mawazo na hisia. Hivyo sheria ya uvutano, inaibua mawazo ambayo kadri yanavyojirudia na mtu akaitikia katika kutenda ndipo tabia huzaliwa.

Tabia zinapozaliwa ndizo zinazoongoza maisha ya mtu. Mtu hufikiri na kuzaa mawazo, nayo huibua hisia na kisha kuchukua hatua.

Kadri hatua zitakavyokuwa zikirudiwa basi, tabia hutengenezeka na kukomaa. Tabia zikiwa zimekomaa basi mtu hujikuta akiongozwa nazo iwe kwa kujua au kotukujua.

Mwandishi wa kitabu hiki Chris Tomasso anatushirikisha tabia tano muhimu za kutusaidia kuvuta maisha bora tunayoyataka.

Anaingia ndani katika kutushirikisha tabia za mvutano zilivyo na namna unavyoweza kuzijenga na mwisho kupata matokeo.

Tabia hizi tano ni utambuzi wa kihisia, tahajudi, kuona urahisi wa jambo, kushukuru na kuachilia.

### UTAMBUZI WA KIHISIA

Hii ni tabia inayojengwa ya kumsaidia mtu kutambua hali anayohisi wakati huo. Kujifahamu kihisia kwamba unajisikiaje kwa hali ya sasa ni tabia inayovuta vitu vingi sana kwa watu. Hisia za upendo na furaha unaona namna zinakuwa zikivuta mambo chanya na yenye ubora katika maisha.

Himizo la kujitambua unajisikiaje lina mchango wa kuathiri maisha yako. Hebu fikiria siku ambazo ulikuwa na hisia za uchungu, utaona karibu kila unachokiona nje kikitoa picha ya uchungu na ubaya tu. Hii ni nguvu ya hisia unazokuwa nazo kwa wakati fulani maishani.

Jenga hisia chanya kila siku maishani kwa mambo yoyote ambayo yatakutokea.

Unavyojenga hisia chanya unakaribisha au kutuma mawimbi kuwa asili ikuletee mazingira chanya, watu na fursa ambazo zitakupa uwe na maisha bora.

Hisia chanya huvuta mawazo chanya nayo hukuongoza katika kutenda au kutengeneza tabia bora maishani mwako.

Vile unavyotengeneza hisia za upendo unavuta maisha mazuri kwako na wanaokuzunguka.

### TAHAJUDI

Ni kitendo cha kutuliza akili. Tabia hii hujengwa kwa mazoezi mengi ya kufanya utunze 'fokasi' yako katika kitu kimoja. Wengine huhesabu mapigo ya moyo au mvuto wa pumzi ili tu kuweka utulivu wa akili.

Kwa asili yetu sisi binadamu huwa hatuwezi kutuliza akili kwa muda mrefu katika eneo moja pekee, lazima kutakuwa kuna kuhamahama.

Hivyo tahajudi inakupa nafasi ya kutuliza akili na kufanya mwili uwe katika hali ya utulivu. Zoezi la tahajudi ni la uimarishaji afya na kiroho pia.

Tafuta eneo tulivu na tenga dakika 20 hadi 30 za kutulia huku mawazo yako ukiyaelekeza katika mwendo wa mapigo ya moyo kwa kuhesabu kimoyo moyo au kutulia kuhesabu mivuto ya hewa.

Kadri unavyoweza kutulia na kufuata mwongozo huu utakuja kuona ilivyo kazi kutuliza akili. Utaona namna kidogo tu akili imehama na kufikiria vitu vingine.

Usiogope ukionana na hii hali wala isikutatishe tamaa. Utaweza siku moja kutuliza akili na kujikuta dakika zote hufikirii chochote na hatua hii ndio utaanza kuona tahajudi ina manufaa makubwa ya kukufanya upumzishe akili na mwili na kuepukana na msongo wa mawazo.

### KUONA URAHISI WA JAMBO

Hii ni tabia ambayo imesaidia watu wengi kupata vile walivyotaka kuvipata. Hii ni tabia ya kuona sura ya kitu kuwa ni kitu rahisi na kina nafasi ya kuwezekana kuwa.

Unapokuwa umejitambua hisia ulizonazo, umejipa utulivu wa ndani wa maisha kisha hatua ya kuona maisha katika upande mwepesi unaruhusu asili kuvuta mambo bora kwako.

Usikaribishe hofu au mashaka juu ya maisha yako. Furahia maisha wakati wa sasa, soma kitabu na sikiliza muziki. Yaone maisha katika wepesi nayo yatakuwa.

### KUSHUKURU

Ni tabia inayofanya wengine wasifanikiwe na wengine wafanikiwe. Wasiofanikiwa ni pale wanasahau nguvu ya kushukuru katika vitu walivyonavyo. Hivyo wanasahau walivyonavyo na hata kama vina manufaa kwao, hawataviona vina thamani.

Unapokuwa mtu wa kushukuru katika maisha unakaribisha kupokea zaidi. Kwa kuwa tendo la kushukuru huwa na hisia chanya basi si ajabu ukapata mambo chanya mengi. Shukuru kila siku uendelee kuvuta maisha bora.

> Unapoachilia hisia hasi, basi unatengeneza nafasi kwa hisia chanya. Ndivyo faida kubwa ya kuachilia mambo katika maisha kunavyoweza kukuvutia maisha bora na yenye furaha.

### KUACHILIA

Hii ni kwa vitu usivyoweza kushughulika navyo ambao ni tabia bora. Unavyotengeneza hali ya kuachilia, inakusaidia kukaribisha nafasi ya kupokea mambo mapya.

Unapoachilia hisia hasi, basi unatengeneza nafasi kwa hisia chanya. Ndivyo faida kubwa ya kuachilia mambo katika maisha kunavyoweza kukuvutia maisha bora na yenye furaha.

Usibaki na kitu ndani yako kinachokuumiza kitaharibu maombi ya maisha unayoyataka.

Hivi vitu vyote unapoviunganisha kuwa kitu kimoja, unatengeneza maisha yenye maana kubwa. Kwa kuwa umejua namna mawazo yanavyoathiri matokeo unayopata nje.

Nenda kafanyie kazi na maisha yako yatakuwa bora na kuvuta mambo chanya

Dk.Raymond Nusura Mgeni anapatikana kupitia raymondpoet@yahoo.com
***+255 676 559 211.***
***Dar-es-Salaam***



WADAU
SABATO KASIKA

# Sauti za wadau

MOJA ya changamoto inayozikabili sekondari za vijijini ni ukosefu wa umeme kwa ajili ya maabara, hali inayoweza kukwamisha ndoto za wanafunzi hasa wa masomo ya Sayansi.



### SWALEHE ATIKI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)


KWA hatua ambayo serikali imefikia katika kuboresha elimu nchini, ni ya kupongeza sana ingawa bado kuna changamoto ndogondogo, ambazo hata sisi wananchi wenyewe tunaweza kuzivalia njuga na kuzimaliza.

Ninasema ndogondogo, kwa sababu suala la kufikisha umeme kila kijiji lipo kwenye hatua nzuri, yaani vijiji ambavyo tayari vina umeme vinaweza kuwa vingi kuliko vile ambavyo bado havijapatiwa. Sasa tatizo linalojitokeza ni kwamba nguzo za umeme zinaweza kuwa zimewekwa barabara kuu tu, kinachobaki ni wananchi kuvuta kupeleka katika nyumba zao au taasisi kuvuta hadi kwenye ofisi.

Kwa jambo hili mimi ninaona kuna haja kwa watu ambao umeme umefika kwenye vijiji vyao kuangalia uwezekano wa kukaa na viongozi wao na kuangalia uwezekano wa kuchangia fedha kwa ajili ya kuvuta umeme hadi kwenye shule zao badala ya kusubiri serikali iwavutie wakati ni kwa faida ya watoto wao.

Serikali imeamua kutoa elimu bure kuanzia shule za msingi hadi kidato cha nne, sasa kwanini wanavijiji nao wasione wana wajibu wa kusaidia kuvuta umeme kupeleka katika shule zao? Wakisubiri kufanyiwa kila kitu na serikali watakuwa wamechelewa sana na watakuwa wanachelewesha maendeleo ya watoto wao kielimu.

Hata kama umeme utakuwa haujafika katika vijiji vyao, siku hizi kuna umeme mbadala wa jua, ambao wanaweza kuchangishana na hatimaye wakaupata bila tatizo kuliko kukaa tu wakidhani hawahusiki kuchangia maendeleo ya elimu.



### JAMES MUSYANGI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

CHANGAMOTO hii ipo ingawa serikali inajitahidi kusambaza umeme nchi nzima. Lakini ninaamini kwamba vijiji vingi havina nishati hiyo, na kama upo basi utakuta shule nyingi hazina.

Kwa hiyo katika mazingira hayo ni vigumu wanafunzi wa masomo ya Sayansi kutimiza ndoto zao na mwisho wa siku nchi inakosa wataalam wa baadaye.

Hivyo zifanyike juhudi za makusudi za kuhakikisha tatizo hili linakwisha, ikiwezekana, wazazi washirikishwe hata kununua 'sola' ili itumike katika shule ambazo hazina umeme wa Tanesco.

Njia hiyo inaweza kusaidia wanafunzi au shule kuondokana na tatizo hilo. Kwenye suala hili ni lazima wazazi wakumbuke kuwa shule ni zao, wana wajibu wa kuzihudumia, siyo kushikilia msimamo usio na manufaa wa kusema kwamba serikali imetangaza elimu bure.

Ufike wakati wazazi wajiongeze kwa manufaa ya watoto wao. Ninalisema hili kwa sababu nina uhakika baadhi yao hawataki kusikia habari ya kuchangia maendeleo ya shule, lakini kama wote wangetambua shule ni mali ya wazazi na wana wajibu wa kuzihudumia, basi changamoto nyingi shuleni zingepungua kama siyo kwisha kabisa.

Sioni kama kuna ugumu wowote viongozi wa vijiji kuitisha mikutano na kuwaambia wazazi jambo kama hilo na kulipatia ufumbuzi. Unaweza kukuta sekondari moja ya kata inahudumia wanafunzi wa vijiji viwili hadi vinne.

Je, wakazi wa vijiji hivyo wanashindwa kununua sola au kuchangia fedha ili kuvuta umeme wa Tanesco kweli wanashindwa! Tubadilike tusisubiri kufanyiwa kila kitu.



### STEPHEN MGOMBOZI (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

BILA kumung'unya maneno ni kwamba serikali itekeleze kwa ukamilifu ahadi zake katika sekta ya elimu, kwani ndio msingi wa rasilimali watu inayotegemewa katika sekta zote nchini.

Ikumbukwe kuwa uwekezaji mzuri katika rasilimali watu ndio njia pekee itakayozalisha wataalam au watu wenye ujuzi na maarifa ya kuipeleka Tanzania miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kati.


Siyo siri kwamba sekondari nyingi za vijijini hazina miundombinu muhimu, ukiwamo umeme, ambao kimsingi unahitajika sana kwenye masomo ya Sayansi. Unakuta shule ina maabara lakini haina umeme, ina umeme lakini haina maabara au ina maabara lakini haina jengo.

Sasa katika hali hiyo ni vigumu sana wanafunzi wa masomo hayo kujifunza kwa vitendo.

Kwa kuwa serikali iliahidi kuboresha shule zake, ni vyema utekelezaji huo ukafanyika kwa vitendo kwani kufanya hivyo sekta ya elimu itaboreka huku shule zetu zikiimarika zaidi kwa ubora wa elimu nchini.

Ni kweli serikali ya awamu ya tano imefanya juhudi mbalimbali katika kuinua kiwango cha elimu nchini.

Kwa mfano kudhibiti ubora wa elimu inayotolewa na vyuo vikuu nchini. Dhamira hii iende hadi kwenye shule za sekondari za vijijini kwa kuhakikisha zote zinakuwa na umeme.



### WINIFRIDA ELIAS (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

NAIBU Waziri wa Nishati na Madini, Dk. Medard Kalemani wakati huo kabla wizara haijatenganishwa na yeye kuwa waziri kamili, aliwahi kusema bungeni kuwa katika miradi inayotekelezwa na REA vijijini, kipaumbele kimewekwa kwenye huduma za kijamii kama vile shule, zahanati, vituo vya afya, nyumba za ibada na mashine za kusukuma maji.

Hiyo ilikuwa ni Aprili mwaka 2016 alipokuwa akijibu swali la mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njenza, aliyetaka kujua katika utekelezaji wa Mradi wa REA II Mbeya Vijijini ina vijiji vingapi vya Halmashauri ya Mbeya kama vimo kwenye REA II na mradi utakamilika lini, na pia alitaka kujua kwanini mradi wa REA II haujalenga kupeleka umeme kwenye huduma za kijamii kama vile shule, zahanati, nyumba za ibada na vyuo.

Binafsi ninalichukulia swali hili kwamba lilionyesha wazi kuwa bado kuna changamoto ya ukosefu wa umeme katika maeneo ya vijijini. Na tayari serikali imekuwa ikijitahidi kuhakikisha shule zote za sekondari zina vifaa vya maabara na vitabu vya kutosha.

Majengo kwa ajili ya maabara zote yamejengwa na halmashauri kwa kushirikiana na wananchi. Sasa kwa utaratibu huo huo wa kushirikiana na halmashauri, utumike pia kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenye shule za sekondari.



### BATA ISSA (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)

SHULE za sekondari zilizoko vijijini siyo tu kwamba zinakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa umeme wa uhakika bali pia hazina walimu wa kutosha wa masomo ya Sayansi.

Kwa hiyo hapa kuna mambo mawili ya kutazamwa kwa kina ili hatimaye kuyatafutia ufumbuzi wa haraka.

Ninatambua jinsi ambavyo serikali inavyotilia mkazo ujenzi wa majengo kwa ajili ya maabara, lakini pia kuna haja ya kuongeza walimu wa masomo ya Sayansi na wataalam wa maabara ili kufanikisha lengo la kuwasaidia wanafunzi wanaosoma masomo hayo.

Hatua hiyo ikifanikiwa inaweza kupata wataalam wengi wa baadaye. Shule zote zikiwa na umeme, walimu wa kutosha wa masomo hayo na wataalam wa maabara, itakuwa ni fursa nzuri kwa wanafunzi kujifunza masomo ya Sayansi, kwa kuzingatia kwamba maabara ni lazima zitegemee umeme. Imekuwa ikidaiwa kuwa baadhi ya walimu wa masomo ya Sayansi huwa wanachukuliwa kwa muda na shule kutoka maeneo mengine na kisha wanaondoka.

Sidhani kama utaratibu huo ni suluhisho la tatizo la uhaba wa walimu wa masomo hayo. Kinachotakiwa ni serikali ikaweka utaratibu maalum wa kuwapata walimu wa kudumu shuleni ikiwa ni pamoja na vifaa vya kufundishia. Pamoja na hayo, bado kuna haja ya kushirikisha jamii ya maeneo husika katika suala la upatikanaji wa nishati ya umeme.

# DC apigia debe wenye ulemavu

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

SERIKALI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, imewahamasisha watu wenye ulemavu kujitokeza kugombea nafasi mbalimbali za uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 24, mwaka huu.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Maryprisca Mahundi, wakati akizungumza na Nipashe namna serikali ya wilaya hiyo, ilivyojipanga kusimamia uchaguzi wa serikali za mitaa.

Alisema uchaguzi uliopita idadi ya watu wenye ulemavu kugombea nafasi za uongozi ilikuwa ndogo, hivyo mwaka huu anatamani idadi kubwa kushiriki kwa sababu ni haki yao kikatiba.

"Nawasisitiza watu wenye ulemavu kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi hizo kwa mujibu wa katiba ya nchi kwa kuhakikisha wanachukua fomu za kugombea," alisema Maryprisca.

Aidha, alivitaka vyama vya siasa hususani Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutenda haki kwa wagombea wote bila kuwabagua wenye ulemavu ambao wanaonyesha nia ya kutaka uongozi.

Alisema vyama vya siasa kutokuwa sehemu ya migogoro na ubaguzi katika kuwatafuta wagombea badala yake waangalie uwezo wa mtu badala ya kuangalia umaarufu na uwezo wa fedha.

Aliwafahamisha wananchi kuwa kampeni za uchaguzi huo wa Serikali za Mitaa zitakuwa za siku saba za mwisho yaani kabla ya Novemba 24 mwaka huu ya siku ya uchaguzi na kwamba mgombea atatakiwa kufanya kampeni zake katika eneo lake husika atakalogombea.

**Nawasisitiza watu wenye ulemavu kujitokeza kwa wingi kugombea nafasi hizo kwa mujibu wa katiba ya nchi kwa kuhakikisha wanachukua fomu za kugombea,**

# Wataka kutengewa maeneo ya kilimo

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

WAKULIMA wa parachichi katika Kijiji cha Lunwa, Mbarali mkoani Mbeya, wameishauri serikali kutenga maeneo ya kilimo kwa ajili ya vijana ili waongeze uzalishaji wa zao hilo na kujikwamua kiuchumi.

Ushauri huo waliutoa mwishoni mwa wiki wakati wakipata elimu ya namna bora ya kulima na kuzalisha zao hilo kwa tija na kuendana na teknolojia iliyotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari) kituo cha Uyole.

Mmoja wa wakulima hao, Jacqueline Moses, alisema lengo la serikali ni kuhakikisha nchi inafikia uchumi wa kati, hivyo lazima yatengwe maeneo rasmi kwa ajili ya vijana kufanya shughuli za kilimo.

Alisema kwa sasa kuna kundi kubwa la vijana wasio na ajira, hivyo sehemu pekee itakayowawezesha kujikwamua na umaskini ni kujiingiza kwenye kilimo hususani cha maparachichi ambacho kinafaida kubwa.

"Vijana wengi wako mtaani hawana ajira au shughuli maalum ya kufanya. Kilimo ndiyo ajira ya uhakika iliyobaki lakini changamoto iliyopo ni uhaba wa maeneo ya kufanyia shughuli hiyo. Tunaomba serikali itenge maeneo rasmi kwa vijana ili wajiingize kwenye kilimo cha parachichi," alisema.

Moses alisema licha ya kuwapo changamoto ya ardhi, aliwashauri vijana kutobweteka badala yake watumie fursa zinazopatikana hususan kilimo cha parachichi na kulima kibiashara.

Aliongeza kuwa mradi wa kuhamasisha kilimo cha parachichi utawasaidia kujikwamua kiuchumi na kutoa ajira kwa vijana na kuahidi kufuata maelekezo wanayopewa na wataalamu wa kilimo.

Ofisa Ugani Kata ya Igurusi, Pius John, alisema mradi wa parachichi utarahisisha upatikanaji wa mbegu ukilinganisha na ilivyokuwa awali wakulima kufuata mbegu hizo kwenye vituo vya utafiti, huku akiongeza kuwa uelewa mdogo wa wakulima juu ya kilimo ni changamoto.

Mtafiti wa Matunda kutoka Tari- Uyole, Daud Mbongo, alisema wakulima wajikite katika kilimo cha parachichi kwa sababu ni zao linalolipa kwa sasa.

Alisema mradi wa parachichi katika kijiji hicho utakuwa na tija kwa wakulima hao kwa kuwa watazalisha kwa kuzingatia teknolojia ya kisasa na kusisitiza kuwa taasisi hiyo itaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa wakulima.




Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Benki ya NMB, Filbert Mponzi (katikati), akijadiliana jambo na Mkuu wa Mkoa wa Mara, Adam Malima (kushoto), walipohudhuria mkutano wa Jukwaa la Biashara baina ya Tanzania na Uganda, lililofanyika jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**.

# Wapongeza mfumo stakabadhi ghalani

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya imekiri kuwa mfumo wa stakabadhi ghalani kupitia zao la kakao umesaidia kupunguza idadi ya wafanyabiashara waliokuwa wanakwenda kununua moja kwa moja kwa wakulima na kukwepa ushuru.

Kuanzishwa kwa mfumo huo, umesaidia ongezeko la kampuni zinazonunua zao hilo kwenye Chama Kikuu cha Ushirika wilayani Kyela na kurejesha sehemu ya faida kwa wananchi.

Akizungumza na Nipashe mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Kim's Chocolate, kupitia kampuni tanzu ya Bioland inayonunua zao hilo, Fons Maex, alisema wilaya ya hiyo ni miongoni mwa maeneo wanayoyategemea kupata zao hilo ili waweze kuendesha kampuni yao.

Alisema kwa sasa wakulima wananufaika na zao hilo kupitia mfumo wa stakabadhi ghalani ambao ulianzishwa na serikali kupitia vyama vya ushirika.

Maex alisema utaratibu huo umesaidia wakulima kuwa na uhakika wa soko na bei inayoridhisha kulinganisha na ilivyokuwa awali ambapo wakulima walikuwa wakiuza kiholela.

"Wakulima wa kakao sasa wananufaika. Hii inatokana na jitihada za serikali kuhimiza kujiunga kwenye vyama vya ushirika na kampuni zimeingia kwenye ushindani wa kununua zao hilo kupitia ushirika na kwa bei elekezi," alisema Maex.

Alisema kwa kutambua mchango huo kampuni iliamua kufanya miradi mbalimbali ya maendeleo ikiwamo ujenzi na ukarabati vyumba vya madarasa katika shule za msingi.

Alisema kampuni hiyo imejenga zaidi ya vyumba 500 vya madarasa na sasa inapanga kutumia zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwenye shule za msingi.

Katika Risala yake Mwalimu wa Shule ya Msingi Mpanda, Doliglas Mwalukasa, alisema shule hiyo inakabiliwa na upungufu wa vyumba vya madarasa ambapo mpaka sasa kuna vyumba nane na hitaji ni vyumba 10.





# Askofu asema kanisa limepoteza mwelekeo

Na Paul Mabeja, DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Mennonite, Dayosisi ya Kati, Amos Muhagaji, amesema makanisa duniani yamepoteza mweleko kutokana na kuunga mkono mambo yasiyompendeza Mungu ikiwamo ndoa ya jinsia moja.

Muhagaji aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua kongamano la tisa la kitaifa la wajane jijini Dodoma.

Alisema hivi sasa makanisa mengi duniani yamepoteza mwelekeo hali ambayo kama haitafanyiwa kazi mapema, kuna uwezekano wa vizazi vya sasa kuacha kabisa kwenda makanisani.

"Kule wenzetu ambao ndiyo walituletea hii dini hivi sasa haya makanisa makubwa yanauzwa na watu wanaanzisha vitu vingine. Hata yale makanisa yaliyobakia wanaokwenda kusali ni wazee pekee yao," alisema Askofu Muhagachi.

Alisema moja ya sababu ambazo zimekuwa zikichangia hali hiyo ni makanisa kuunga mkono vitendo ambavyo si mpango wa Mungu kama vile ndoa ya jinsia moja na mambo mengine yasiyo mpenda Mungu.

"Mimi wakati nafanya utafiti wangu nchini Marekani nilikuta kanisa linaongozwa na askofu shoga, lakini hawa wachungaji mashoga ndiyo usiseme na ndoa za jinsia moja zinafungwa kila siku makanisani. Hali ile mimi ilinikera sana sasa kama hatutakuwa na mpango mzuri wa kulinusuru kanisa, basi miaka ijayo hata sisi hapa vijana hawatashiriki kabisa ibada makanisani," alisema.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo wa kiroho, utafiti unaonyesha kuwa katika miaka 20 ijayo, Afrika hali itakuwa kama ilivyo nchini Marekani na nchi zingine za Ulaya ambako vijana wengi hawataingia makanisani.

"Nikiwa nchini Marekani siku moja kutokana na watu wanaokutokuja kanisani ilibidi kwenda katika nyumba na kuwagongea kuita waje kanisani lakini ukienda mtu anatoka na Dola 500, anasema nenda kampe Mungu kanisani mimi nikawaambia hatutaki hela yako na yeye anakujibu kama hutaki basi toka mlangoni mwangu. Hali hii si nzuri kabisa kwa kanisa tena," alisema.

Kuhusu kongamanao hilo, askofu huyo alisema wajane nchini bado wanakumbana na changamoto mbalimbali ikiwamo unyanyasaji wa kijinsia.

"Wajane nchini bado wanakumbana na changamoto kubwa sana hasa pale baada ya kufiwa na waume zao. Wanabaki na majeraha makubwa na sisi viongozi wa dini tunawatelekeza kabisa bila hata kwenda kuwajulia hali. Tunasahau wajibu wetu kabisa," alisema Askofu Muhagachi.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Amazing Grace, ambayo iliandaa na kuratibu kongamano hilo, Paul Mwaga, alisema lengo la kuwakutanisha wajane hao ni kuwajengea uwezo ili kujiamini na kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Alisema wajane wengi wanaishi katika maisha ya mateso makubwa kutokana na kudhulumiwa mali na ndugu wa waume zao baada ya kufa. Mwanaga alisema pia katika kongamano hilo wajane watapatiwa masomo yatakayo wawezesha kuwajengea stadi za maisha na kazi.

Zaidi ya wajane 120 wanashiriki katika kongamano hilo kutoka makanisa tofauti 10 nchini pamoja na wengine kutoka nchi za Congo, Kenya na Malawi.



Mwelimishaji Terry Gbemundu maarufu Mama Terry (kulia), akitoa elimu kwenye warsha ya kukabiliana na msongo wa mawazo sehemu za kazi, kwenye ndoa na familia iliyowashirikisha wabunge, wafanyakazi na wanandoa iliyoandaliwa na Shirika la Endless Success Foundation (ESUFO), jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Msongo mawazo chanzo mifarakano ya ndoa

Na Ibrahim Joseph, DODOMA

IMEELEZWA kuwa msongo wa mawazo ni chanzo cha mfarakano na ugomvi katika familia nyingi pia husababisha kuathiri ufanisi sehemu za kazi.

Hayo yalielezwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Endless Success Foundation (Esufo), Amina Feruzi, wakati wa warsha ya kukabiliana na msongo wa mawazo sehemu za kazi, kwenye ndoa na familia iliyohusisha wabunge, wanandoa na wafanyakazi wa ofisi mbalimbali inayofanyika jana jijini hapa.

Mkurungenzi huyo alisema msongo wa mawazo umekuwa chanzo cha changamoto ya migogoro mingi na mafarakano katika familia na kuvunjika kwa ndoa nyingi.

"Hii ni changamoto kubwa sana ndiyo maana shirika letu tumeona tutoe mafunzo kwa watumishi wa umma na wanandoa ili kuwajengea uwezo wa kuyabaini haya," alisema.

Aliongeza msongo wa mawazo umesababisha hata kupunguza ufanisi sehemu za kazi ofisini, hali ambayo inahitaji elimu ya kutoka huko.

Feruzi alisema msongo wa mawazo unaweza kuanzia ofisini au nyumbani na unasababisha mhusika kushindwa kufanya kazi au majukumu kwenye eneo lake.

"Unaweza kumkuta mtu nyumbani au ofisini anakuwa na hasira kila anayemgusa ni tatizo. Kumbe mtu huyo ana msongo wa mawazo. Msipomsaidia anaweza kuharibu kazi au familia," alisema.

Pia alisema msongo wa mawazo umekuwa chanzo cha kuvunjika kwa ndoa nyingi na kusababisha familia za wahusika hasa watoto kukosa mwelekeo wa maisha.

Alisema warsha hiyo ina lengo la kuwajengea uwezo makundi hayo ili kwenda sambamba na namna ya mbinu za kukabiliana na msongo wa mawazo na kuongeza kuwa shirika hilo lina fanyakazi kwa nchi nzima na wanatoa ushauri wa kuondoa msongo wa mawazo kwa makundi mbalimbali na mtu mmoja moja.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge inayoshughulikia masuala ya Ukimwi na Dawa za kulevya, Oscar Mukasa, alilishukuru shirika hilo kwa kuandaa mafunzo hayo kwa makundi hayo.

Mukasa alisema kuna baadhi ya changamoto za masongo wa mawazo zisiposhughulikwa zitaendelea kuleta madhara katika jamii na familia.

"Tumekuwa tukikutana na watu hawa kila siku ofisini na kuna wakati tunasema mtu huyo hafai kumbe ni msongo wa mawazo. Kuna wengine wanajiua kumbe ni msongo wa mawazo. Kweli tunahitaji msaada ili kupunguza changamoto hii," alisema.

Alisema jamii ikijengewa uwezo wa kuyabaini hayo itasaidia kuokoa ndoa na mafarakano sehemu za kazi ili kuendeleza uchumi wa nchi.

Alishauri wafanyakazi, wabunge na wanafamilia waliopata mafunzo hayo kupeleka elimu hiyo kwa makundi mengine ili kunusuru kizazi hiki na majanga yanayojitokeza.

# Vijana kuwezeshwa kuzitambua fursa

Na Paul Mabeja, DODOMA

VIJANA wa vijiji sita Chamwino mkoani Dodoma, wanatarajia kunufaika na mafunzo ya mradi wa kuwajengea uwezo ili kutambua na kukamata fursa zilizipo katika maeneo yao.

Hatua hiyo itawasaidia kuondokana na dhana ya kukimbilia mjini kwa madai ya kwenda kutafuta ajira.

Mradi huo ambao utatekelezwa na shirika lisilo la kiserikali la Mtandao wa Mazingira Dodoma (Donet), utagharimu Sh. milioni 40 chini ya ufadhili wa The Foundation for Civil Society (FCS).

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Donet, Joshua Mshuda, alisema lengo la mradi huo ni kuwawezesha vijana wa vijiji kuondokana na tabia ya kukimbilia mjini kutafuta ajira.

Alisema hivi sasa vijana wengi wa vijijini wamekuwa na tabia ya kukimbilia mjini kwa madai kuwa wanakwenda kutafuta ajira na kushindwa kutambua kuwa vijijini ziko fursa ambazo zinaweza kuwakwamua kiuchumi.

"Lengo lingine ni kuhahakikisha mradi huu unawawezesha vijana wa vijiji katika kukamata fursa zilizoko katika maeneo yao pamoja na kuwawezesha kuanzisha shughuli rafiki katika maeneo yao ili kujiinua kiuchumi na kuboresha maisha yao," alisema Mshuda.

Alisema walengwa wa mradi huo ni vijana wa kike na kiume wenye umri kati ya miaka 18 na 35.

"Mradi huu utatekelezwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino katika kata za Dabalo, Chilonwa, Membe na Msanga katika vijiji sita ambavyo ni Msanga, Nzali, Membe, Dabalo, Chilonwa na Igamba. Muda wa utekelezaji ni miezi minane kutoka Julai 2019 hadi Februari 2020," alisema Mshuda.

Aliwataka vijana kuhakikisha kuwa wanajitokeza kwa wingi ili kupata fursa hiyo ya mafunzo ambayo yatawajenga kujitegemea kupitia fursa zilizoko katika maeneo yao.

"Mafunzo hayo tunayotoa kwa vijana hawa, yatawezesha kuwajengea uwezo katika kutambua na kukamata fursa zilizopo bila kujali eneo wanaloishi ili kubaini fursa zilizoko ambazo watazitumia kuanzisha miradi ya kimaendeleo na kuendesha maisha yao pamoja na familia zao kwa ujumla," alisema Mshuda.



## HABARI ZANZIBAR

# Dk. Shein aridhishwa ushirikiano na Cuba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Ali Mohamed Shein, amesema serikali inathamini ushirikiano uliopo katika sekta ya afya na nchi ya Cuba imo katika ushirikiano na Zanzibar ya kusomesha madaktari na tayari kuna madaktari 15 wanasoma nchini humo, katika Chuo Kikuu cha Mantanzas.

Alisema kutokana na juhudi hizo, ipo haja ya kuendelezwa ushirikiano zaidi kwa Jamhuri ya Watu wa Cuba kutoa nafasi ya masomo ya udaktari bingwa kwa madaktari wa Zanzibar hasa ikizingatiwa kuwa Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), kimeshaanza kutoa wahitimu mbalimbali wa fani hiyo.

Akizungumza na Naibu Waziri wa Kwanza wa Wizara ya Mambo ya Nje ya Jamhuri ya Watu wa Cuba, Marcelino Medina Gonzalez, Ikulu mjini Zanzibar, Dk. Shein aliipongeza Cuba kwa kuendeleza ushirikiano kwa kuwa pande mbili hizo zina historia kubwa hasa ikizingatiwa kuwa nchi ni miongoni mwa za kwanza kuyatambua Mapinduzi matukufu ya Zanzibar ya Januari 12, 1964.

Dk. Shein alisisitiza haja ya kuendeleza uhusiano na ushirikiano katika sekta ya utalii hasa ikizingatiwa kuwa Cuba imepiga hatua kubwa katika sekta hiyo.

Alieleza mafanikio makubwa yaliofikiwa na Cuba katika sekta ya utalii hasa katika eneo la ukanda wa utalii unaojulikana kwa jina la Varadero, ambao unavivutio kadhaa vya kitalii zikiwamo hoteli za kisasa za hadhi ya juu, maeneo ya kihistoria na fukwe za kuvutia.

Alisema Jamhuri ya Watu wa Cuba na Tanzania ikiwamo Zanzibar ni marafiki wa damu na urafiki wao umekuwa ukiimarika hivyo kuna kila sababu za kuuimarisha zaidi kwa manufaa ya pande zote mbili.

Dk. Shein alimweleza kiongozi huyo jinsi Muungano uliopo kati ya Zanzibar na Tanganyika ambao uliasisiwa Aprili 26, 1964 kuwa ni wa kihistoria na wapekee hadi hivi sasa kwa nchi za Bara la Afrika.

Kwa upande wake Gonzalez alimweleza Dk. Shein jinsi ya nchi yake inavyofarajika na uhusiano na ushirikiano wa kihistoria uliopo kati yake na Zanzibar na kuahidi kuuendeleza.

Gonzalez aliyefuatana na Balozi wa Cuba nchini, Profesa Lucas Domingo Hernades, alisema ujio wake umezidi kutoa fursa ya kuendelezwa kwa ushirikiano katika sekta mbalimbali za maendeleo na umewakutanisha na viongozi kadhaa na hatimaye kujadiliana kuhusu sekta hizo.

Alisema miongoni mwa sekta hizo ni afya, elimu, utalii, kilimo, biashara na kusisitiza kuwa iwapo ushirikiano zaidi utaendelezwa kupitia sekta hizo, mafanikio zaidi yataendelea kupatikana kwa pande zote mbili.

Alimhakikishia Rais Dk. Shein kuwa Jamhuri ya Watu wa Cuba, itaendelea kuiunga mkono Zanzibar katika kuimarisha sekta ya afya ikiwa ni pamoja na kuendeleza ushirikiano wa kuwasomesha madaktari wazalendo nchini Cuba katika vyuo vyake mbalimbali kikiwamo Chuo Kikuu cha Mantanzas.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Kata ya Rusoli, Musoma Vijijini mkoani Mara, Sabato Mkome (kushoto), akikabidhi hati ya heshima kwa kutambua jitihada za Mbunge wa jimbo hilo, Prof. Sospeter Muhongo katika kuhamasisha maendeleo, kwa msaidizi wake Hamisa Gamba katika hafla iliyofanyika juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**.

# Vijana 16 waenda Qatar kujifunza kulea watoto

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMLA ya vijana 16 wa kike wanatarajiwa kuondoka leo kuelekea nchini Qatar kupata mafunzo ya kazi na ajira kwa fani ya ulezi wa watoto.

Vijana hao ambao wamesafirishwa na Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto Zanzibar wameagwa na kukabidhiwa tiketi, visa, mkataba, hati ya kusafiria na fedha taslimu kwa ajili ya kujikimu na Waziri wa Wizara hiyo, Moudline Castico.

Akizungumza katika hafla hiyo, Castico aliwataka vijana hao wawe na tabasamu kwa watoto watakaowasimamia na kuwalea kwa misingi ya mila na tamaduni zao.

Alisema kuwa wanakwenda huko kulea watoto ambao watakuwa ni viongozi wa baadaye ambao wanapaswa kulelewa katika misingi iliyo bora.

Naye Mkurugenzi wa Ajira wa Wizara hiyo, Ali Ameir, alisema kuwa mchakato wa kuwapata vijana hao ulifanyika kwa awamu mbili na vijana 90 walijitokea kuomba na kupatikana 16 ambao ndio wanasafiri leo.

Alisema kuwa fursa za kusafirisha vijana kwenda nchini Qatar, mchakato wake ulianza 2014 na kutiwa baraka 2018 ambapo walisafirisha vijana 35 kwa nafasi ya udereva na mwaka huu kuna utaratibu mpya ambao vijana hao watapata mafunzo ya kazi kwa muda wa mwaka mmoja na baadaye watafanya ajira kwa miaka miwili.

Hata hivyo, alisema kuwa nafasi zilizokuwa zinatakiwa ni 30, lakini wamepatikana 16 baada ya 14 kukosa sifa.

Alisema wanatarajia mwakani idadi ya vijana itaongezeka, lakini itategemea na huduma ambazo watazitoa.

Akitoa shukrani zao kwa niaba ya wazazi wenzake, Hamad Suleiman Hamad, aliishukuru serikali kufanya hivyo na kumwomba Mungu awawezeshe vyema katika kufanya kazi zao.

# Bil. 1.8/- zatengwa ukarabati hospitali Pemba

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema imetenga jumla ya Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya ukarabati mkubwa hospitali ya Chakechake Pemba, kufikia kiwango cha hospitali ya rufani.

Naibu Waziri wa Afya, Harusi Said Suleiman, alisema hayo wakati akitoa ufafanuzi kuhusu mikakati ya Wizara ya Afya kuimarisha huduma za afya katika kisiwa cha Pemba.

Alisema katika Wilaya ya Chakechake, serikali itaifanyia ukarabati mkubwa hospitali hiyo ili kuwa na sifa na hadhi ya kutoa huduma zote muhimu kwa wananchi.

Alisema kwa kuanzia ukarabati huo utahusisha wodi ya watoto pamoja na wajawazito na jengo la utawala.

Alisema maandalizi yote ya ukarabati huo yamekamilika na kazi hizo zinatarajiwa kufanywa na wakala wa majengo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

"Katika kuimarisha huduma za afya kisiwani Pemba, serikali imetenga Sh. bilioni 1.8 kwa ajili ya ukarabati mkubwa wa Hospitali ya Chakechake Pemba ili iwe na hadhi ya hospitali ya rufani kwa kutoa huduma muhimu za tiba kwa wananchi," alisema.

Suleiman alisema kuimarishwa kwa huduma katika hospitali ya Chakechake kwa kiasi kikubwa kutapunguza tatizo la baadhi ya wagonjwa kupelekwa mkoani kwa ajili ya kupata huduma za afya.

Kwa upande wao wananchi wa kisiwa cha Pemba walisema kuwa kujengwa kwa hospitali hiyo, kutarahisisha kupata huduma za afya bila ya usumbufu.

"Kukarabitiwa kwa jengo hili itarahisiha upatikanaji wa huduma za afya hasa kwa sisi kinamama na watoto kwa sababu wodi ya kinamama na watoto ni ndogo, lakini jengo hilo limechakaa hivyo linatishia amani ya wagonjwa wanaofika hospitalini hapo," alisema Asha Hamad, mkazi wa Chakechake, Pemba.

# Wahitimu mafunzo ya kijeshi waaswa uhalifu

**Na Dege Masoli,** HANDENI

MKURUGENZI wa Suma-JKT, Kanali Rajab Mabele, amewaonya vijana wanaopitia mafunzo ya kijeshi nchini kutojihusisha na matendo ya kihalifu, badala yake watambue jukumu lao ni kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama ili wawe mikono salama na taifa lao.

Kanal Mabele alitoa onyo hilo kwenye hafla fupi ya kufungwa kwa mafunzo ya vijana Operesheni Makao Makuu Dodoma wanaomaliza kwa mujibu wa sheria katika kambi ya kijeshi la Mgambo JKT wilayani Handeni.

Aliwaonya vijana wanaobahatika kupitia mafunzo ya kijeshi nchini kuepuka vishawishi vya uvunjifu wa amani, na kwamba kufanya hivyo watakuwa wamekiuka lengo la serikali la kuwapa mafunzo hayo kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kujitegemea, kujilinda wao na taifa kwa ujumla.

Alisema kukubali kutumika vibaya kwenye matendo ya kihalifu ni usaliti dhidi ya nchi yao na badala yake watambue jukumu lao kuwa pamoja na mambo mengine kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama kufichua, kukabiliana na kuzuia uhalifu.

"Malengo ni kuwajenga vijana katika malezi ya pamoja, upendo, mshikamano na katika maadili mema na ndiyo maana tumechukua makundi mbalimbali na ya aina zote ya vijana hapa kambini... sasa zingatieni kiapo chenu," alisisitiza Kanali Mabele.

Katika risala ya wahitimu hao walitoa kero kadhaa pamoja na ushauri kwa serikali, huku wakisisitiza kuwa wazalendo kwa nchi yao kwa kutii amri zilizopo na zitakazotolewa mara kwa mara kwao.

Kamanda wa Kikosi cha Mgambo JKT, Meja Adrew Lwanda, katika taarifa yake, alisema jumla ya vijana 1,290 kati ya 1,314 wamehitimu mafunzo hayo ya miezi mitatu na kwamba 24 hawakumaliza kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo utoro.



Wafanyakazi wa Bima ya AAR wakiwa katika hafla ya kumpongeza Mkurugenzi wao Violet Mordichai, kwa kushinda tuzo ya Mkurugenzi Bora wa Bima Tanzania iliyotolewa na WIBF (Women in Insurance and Banking Forum) jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri yawezesha vijana pikipiki 70 kwa ajira

**Na Juster Prudence,** TUDARCo

HALMASHAURI ya Jiji la Tanga imetoa pikipiki 70 zenye thamani ya Sh. milioni 182 kwa ajili ya kuwawezesha vijana kujiajiri.

Akizungumza wakati wa utoaji wa pikipiki hizo jana, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Martine Shigela, alisema mikopo hiyo waliyopewa haina riba hivyo watarudisha fedha ileile waliyokopeshwa huku akiwataka kurejesha kwa uaminifu ili na wengine waweze kukopeshwa.

"Kwanza mikopo hii haina riba kwa hiyo utarudisha fedha ileile uliyokopeshwa ni vema tukatumia vizuri pikipiki hizi tuweze kurejesha mikopo halmashauri na watu wengine waweze kukopa," alisema Shigela.

Alisema Halmashauri ya Jiji la Tanga imekuwa kinara wa kutoa mikopo kwa wananchi ikiwa ni pamoja na mkopo wa cherehani zenye thamani ya Sh. milioni 100 walizopewa walemavu na wanawake katika kata mbalimbali za mkoa huo.

Pia aliwaomba wananchi wa Tanga kutotumia mikopo ya pikipiki hizo kwa ajili ya kuzunguka mtaani na badala yake wazitumie kwa utaratibu mzuri ili ziweze kuwanufaisha wao pamoja na mkoa mzima wa Tanga.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii Jiji la Tanga, Dorah Tumbo, alisema halmashauri itatoa ofisi kwa wanakikundi wanufaika wa mkopo huo na kushirikiana na Kamanda wa Usalama Barabarani watatoa mafunzo ya usalama na ujasiriamali ili waweze kuendesha shughuli zao kwa ufanisi zaidi.

Wananchi ambao ndiyo wanufaika wa mkopo huo waliishukuru halmashauri kwa

# Usafiri maji wapandisha mapato TRA Mwanza

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

USAFIRI wa maji kusafirisha bidhaa kupitia Bandari ya Mwanza, umepandisha mapato ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Mwanza.

Mapato kwa kipindi cha miezi miwili yamepanda kwa zaidi ya Sh. bilioni 10.3.

Akizungumza na wafanyabiashara wanaotumia bandari na uwanja wa ndege kusafirisha bidhaa zao Meneja TRA Mkoa wa Mwanza, Joseph Mtandika, alisema ongezeko hilo limekuja baada ya kuanza kutumika kwa bandari hiyo kusafirisha bidhaa, hivyo kuwa chanzo cha pato kuongezeka.

"Kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kumekuwa na ongezeko la mapato ya zaidi ya Sh. bilioni 10.3 kwa Julai na Agosti ukilinganisha na mwaka wa fedha 2017/2018, ambapo kwa Julai na Agosti tulikusanya Sh. bilioni 8.3," alisema Mtandika.

Mmoja wa wafanyabiashara wa Mkoa wa Mwanza, Brown Mushi, aliwaomba wafanyakazi wa forodha na Jeshi la Polisi kushirikiana ili kuondoa usumbufu wanaopitia wakati wa usafirishaji wa bidhaa zao inayopelekea kucheleweshwa kuziingiza sokoni, hivyo kusababisha serikali kutopata mapato kwa muda.

Alisema changamoto wanayokumbana nayo ni makadirio wanayokadiriwa ambayo yanawasababishia kutotendewa haki kwa kuwa bidhaa wanazouza wenyewe ndio wanajua wamenunuaje na watauzaje.

"Wafanyabiashara tunashindwa kuaminika na baadhi ya mamlaka katika mazingira tunayofanyiwa ukaguzi, hivyo inatusababishia kucheleweshwa njiani kwa kukamatwa na askari wa usalama barabarani wakidai baadhi ya nyaraka na hata tukiwapa hawana ujuzi wa kuzielewa na kusababishia usumbufu," alisema Mushi.

Naye Meneja Msaidizi wa Forodha Mkoa wa Mwanza, Christopher Sojo, alisema soko la Afrika Mashariki lina unafuu wa kodi kwa bidhaa ambazo zimetengenezwa ndani ya nchi za ukanda huo, hivyo ni fursa kwa wafanyabiashara kutumia Bandari ya Mwanza Kusini ili kupunguza gharama za biashara.

"Tungependa kuwa na wafanyabiashara ambao hawajihusishi na magendo wala biashara haramu na ikitokea hivyo wafanyabiashara wengine watoe taarifa katika mamlaka husika ili ziweze kuchukuliwa hatua kuhakikisha mapato ya nchi hayapotei," alisema Sojo.

# Maandalizi mazishi ya Mugabe yakamilika

**HARARE,** Zimbabwe

MWILI wa Rais wa zamani wa Zimbabwe, Robert Mugabe unatarajiwa kuwasili kesho nchini humo katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Robert Gabriel Mugabe mjini Harare.

Mugabe (95), alifariki dunia wiki iliyopita akiwa hospitalini nchini Singapore baada ya kuugua kwa muda mrefu.

Kwa mujibu wa Shirika la Habari la Reuters taarifa ya serikali ilitumwa kwenye ofisi za ubalozi Jumapili na kusema ibada ya mazishi ya Mugabe itafanyika katika uwanja wa taifa wa michezo mjini Harare siku ya Jumamosi na mazishi siku moja baadae.

Taarifa zilieleza kuwa wakuu wa nchi mbalimbali watakaohudhuria maombolezo hayo wataondoka mara moja kwa sababu maofisa wa serikali ya Zimbabwe watakuwa na shughuli nyingi za maandalizi ya mazishi hayo.

**Mugabe (95), alifariki dunia wiki iliyopita akiwa hospitalini nchini Singapore baada ya kuugua kwa muda mrefu.**

Lakini hadi jana, mwili wa Mugabe ulikuwa bado haujawasili nchini humo kutoka Singapore, na kwamba mjane wa marehemu, marafiki wa karibu pamoja na maofisa wa serikali nao wamebakia Singapore.



Gazeti la The Obsever juzi lilimnukuu msemaji wa chama cha siasa cha ZANU-PF, Simon Khaya Moyo akieleza kuwa Mugabe atazikwa katika makaburi ya mashujaa na shughuli za kuaga mwili wake zitafanyika katika uwanja wa taifa na idadi kubwa ya viongozi mashuhuri kutoka Afrika wanatarajia kuhudhuria. **VOA**



Wanajeshi wa Burkina Faso wakiwa katika operesheni ya kijeshi inayoendelea kati ya maeneo ya Guendbila na Baaalogho. **PICHA: AFP**

# Iran yapuuza vitisho vya Marekani

**TEHRAN,** Iran

MELI ya mafuta iliyokuwa ikishukiwa kujaribu kufikisha mafuta ya Iran nchini Syria licha ya vikwazo vya kimataifa hatimaye imeuza shehena iliyokuwa ikisafirisha.

Picha za satelaiti zilizotolewa zilionesha kuwa meli hiyo iitwayo Adrian Darya-1, ilikuwa karibu na pwani ya Syria mpaka Ijumaa.

Hata hivyo, Msemaji wa Wizara ya Mambo ya Nje wa Iran, Abbas Mousavi alisema meli hizo imefikisha mzigo baada ya kutia nanga kwenye pwani ya bahari ya Mediterania.

Meli hiyo imekuwa katika mzozo wa kidiplomasia baina ya Marekani na Iran, na ilikuwa imebeba shehena ya mapipa ya mafuta milioni 2.1.

Picha za Setilaiti zilitolewa na kampuni ya Maxar ambazo zilionyesha eneo la Adrian Darya maili kadhaa kwenye ufukwe wa badanri ya Syria wa Tartus Ijumaa.

Meli hiyo ilikamatwa na wanajeshi wa Uingereza karibu na pwani ya Giblatar Julai, mwaka huu na kushikiliwa mpaka Agosti 15 baada ya Iran kutoa hakikisho kuwa meli hiyo haitaelekea Syria.

Marekani imeshatoa onyo la kumuwekea vikwazo vya kiuchumi yeyote atakayenunua mafuta hayo.

Ofisa wa Hazina ya Marekani, Sigal Mandelker alisema: "Tutaendelea kuiwekea shinikizo Iran na kama Rais (Trump) alivyosema hakutakuwa na msamaha wa aina yeyote kwa mafuta ya Iran.

Wakati huohuo, Wizara ya Mambo ya Nje ya Iran imesema kuwa meli ya mafuta yenye usajili wa Uingereza ambayo ilikamatwa na Iran kwa kile wengi walichoona kuwa ni kulipiza kisasi inakaribia kuachiwa.

Mousavi alisema Meli ya Stena Impero ipo katika hatua za mwisho za kisheria nchini Iran na itaachiliwa hivi karibuni.

Stena Impero ilitiwa nguvuni na mamlaka za Iran Julai 19, kwa kile kilichoitwa kukiuka sheria za bahari - na Iran imekanusha vikali kuwa imefanya hivyo kulipiza kisasi baada ya meli yake kukamatwa na wanamaji wa Uingereza.

Tukio hili lilitokea wakati kukiwa na mvutano kati ya Uingereza, Marekani na Iran. Julai 9, mwaka huu Uingereza ilieleza tishio la usalama katika maji ya Iran kwenye Ghuba ni kubwa.

Wakati huohuo, Marekani ilidai kuwa ilidungua ndege isiyo na rubani kwenye Ghuba, baada ya Iran kushambulia ndege isiyo na rubani katika eneo hilo Juni.

Raisi wa Marekani Donald Trump alieleza kuwa atafanya mazungumzo na Uingereza kufuatia madai kuwa Iran imeikamata meli iliyosajiliwa nchini Uingereza. **BBC**

# Kiongozi waasi ahimiza kinga dhidi ya ebola

**KINSHASA,** Congo

KAMANDA mmoja wa kundi la wapiganaji la Maimai amejitenga na wenzake na kuwataka raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) kujikinga dhidi ya maambukizi ya ugonjwa wa ebola na wasiwashambulie watabibu.

Kwa mara ya kwanza kabisa, tangu kuripuka kwa homa ya ugonjwa wa ebola katika mikoa ya Kivu ya kaskazini pamoja na Ituri kaskazini mashariki ya Congo, kamanda huyo amesimama kidete na kuwahamasisha wakazi kujikinga dhidi ya ugonjwa wa ebola na kutowashambulia matabibu wanaoshiriki katika vita dhidi ya homa hiyo ambayo kwa sasa imesababisha vifo vya watu zaidi ya 2000 tangu kuripuka agosti mwaka 2018.

Akiwahutubia wakazi wa Mataba, kitongoji kilicho umbali wa kilomita 15 kusini mwa mji wa Beni, kabla ya kupata chanjo dhidi ya homa ya ebola, Jenerali Kambale Mayani wa kundi la UPLC alisema, makundi ya Maimai yanayowashambulia watabibu pamoja na kuvishambulia vituo vya afya wanapaswa kuacha mara moja. **DW**

# Brexit yamng'oa waziri

**LONDON,** Uingereza

HALI ya kisiasa nchini Uingereza imeendelea kuzorota, kufuatia kujiuzulu kwa mmoja wa mawaziri wa ngazi ya juu katika serikali ya Boris Johnson.

Waziri wa Wafanyakazi na Malipo ya Uzeeni, Amber Rudd, aliuacha wadhifa wake na kudai kwamba Waziri Mkuu, Johnson hafanyi vya kutosha katika kutafuta muafaka unaostahili kabla ya nchi hiyo kujiondoa katika Umoja wa Ulaya (Brexit).

Rudd alisema hajaona ushahidi wowote kuwa Johnson anatafuta makubaliano yoyote kabla ya tarehe ya mwisho iliyowekwa ya nchi hiyo kuondoka kabisa kwenye umoja huo.

Katika barua yake ya kujiuzulu, waziri huyo alisema: "Serikali ya Johnson inatumia muda na rasilimali nyingi kujitayarisha kuondoka kwa umoja huo bila makubaliano yoyote, sijaona kiwango kama hicho cha shauku, katika kutaka mazungumzo na umoja wa ulaya". **VOA**

# Tetemeko la ardhi latikisa mkoa Katavi

**Na Mary Geofrey**

TETEMEKO la ardhi limetokea usiku wa kuamkia jana mkoani Katavi na kuyakumba baadhi ya maeneo na mikoa ya jirani.

Kwa mujibu wa mjiolojia kutoka Wakala wa Jiolojia Tanzania (GST), Gabriel Mbogoni, tetemeko hilo lilikuwa na ukubwa wa 5.5 katika vipimo vya ritcher na kilomita 10.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Katavi, Benjamin Kuzaga, aliiambia Nipashe kuwa tetemeko hilo lililotokea saa (9:00 usiku) lilidumu kwa dakika tatu huku akieleza kwamba athari zake bado hazijajulikana.

Kamanda Kuzaga alisema tetemeko hilo lilitokea katika wilaya tatu za Mpanda, Mlele na Tanganyika mkoani Katavi.

"Ni kweli kuna tetemeko la ardhi ambalo limetokea usiku wa kuamkia leo majira ya saa 9:00 usiku na limedumu kwa dakika tatu. Mpaka sasa hakuna madhara kwa binadamu, " Kamanda Kuzaga alisema.

Alisema wanaendelea kushirikiana na wakuu wa wilaya, wakurugenzi wote ili kubaini kama kuna madhara mengine yoyote yaliyotokea kutokana na tetemeko hilo.

Aidha, kamanda aliwataka wakazi wa mkoa huo kukaa maeneo ya wazi, ili waweze kujikinga pindi tetemeko hilo litakapotokea tena.

**TETEMEKO LA KAGERA**

Tetemeko kama hilo, liliwahi kutokea mkoani Kagera Septemba 10, 2016 karibu na mji wa Bukoba.

Tetemeko hilo lilikuwa na nguvu ya 5.9 kwenye kipimo cha MMS karibu na kilomita 40 chini ya uso wa ardhi katika kata ya Nsunga karibu na mpaka kati ya Tanzania na Uganda.

Kutokana na tetemeko hilo, watu 17 waliripotiwa kupoteza maisha na wengine 440 walijeruhiwa na zaidi ya nyumba 2,000 ziliharibiwa.

Aidha, lilisababisha kishindo na mshtuko hadi nchi jirani za Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Kenya.

Nchini Uganda maeneo yaliyoathiriwa na tetemeko hilo ni Kyebe, Minziro na Kannabulemu.




Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Harrison Mwakyembe (kushoto), akifunua kitambaa kuashiria uwekaji wa jiwe la msingi katika ujenzi wa ukumbi wa chakula, maabara na chumba cha kompyuta wakati wa mahafali ya 15 ya darasa la saba na wanafunzi wa awali katika Shule ya awali na Msingi ya Bethel Mission Mabibo Makuburi jijini Dar es Salaam juzi. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Simiyu yauza pamba ya bil. 65/-

**Na Happy Severine,** SIMIYU

LICHA ya ununuzi wa pamba kutokuwa mzuri katika maeneo mengi yanayolima zao hilo nchini kutokana na kushuka kwa bei, mkoa wa Simiyu umeuza kilo 54,257,314.0 zenye thamani ya Sh. 65,108,775,600.00.

Aidha, pamba iliyokusanywa kwenye maghala ni kilo milioni 132 yenye thamani ya Sh. bilioni 159.3, na iliyosafirishwa ni kilo milioni 83 yenye thamani ya Sh. bilioni 100. Kilo milioni 54 yenye thamani ya Sh.bilioni 65, haijalipiwa.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, mara baada ya kufanya ziara ya kukagua hali ya maendeleo ya ununuzi wa pamba mkoani humo.

Mtaka alisema kuwa kuanzia jana atahakikisha kampuni zote yanayodaiwa yanapeleka fedha za pamba kwenye Vyama vya Msingi vya Ushirika (AMCOS) ili kufikia mwishoni mwa Septemba iwe imenunuliwa yote, hatua itakayopelekea wakulima kupata fedha za kujiandaa na msimu wa kilimo na kujikimu kimahitaji.

Aliwataka wakulima ambao bado wana pamba majumbani kuhakikisha wanaipeleka kwenye AMCOS ili kufikia wanunuzi, na kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza ikiwa kwenye makazi yao.

Pia aliyataka kampuni kuhakikisha yanakusanya pamba iliyopo kwenye maeneo ya pembezoni ili msimu wa mvua ukianza isiwe changamoto kuyafikia.

Kuhusu baadhi ya wanunuzi ambao si waaminifu ambao wamekuwa wakinunua pamba kwa watu binafsi, alisema serikali itawachukulia hatua kali za kisheria ikiwamo kuitaifisha na fedha zitakazopatikana zitafanya shughuli za maendeleo mkoani.

Mkuu wa Wilaya ya Bariadi, Festo Kiswaga na Mkuu wa Wilaya ya Maswa, Seif Shekalage, walisema zaidi ya asilimia 80 ya pamba imeshalipiwa, huku wakiwahakikishia wakulima kuwa pamba yote itanunuliwa na kulipwa fedha zao.

Mwenyekiti wa Chama cha Ushirika Mkoa wa Simiyu (SIMCU), Charles Madata, alisema kuelekea msimu wa kilimo ni vyema pembejeo ziwafikie kwa wakati ili kwenda sambamba na msimu.

# Wanufaika Tasaf watakiwa kuchangamkia viwanda

**Na Elizabeth Zaya,** SINGIDA

MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida Vijijini, Rashid Mandoa, amewashauri wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf) kuchangamkia fursa kwa kutengeneza bidhaa zinazoweza kutumika na viwanda vilivyomo mkoani humo.

Mandoa alitoa wito huo wakati wa majumuisho ya ziara ya maofisa wa Tasaf wilayani humo.

Alisema mkoa wa Singida ikiwamo wilaya yake umebarikiwa kuwa na viwanda vingi, na kwamba kuna haja kwa wananchi wakiwamo walengwa wa Tasaf kuchangamkia fursa zinazopatikana humo kutokana na uwapo wa viwanda.

"Tumeshuhudia wote namna hawa wanufaika wa Tasaf wanavyochakarika kuanzisha vikundi na miradi mingi midogo, lakini nawashauri kwamba hapa kwetu kuna viwanda vingi, watumie na fursa hiyo pia, naamini kupitia vikundi vyao wataweza kuzalisha bidhaa za kutumika katika viwanda hivyo," alisema Mandoa.

Aliongeza: "Walengwa hawa wa Tasaf wamefundishwa namna ya kuwekeza hata kwa kidogo chochote wanachopata, tumeshuhudia namna wanavyojishughulisha na kilimo cha alizeti, dengu na vitunguu na wanafuga pia."

"Yote ni fursa nzuri ambayo wanaweza kuziongezea thamani bidhaa zao na wakauza viwandani, ninaamini watafanya vitu vikubwa ambavyo vitawaacha watu midomo wazi ambao walikuwa wanawadharau."

Akizungumzia ziara hiyo ya kutathmini shughuli zinazofanywa na walengwa, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Tasaf, Zuhura Mdungi, alisema lengo ni kubaini mafanikio na changamoto za utekelezaji wa mpango huo na kutafuta mbinu sahihi za kukabiliana nazo.

"Mfano hapa wilayani wapo watoto wengi, lakini tuliofanikiwa kuwafikia ni 4,092 tunahakikisha wanapelekwa kliniki na kupata huduma nyingine za afya panapohitajika na kubwa zaidi wanahudhuria masomo yao bila vikwazo," alisema Mdungi.

Mdungi alitoa ushauri kwa viongozi wanaosimamia walengwa wa Tasaf katika kila mkoa, kuhakikisha wanatoa elimu ya kutosha kwa walengwa hao namna ya kuendelea kujiwekea akiba na kujishughulisha katika shughuli mbalimbali halali za kujiongezea kipato na pale wanapofanikiwa kuwapisha wengine.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


## NIPASHE NI JIBU LAKO

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**

**Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**au piga simu: 0767 223311**


### KUPOTEA KWA HATI YA KIWANJA

MRISHO MOSHI FARIJALA Anatangaza kupotelewa na ofa ya kiwanja chenye namba 73/B Killichopo KIHONDA.

Yeyote atakae iona ofa hiyo ya kiwanja anaombwa atoe taarifa ktk kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: MOR/MOR/RB/149463/2019.

215410302

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi NO;168/2019.

Ombi la **LUCAS STEPHANO MASDON** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **SAMSON STEPHANO MASDON.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe **16/09/2019** kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa

215410202

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Anuani ya Simu:"WARAKA" Ofisi ya Baraza la Ardhi na Nyumba(W)
Simu 212009 S.L.P 5058,
Telefax 2124576 TANGA
(Makao makuu)
Simu 027-2642622- (Tanga) 02/9/2019

**YAH: SHAURI NAMBA 27 LA 2019**

**SHABANI ELIAS KIBOMA ..........MDAI**
**DHIDI YA**
**ROSEMARY KASHANGA............... WADAIWA**


**KWA: ROSEMARY KASHANGA – POPOTE ULIPO**

SHABANI ELIAS KIBOMA, amefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya ya Tanga dhidi yako. Shauri husika limepangwa kutajwa tarehe 18/09/2019 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Hivyo basi, unatakiwa kufika katika Baraza hili bila kukosa. Vielelezo vyote vya kesi vinapatikana katika Masijala ya wazi ya Baraza la Ardhi na Nyumba (W) Tanga. Endapo hutatekeleza haya, shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa uamuzi.
AMRI: hii imetolewa na kutiwa Saini Muhuri/Lakiri wa Baraza hili leo tarehe 09/09/2019.

215410602

---

### KUPOTEA KWA CHETI



**Fortunatus Palapala Malima** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0332/0734** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya Sekondari Morogoro.

**Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: DOM/RB/461/2019**

115327502

---

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA
USIMAMIZI WA MIRATHI
(S.M.M.1984 NYONGEZA)
YA 5 KANUNI YA 2
Katika mahakama ya mwanzo
MJINI MOROGORO

Usimamizi wa mirathi NO;174/2019.

Ombi la **PAUL SALVATORY MJEMA** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **MATHIAS HAMPHREY MJEMA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 26/09/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 09/09/2019

215410402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI NA. 225 YA 2019**
**BAINA YA**
**ZAINAB KAISI...................................MUOMBAJI**
**(Msimamizi wa mirathi ya Marehemu Mohamed Kaisi)**
**DHIDI YA**
**HAMISI RAMADHANI KAGOLWA**
**JOHN AGREI MZAVA .........................................WADAIWA**

JULIANA JOHN NA WENZAKE 13

KWA:-HAMISI RAMADHANI KAGOLWA
JOHN AGREI MZAVA
JULIANA JOHN NA WENZAKE 13
POPOTE MLIPO

**YAH:KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika Nakala ya Maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili.

Kwa hiyo mnatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili Wewe binafsi,Wakili au Mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 18.09.2019 saa 3.00 asubuhi. Kwa mujibu wa maombi hayo mnatakiwa kuleta utetezi wenu kwa maandishi.

ANGALIZO:-Kama hamkuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu,Baraza likithibitisha kuwa mmepokea Hati ya Wito,Baraza linaweza kutoa Hukumu dhidi yenu.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 2 ya Mwezi wa September,2019.

215411301

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

ABEL NHALIKI MPEMBA anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **SUZUKI CARRY** yenye namba za usajili **T 142 CNG.** Chassis No. DC51T518548, Engine No. F6AEAA8548.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi DOD/DOD/RB/172097/2019.

215411202

---

IN THE COURT OF DISTRICT DELEGATE OF
DODOMA
AT DODOMA

Probate and Administration cause no. 69 of 2019
In the matter of the Estate of the late STEVEN NKANA KASANYI

AND
IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY VICTOR KASANYI

**GENERAL CITATION**

(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 of 1963)

ALL PERSONS claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filled on or before the 19 Day of September 2019.

Dated at Dodoma this 30TH day of August 2019

215411402

---

### KUPOTEA KWA VYETI



Samson Mwakyusa anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0450-0063 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka2005 katika Shule ya Sekondari Usoke.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: 2546/2019

115410902

---

### KUPOTEA KWA VYETI



Christina L. Marwa anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1060/0011 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2011 katika Shule ya Sekondari St. Mary's.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa: UD/B.I/1/VOL.XVII/2019

15409102

---

### KUPOTEA KWA KADI

Famari Investment T. Ltd anatangaza kuptea kwa kadi ya gari aina ya TRACTOR yenye usajili wa namba T502 CQP yenye chasis namba 5211546.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: CHAR/RB/400/2019

215410802

---

### KUPOTEA KWA KADI

Famari Investment T. Ltd anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SCANIA yenye usajili wa namba T950 CQN yenye chasis namba 5212027.

Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochcote cha Polisi.

Polisi Taarifa: CHAR/RB/400/2019

215410802

---

IN THE DISTRICT LAND AND HOUSING TRIBUNAL
**FOR MBEYA AT MBEYA**
APPLICATION No.139 OF 2019
SIMON JULIUS GATUNA=================APPLICANT
Versus
LAURENT LAITON=== 1st RESPONDENT , SHONGO TAMSON===2ndRESPONDENT
SILINJANJE ZAMBI===3RDRESPONDENT,NDUDU TAMSON===4THRESPONDENT
CHAKUPEWA KIBOSI===5THRESPONDENT,KASIMU TALA===6THRESPONDENT
ROZINA VYASYOLE===7THRESPONDENT,DICKSON MWATUMBE===8THRESPONDENT

**SUMMONS TO FILE DEFENCE AND NOTICE FOR HEARNG.**

This is to inform the respondent that the above case has been filed against you in this Tribunal.
TAKE NOTICE THAT,you have to file the Written Statement of Defence upon receipt of this notice.
TAKE FURTHER NOTICE THAT.In case the same is not filed immediately after receipt of this notice,the Tribunal will proceed to make necessary orders.
The case will come for mention on16th day of September,2019.

Given under my **HAND** and the **SEAL** of the Tribunal this 28th day of Augost,2019.

215411502

---

IN THE DISTRICT LAND AND HOUSINGTRIBUNAL
FOR MBEYA AT MBEYA
APPLICATION No.139 OF 2019
SIMON JULIUS GATUNA===============APPLICANT
Versus
JAMSON WILSON==9THRESPONDENT,UPENDO MAJALIWA==10THRESPONDENT
SHINA TAMSON ==11THRESPONDENT,KENEDY SAWANGA==12THRESPONDENT
MARY JACKSON==13THRESPONDENT,RICHARD JACKSON==14THRESPONDENT
MASHAKA===15THRESPONDENT,MALUGU BOYMANDA===16THRESPONDENT
ISMAIL MWINUKA==17THRESPONDENT

**SUMMONS TO FILE DEFENCE AND NOTICE FOR HEARING.**

This is to inform the respondent that the above case has been filed against you in this Tribunal.
TAKE NOTICE THAT,you have to file the Written Statement of Defence upon receipt of this notice.
TAKE FURTHER NOTICE THAT.In case the same is not filed immediately after receipt of this notice,
the Tribunal will proceed to make necessary orders.
The case will come for mention on 16th day of September,2019.
Given under my **HAND** and the **SEAL** of the Tribunal this 28th day of Augost,2019.

215411502

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Baruapepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Jumatano** tarehe **11-09-2019** kampuni ya **NZASULE SAWMILL INVESTMENTCO. LTD** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **MUFINDI** kuelekea **RUJEWA,** gari hizo zenye namba za usajili:
   **T187 BNY / T 725 ASH.**
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| Urefu | - | mita | 17 |
| Upana | - | mita | 3.66 |
| Kimo | - | mita | 4.7 |

3. Njia itakayotumika **MUFINDI hadi RUJEWA.** Gari litasafiri muda wa mchana tu **(kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

---

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MESSI KUPEWA MKATABA WA MAISHA BARCA



**BARCELONA,** Hispania

KLABU ya Barcelona ipo tayari kumwongezea mkataba mpya, Lionel Messi ambao utamfanya amalizie kipindi chake cha uchezaji hapo kwenye dimba la Nou Camp.

Nyota huyo wa Argentina amebakiwa na miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa, lakini Barca inajiamini kwamba itaweza kumshawishi mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kuendelea kucheza baada ya Kombe la Dunia mwaka 2022.

Na mkataba huo mpya utakuwa wa maisha kwani pia utamfanya Messi abakie hapo Barca kwa muda mrefu hata baada ya kipindi chake cha uchezaji kumalizika, kwa mujibu wa Gazeti la Mundo Deportivo.

Hakuna haraka ya kusaini mkataba huo mpya, lakini Rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu na baba wa Messi, Jorge ambaye ni wakala wake, wamekuwa wakiwasiliana mara kwa mara.

Messi bado ana matarajio ya kuichezea Argentina kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar na kipindi hicho atakuwa na umri wa miaka 35.

Hata hivyo, Messi aliwahi kuripotiwa akisema kwamba, akimaliza muda wake wa kucheza pale Barca atarudi nyumbai kwao Rosario nchini Argentina kumalizia soka katika klabu yake ya utotoni ya Newell's Old Boys.

Lakini kuondoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Hispania, hakutakuwa kazi rahisi zaidi kwa Messi ambaye amekaa na klabu hiyo kwa kipindi cha karibia miongo miwili akianzia kikosi cha vijana mwaka 2001.

Kwa kipindi hicho chote amefunga mabao 419 katika mechi 452 alizocheza katika kikosi cha timu ya wakubwa kwa muda wa miaka 15.

# Emerson aipa pigo Chelsea

**LONDON,** England

CHELSEA imepata pigo kwenye kikosi chake baada ya Emerson Palmieri kuumia misuli wakati akiichezea Italia kwenye mchezo wa kuwania kufuzu michuano ya Euro dhidi ya Finland Jumapili.

Beki huyo wa kushoto mwenye umri wa miaka 25, alianza kwenye kikosi cha Italia kinachoongoza msimamo wa Kundi J katika kufuzu Euro 2020 kwenye uwanja wa Tampere.

Lakini Emerson aliumia dakika sita tu baada ya mchezo huo, wakati akipambana na mshambuliaji wa Norwich, Teemu Pukki.

Emerson mzaliwa wa Brazil na aliyehamia Italia, sasa anaonekana kwamba ataukosa mchezo wa Chelsea dhidi ya Wolves Jumamosi.

Na kocha wa Chelsea, Frank Lampard pia anakabiliwa na mchezo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Valencia, na baada ya hapo wataifuata Liverpool.

Mchezo mwingine mwezi huu ni ule wa Kombe la Carabao dhidi ya Grimsby au Macclesfield, na mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Brighton.





# *Man City yajitosa kumwania Skriniar*

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City inajipanga kutoa ofa kwa nyota wa Inter Milan, Milan Skriniar wakati wa dirisha dogo la usajili Januari kwa ajili ya kumaliza tatizo la majeruhi kwenye kikosi hicho.

Aymeric Laporte, ambaye ni beki wa kati chaguo la kwanza, amefanyiwa upasuaji wa goti na hatarajii kurudi uwanjani kabla ya mwaka mpya.

Na hiyo imekifanya kikosi cha Man City kubakiwa na Nicolas Otamendi na John Stones kama ndio mabeki wa kati pekee wa kocha, Pep Guardiola.

Kwa mujibu wa Gazeti la Express, City wanataka kuimarisha safu yao ya ulinzi kwa kumsajili Skriniar Januari. Mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England wanashika nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi na wanataka kuimarisha kikosi chao ili kupambana na Liverpool.

Kwa sasa kocha huyo wa City ameamua kumtumia Rodri na Fernandinho kama mabeki wa kati.

Na pia Kyle Walker ambaye anatumika kucheza kama beki wa tatu akiwa kwenye kikosi cha England.

Skriniar mwenye umri wa miaka 24, awali alikuwa anawaniwa na wapinzani wa Man City, Manchester United.

HABARI MICHEZO

# MARTINEZ ASEMA LUKAKU NI KAMA AMEZALIWA UPYA



**LONDON,** England

ROMELU Lukaku yupo tayari kuthibitisha ubora wake katika ukurasa mpya wa maisha yake ya soka akiwa na Inter Milan, kwa mujibu wa kocha wa timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez.

Lukaku hatimaye alifanikiwa kukamilisha uhamisho wake wa kutua pale Inter Milan mwezi uliopita, miaka miwili baada ya mshambuliaji huyo wa zamani wa Chelsea kujiunga na Manchester United akitokea Everton.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alifunga mara mbili katika mechi mbili na klabu yake hiyo mpya na Martinez - ambaye aliwahi kumnoa Lukaku pale Everton - amesema mshambuliaji huyo anaonekana kama amezaliwa upya.

"Hii ni mara ya kwanza nimemwona akiwa huru na mwenye furaha. Awali sikumwona Rom akiwa na furaha, lakini sasa anaonekana mwenye furaha kubwa akiwa katika changamoto mpya," alisema Martinez akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wa Ubelgiji dhidi ya Scotland.

"Nafikiri kwa sasa yupo tayari kukabiliana na ukurasa mpya wa maisha ya soka akiwa na Inter Milan.

"Na anaonyesha hamasa kubwa na amejipanga kuthibitisha ubora wake hadi kwenye timu ya taifa, hivyo nimevutiwa na namna alivyo na furaha kwa sasa na nina amini atakuwa kwenye wakati bora zaidi.

"Romelu ni mmoja wa wachezaji bora wa soka la kisasa na anaonekana ni kama amezaliwa upya."

## Rose kuanika ukweli hatima yake

**LONDON,** England

DANNY Rose amesema kwamba ukweli kuhusu kutojulikana kwa hatima yake hapo Tottenham wakati wa dirisha la usajili la kipindi cha joto kilichopita utajulikana.

Majaliwa ya Rose hapo Spurs yalionekana kama yamefikia mwisho baada ya klabu hiyo kumuacha kwenye ziara ya maandalizi ya msimu mpya wa ligi barani Asia ili aweze kupata nafasi ya kupata timu ya kumnunua, lakini mpango huo ukashindikana.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ameanza kwenye mechi zote nne za Ligi Kuu za Tottenham msimu huu na pia alianza kwenye kikosi cha England kilichocheza dhidi ya Bulgaria kwenye mchezo wa kufuzu michuano ya Mataifa ya Ulaya juzi Jumamosi.

Rose amebainisha kwamba ukweli kamili kuhusu majaliwa yake utawekwa hadharani hivi karibuni.

"Haikuwa ngumu, kila kitu kitakuwa hadharani," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Si kila kitu kilichoandikwa wakati wa dirisha la usajili kilikuwa cha kweli na nafikiri nitasema kilichotokea.

"Pengine ningekuwa na furaha zaidi kama ningeuzwa, lakini kuanza kwenye mechi za kwanza nne za Tottenham na kuanza katika kikosi cha England kumenipa hamasa.

"Siwezi kuongopa kwa sasa nina furaha, lakini nataka kusema kwamba, kila kilichoandikwa wakati wa kipindi cha usajili hakikuwa cha kweli."

Licha ya Spurs kutaka kuondoka kipindi cha majira ya joto, Rose hana shaka yoyote na uhusiano wake na kocha, Mauricio Pochettino kwani imebaki kuwa imara.



## Southgate: Fowadi ya England ni bora duniani



**LONDON,** England

GARETH Southgate anaamini kwamba, safu ya ushambuliaji ya England ndiyo yenye hamasa na bora zaidi kuliko yoyote katika dunia ya soka kwa sasa.


Mshindi wa Kiatu cha Dhahabu wa Kombe la Dunia, Harry Kane alifunga 'hat-trick' Jumamosi wakati England ikiibuka na ushindi wa 4-0 dhidi ya Bulgaria kwenye mchezo wa kufuzu kwa michuano ya Euro 2020.

Nahodha huyo wa England si tu kwamba amefunga mabao 25 katika mechi 40 za kimataifa, bali pia amekuwa na upatina mzuri na Raheem Sterling na Marcus Rashford, pamoja na makinda Jadon Sancho na Callum Hudson-Odoi.

"Nafikiri kwa sasa safu ya ushambuliaji ya England ndio inayohamasisha zaidi," alisema Southgate akiwaambia waandishi wa habari.

"Ukiangalia safu ya wachezaji watatu pale mbele kwa hakika ni imara zaidi. Tuna Sancho na Hudson-Odoi ambao wanaendelea kuimarika kwa uhakika kabisa inavutia.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA



# RAMOS AIFIKIA REKODI YA CASILLAS, ATAKA 200

Bado ninapaswa kupiku idadi hiyo na ninatumai bado ninaweza kuichezea nchi hii...

**MADRID,** Hispania

NAHODHA wa Hispania, Sergio Ramos, amesema lengo lake ni kufikisha mechi 200 za kimataifa baada ya kufikia rekodi ya Iker Casillas timu ya Taifa ya Hispania.

**Ramos amefikia rekodi ya Casillas kufuatia juzi, Jumapili kuichezea timu ya Taifa ya Hispania mechi ya 167 wakati wakishinda 4-0 dhidi ya Visiwa vya Faroe kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020.**

Baada ya kumfikia Casillas katika mechi hiyo ya kuwania kufuzu ya Kundi F, beki huyo mwenye umri wa miaka 33, ambaye kwa mara ya kwanza alianza kuichezea timu ya taifa mwaka 2005, alisema: "Rekodi zipo pale kwa ajili ya kuvunjwa.

"Natumai kuwa kasi hii, shauku na matamanio huambatana nami kila wakati na kwamba ninafikia mechi 200, ambazo ndizo lengo.

"Unapaswa kulifanya hilo kuwa gumu."

Casillas alimsifu Ramos baada ya nahodha huyo wa Hispania na Real Madrid kuungana naye katika kitabu hicho cha historia.

"Hongera kwa mechi hizo 167!! Natumai kuna nyingi zaidi. Kipindi kizuri tumeishi na @SeFutbol," Casillas alitupia katika mtandao.

Ramos, ambaye ni mshindi mara mbili wa Kombe la Ulaya mwaka 2008 na 2012 na mshindi wa Kombe la Dunia 2010 - alijibu: "Nimejifurahisha na sifa za Iker.

"Bado ninapaswa kupiku [idadi hiyo] na ninatumai bado ninaweza kuichezea nchi hii kwa miaka mingi zaidi."

Mabao mawili mawili kutoka kwa Rodrigo na Paco Alcacer dhidi ya Visiwa vya Faroe yaliiweka Hispania katika mbio nzuri za kufuzu Euro 2020.

Hispania imeshinda mechi zake sita na hivyo kuongoza Kundi F kwa pointi saba zaidi ya Sweden inayoshika nafasi ya pili, huku Romania ikiwa na alama 10 katika nafasi ya tatu, wakati Visiwa vya Foroe vikiburuza mkia bila pointi katika kundi hilo ambalo pia linajumuisha Norway na Malta.

Ramos alimsifu Kocha Mkuu wa Hispania, Robert Moreno, ambaye amebeba mikoba ya Luis Enrique kuanzia Juni mwaka huu baada ya kocha huyo wa zamani wa Barcelona aliyeachia ngazi kwa sababu binafsi kabla ya bintiye kufariki mwezi uliopita.

"Nadhani yupo vizuri na tumefurahishwa naye," Ramos alisema.

"Anakijua kikosi chetu na namna ya uchezaji wetu vizuri. Anaweza kutusaidia."

## ZISIKUPITE

### MESSI KUFUNGWA MAISHA

BARCELONA inaandaa mkataba mpya kwa Lionel Messi ambao utambakiza Nou Camp nyota huyo wa kimataifa wa Argentina kwa kipindi chote kilichobaki katika maisha yake kisoka. ***(Mundo Deportivo - in Spanish)***

### VAN DIJK APAGAWA MZIGO LIVER

BEKI wa Liverpool, Virgil van Dijk, anapagawa na mazungumzo kuwa atapewa ofa ya mkataba mpya utakaomfanya kulipwa pauni 200,000 kwa wiki. ***(Liverpool Echo)***

### PALMIERI, CHELSEA KUTETA

CHELSEA imekuwa ikilazimishwa kurejea mazungumzo ya mkataba mpya na beki wa kushoto, Emerson Palmieri, 25, wakati kocha wa zamani wa 'Blues', Maurizo Sarri akivutiwa kuzungumza na nyota huyo wa kimataifa wa Brazil kuipata huduma yake Juventus. ***(Express)***

### LUIS AZIINGIZA VITANI UTD, CITY

MANCHESTER United na Manchester City zinajiandaa kuingia katika mbio za kuwania saini ya kiungo wa Benfica na Ureno U-20, Florentino Luis, 20. ***(Star)***

### SABABU POGBA KUICHUNIA REAL

KIUNGO Mfaransa Paul Pogba, amebaki Manchester United badala ya kwenda Real Madrid kwa sababu ya dili la wadhamini wa michezo la pauni milioni 150. ***(Sun)***

### KUZITOSA UNITED, JUVENTUS

KIUNGO wa Lazio, Sergej Milinkovic-Savic, 24, yupo mbioni kutia saini mkataba mpya, licha ya nyota huyo wa kimataifa wa Serbia kuzivutia Manchester United, Paris St-Germain na Juventus. ***(Mail)***

### ROJO KUTIMKIA ASTON VILLA

BEKI wa Manchester United, Marcos Rojo, alikuwa akihusishwa na kuondoka majira haya ya joto, atatoa msukumo wa kujiunga Aston Villa Januari. ***(Birmingham Live)***

### BADO AITAMANI ARSENAL

KELECHI Nwakali, 21, kiungo Mnigeria ambaye amejiunga na klabu ya Daraja la Pili ya Hispania, Huesca akitokea Arsenal majira haya ya joto, anataka kurudi Uwanja wa Emirates kwa siku zijazo. ***(Score Nigeria)***

### KUPAMBANA NA SESSEGNON

BEKI wa kushoto Danny Rose, 29, anataka kubaki na kupigania namba Tottenham Hotspur licha ya kuzivutia klabu nyingine pamoja na kutua kwa Muingereza Ryan Sessegnon, 19, kutoka Fulham majira ya joto. ***(Mirror)***

### REAL KUMRUDIA VAN DE BEEK

REAL Madrid itarudia mpango wake wa kumsajili kiungo wa Ajax, Mholanzi Donny van de Beek, 22, majira ya joto yajayo. ***(Mail)***

### HATAKI KUSIKIA KUSTAAFU

KIPA wa Bayern Munich na Ujerumani, Manuel Neuer, 33, hana mpango wa kustaafu. ***(Mirror)***

### PUEL ATAZAMWA LISBON

KOCHA wa zamani wa Leicester City, Claude Puel nafasi ya kuinoa Sporting Lisbon ya Ureno inamhusu. ***(L'Equipe - in French)***

HABARI MICHEZO

## Mchenga kuivaa TMT robo fainali

**Na Sabato Kasika**

TIMU ya mpira wa kikapu ya Mchenga Bball, ambayo ni bingwa mtetezi wa Sprite Bball Kings 2018, itachuana na TMT kwenye mchezo wa robo fainali ya mashindano hayo mwaka huu.

Mchenga Bball imetinga robo fainali baada ya kuiondoa Temeke Heroes kwa vikapu 114 - 92, katika mchezo uliofanyika Jumamosi kwenye viwanja vya Don Bosco jijini Dar es Salaam.

Timu hiyo imepangwa kuumana na TMT baada ya droo iliyochezeshwa jana katika ofisi za East Africa Radio na EATV, mikocheni, jijini Dar es Salaam.

Mbali na timu hiyo, nyingine zilizotinga fainali ni Flying Dribblers ambayo itakwaana na Dream Chaser, wakati Tumaduni ikitarajia kupimana nguvu na Ukonga Hitmen na KG Dallas nayo ukiumana na Water Instutite.

Kwa mujibu wa msemaji wa mashindano hayo Goza Chuma, robo fainali itachezwa Septemba 15 na kwamba viwanja ambavyo mchezo huo utafanyika vitajulikana baadaye.

"Niwakumbushe kuwa mashindano haya yanaandaliwa na East Africa Televisheni na East Africa Radio kwa kushirikiana na kinywaji cha Sprite ili kuibua vipaji vya mpira wa kikapu nchini," alisema Chuma.

Alifafanua kuwa East Africa Televisheni na East Africa Radio ni chombo cha habari kinachoziunganisha nchi za Afrika Mashariki kikiwalenga zaidi vijana kuanzia miaka 18 hadi 35 ili kuwahabarikisha, kuwaburudisha na kuwaelimisha kupitia vipindi mbalimbali.

## Omondi, Pilipili kuwasha Dodoma

**Na Mwandishi Wetu**

MCHEKESHAJI maarufu wa Afrika Mashariki, Erick Omondi, anatarajia kutua nchini na kufanya 'shoo' kali ya 'standup comedy' katika jukwaa moja na mchekeshaji maarufu nchini, Emmanuel Mathias maarufu Mc Pilipili, mkoani Dodoma Septemba 28, mwaka huu.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, mwandaaji wa Tamasha la Pilipili Live Comedy Festival, Mc Pilipili alisema tamasha hilo litawakutanisha wakali hao katika jukwaa moja na kila mmoja kuonyesha kazi zake.

Alisema Erick amekuwa akimvutia tangu alipoanza kazi ya uchekeshaji na yeye ndiye aliyemtia moyo katika kuingia kwenye fani ya uchekeshaji baada ya kwenda kumuona katika moja ya kazi zake jijini Nairobi, Kenya.

"Nampenda sana Erick Omondi na anakuja Dodoma kufanya 'shoo' kali ya uchekeshaji ambayo najua itagonga nyoyo za mashabiki wetu na kiingilio sio kikubwa sana V.V.I.P ni Sh. 50,000, V.I.P Sh. 30,000, huku kawaida ikiwa Sh. 10,000 ninaimani itakuwa 'shoo' kubwa na ya aina yake kwa Erick kuja Dodoma," Mc Pilipili alisema.

# SIMBA, MTIBWA SUGAR ZAWAISHWA UHURU

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wakiendelea kujifua katika viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam, Bodi ya Ligi Kuu imerudisha nyuma mechi yao ya ligi hiyo dhidi ya Mtibwa Sugar.

**Awali mechi hiyo ilikuwa ipigwe Septemba 18, mwaka huu katika Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, lakini sasa mchezo huo utapigwa Ijumaa Septemba 13, wiki hii katika dimba hilo maarufu 'Shamba la Bibi'.**

"Mchezo wa Ligi Kuu dhidi ya Mtibwa Sugar ambao ulipangwa kuchezwa Septemba 18, mwaka huu umerudishwa nyuma na sasa utachezwa Ijumaa Septemba 13, saa 10:00 jioni kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam," ilieleza taarifa ya Simba.

Nipashe lilipomuuliza Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka nchini (TFF), Cliford Ndimbo, sababu za mabadiliko hayo ya ratiba kwa mechi hiyo ya Simba, alisema yametokana na timu hiyo kutolewa kwenye mashindano ya kimataifa, Ligi ya Mabingwa Afrika, hivyo sasa kutokukabiliwa na ratiba ngumu.

"Awali ratiba hiyo ilipangwa ikilenga kwamba Simba ingeweza kuendelea na michuano ya kimataifa, lakini sasa imetolewa hivyo inaweza kucheza kwa sababu haikabiliwa na ratiba ngumu ndiyo maana kumefanyika mabadiliko hayo," Ndimbo alisema.

Simba iliyokuwa ikiiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ilitolewa raundi ya awali na UD Songo ya Msumbiji kwa faida ya bao la ugenini baada ya kulazimisha suluhu nchini humo kabla ya kulazimishwa sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Katika hatua nyingine uongozi wa Mtibwa Sugar umeshaweka wazi lengo la kupata pointi tatu za kwanza msimu huu baada ya kukubali kupoteza katika mechi ya ufunguzi kwa kuchapwa mabao 3-1 dhidi ya Lipuli FC kwenye Uwanja wa Kumbukumbu ya Samora mjini Iringa.

"Tulipoteza mbele ya Lipuli sasa ni muhimu kwetu kushinda mchezo wetu dhidi ya Simba, tunahitaji kupata pointi tatu zao ili kujiweka kwenye mazingira ya ushindani," Ofisa Habari wa Mtibwa Sugar, Thobias Kifaru alisema.



Kocha wa Timu ya Mchenga Bball, Mohamed Yusuf (kushoto) akijinasibu mbele ya Kocha wa TMT, Isihaka Masoud, kwamba timu yake imejiandaa kutetea ubingwa, wakati wa upangaji wa droo ya hatua ya robo fainali iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# NMB kuendelea kuibeba gofu TPDF

**Na Faustine Feliciane**

KATIKA kusapoti harakati za kimichezo na kiuchumi kwa timu za Majeshi ya Ulinzi na Usalama Tanzania (TPDF), Benki ya NMB imeahidi kuendeleza udhamini wao kwao.

Ahadi hiyo imetolewa wakati ikipongezwa kwa mchango uliobadili taswira ya mchezo wa gofu nchini kiasi cha kuvutia wengi miongoni mwa Watanzania.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi zawadi kwa washindi wa Michuano ya Gofu ya Mkuu wa Majeshi Tanzania (CDF Cup 2019), Mkuu wa Kitengo cha Wafanyabiashara Wakubwa wa NMB, Filbert Mponzi, alisema benki yake itadumisha kadri iwezavyo ushirikiano na sapoti kwa TPDF.

Hafla hiyo ilifanyika katika Viwanja vya Gofu Lugalo, ilikofanyika michuano ya siku mbili ya CDF Cup 2019, iliyodhaminiwa na Benki ya NMB, ikiwa na lengo la kuadhimisha Siku ya Majeshi ya Wananchi wa Tanzania (JWTZ), ambayo hufanyika Septemba Mosi ya kila mwaka.

Mponzi alisema Maajeshi ya Ulinzi na Usalama nchini ni miongoni mwa taasisi nyeti zilizo na wateja wengi katika benki yake na kwamba hicho ndicho huwapa msukumo wa kusaidia michezo na timu zao kulingana na mahitaji.

"NMB, tunaahidi kuendelea kudhamini CDF Cup, lakini pia kusapoti timu za Majeshi Tanzania, na hii inatokana na sera ya kusapoti michezo ya benki yetu, ambayo pia tulidhamini ushiriki wa Jeshi la Tanzania katika Mashindano ya Majeshi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki nchini Kenya," alisema Mponzi.

NMB CDF Cup ni michuano inayoratibiwa na Klabu ya Gofu Lugalo na kudhaminiwa na benki hiyo, ambako mwaka huu iliwakutanisha washiriki wengi zaidi na kuvunja rekodi, kati yao 127 wa ridhaa, 19 wa kulipwa na 25 watoto (Juniors), huku Ally Mcharo wa TPC Moshi akiibuka mshindi wa jumla.

Akizungumza baada ya kukabidhiwa taji la jumla la michuano hiyo na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi, Mohamed Yakubu, Mcharo aliipongeza NMB kwa sapoti iliyobadili taswira ya mchezo na kuufanya kuwa mmoja kati ya michezo pendwa nchini, kauli iliyoungwa mkono na Mnadhimu Mkuu, Yakubu.

Mcharo aliiomba benki hiyo kutouacha njiani mchezo huo, badala yake iendelee kuusapoti na kudhamini mashindano mbalimbali ya gofu, ili kuzalisha wakali watakaolitangaza taifa nje ya mipaka ya Tanzania na Afrika kwa ujumla.

NMB imeidhamini CDF Cup 2019 kwa kitita cha Sh. milioni 21.7. Benki hiyo imekuwa mdau mkubwa wa gofu na mshirika mzuri wa timu za majeshi, ambako mwaka huu iliidhamini timu ya Tanzania iliyoshiriki michuano ya Majeshi Afrika Mashariki, kwa Sh. milioni 15.

# Michezo

Jumanne Septemba 10, 2019

Nipashe




Ramos aifikia rekodi ya Casillas UKURASA 30

HUFUNGI...



Winga wa Hispania, Mikel Oyarzabal akijaribu kufunga dhidi ya kipa wa Visiwa vya Faroe, Gunnar Nielsen kwenye mechi ya kuwania kufuzu Euro 2020 iliyopigwa Hispania na wenyeji hao kushinda 4-0 juzi. **HABARI UK. 30**

# Yanga yasaidiwa kuimaliza Zesco

●●● Yathibitisha kupokea taarifa kutoka Bodi ya Ligi Kuu kuhusu mabadiliko waliyofanya ili kuhakikisha...

**Na Faustine Feliciane**

YANGA imerahisishiwa njia ya kuhakikisha inasonga mbele kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika baada ya Bodi ya Ligi Kuu kusogeza mbele mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Mbeya City ili kuwapa nafasi wawakilishi hao wa Tanzania kujiandaa vema na mechi yao ya raundi ya kwanza dhidi ya Zesco ya Zambia.

Ratiba ya awali ilikuwa ikionyesha baada ya mechi ya raundi ya kwanza ya Ligi ya Mabingwa kati ya Yanga na Zesco Jumamosi Septemba 14, kikosi hicho kinachonolewa na Mwinyi Zahera, kingecheza mchezo mmoja wa Ligi Kuu dhidi ya Mbeya City kabla ya kwenda kurudiana na Zesco ugenini Septemba 22.

Hata hivyo, Bodi ya Ligi Kuu kupitia kwa Mtendaji wake Mkuu, Boniface Wambura, imeuondoa mchezo huo dhidi ya Mbeya City na sasa utapangiwa tarehe nyingine, hivyo kutoa mwanya kwa Yanga kujiandaa vema kabla ya kurudiana na Zesco.

**Tayari Bodi ya Ligi Kuu imewaandikia Yanga na Mbeya City barua kuwajulisha mabadiliko hayo ambapo Yanga kupitia kwa mratibu wake, Hafidh Saleh imethibitisha kuipata.**

"Ni kweli mchezo na Mbeya City haupo tena na hii kwetu ni faraja kuona tutakuwa na muda mzuri kujiandaa na mchezo wetu wa marudiano ugenini," alisema Saleh.

Endapo Yanga itawatupa nje Zesco itatinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Hata hivyo, kama itaong'olewa na Wazambia hao itaangukia kucheza mechi ya mchujo na mojawapo ya timu zitakazofuzu raundi ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika kusaka nafasi ya kucheza hatua ya makundi ya shirikisho.

Yanga imetinga hatua hiyo baada ya kuitoa Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mabao 2-1 ikitoka sare ya bao 1-1 Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam kabla ya kushinda ugenini 1-0.

Timu nyingine ya Tanzania inayoshiriki michuano ya CAF ni Azam FC, ambayo Ijumaa itaikaribisha Triangle FC ya Zimbabwe kwenye Kombe la Shirikisho.

Azam imetinga hatua hiyo baada ya kuitoa Fasil Kenema ya Ethiopia kwa jumla ya mabao 3-2.

# Kaseja atoa siri ya penalti miaka 19

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kuibeba Tanzania kwa kuiongoza Taifa Stars kuitoa timu ya Taifa ya Burundi kwenye mechi ya kuwania kufuzu hatua ya makundi ya kusaka tiketi ya kushiriki Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, kipa mkongwe nchini, Juma Kaseja, ametoa siri ya miaka 19 ya uhodari wake wa kucheza penalti.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Taifa na Stars kusonga mbele kwa changamoto ya mikwaju ya penalti 3-0 baada ya dakika 120 kumalizika kwa sare ya bao 1-1, Kaseja aliendeleza ubora wake wa kucheza penalti kwa mara ya pili mfululizo tangu arejeshwe Stars, ikiwa ni baada ya mwezi uliopita kucheza tena penalti wakati wakiitoa timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars kwenye kinyang'anyiro cha kuwania kufuzu fainali za Afrika kwa Wachezaji wa Ndani, CHAN.

Akizungumza baada ya mechi hiyo juzi, Kaseja alisema uwezo wake wa kucheza mikwaju ya penalti hajafundishwa na kocha yeyote na kwamba hicho ni kipaji chake na kujituma kwake.

"Katika kipindi cha miaka 19 nilichocheza soka kuanzia ngazi ya chini hadi Ligi Kuu sijawahi kufundishwa na mtu yeyote namna ya kudaka penalti, hiki ni kipaji changu kutoka kwa Mungu," alisema Kaseja.

Kaseja ambaye alishaporwa namba katika kikosi cha Taifa Stars na Aishi Manula wa Simba kabla ya Kaimu Kocha Mkuu wa Stars, Etienne Ndayiragije kumrejesha akianza na mechi hiyo ya CHAN dhidi ya Harambee Stars, mbali na kucheza penalti hizo alionyesha uwezo mkubwa wa kuokoa hatari kadhaa kabla ya hatua hiyo ya penalti.

Katika mechi hiyo, Kaseja alianza kwa kuidaka penalti ya Omari Ngando, kisha Saedo Berahino na Gael Bigirimana walikosa penalti zao kwa kupiga nje huku zile za Taifa Stars zikizamishwa kimyani na Erasto Nyoni, Himid Mao na Gadiel Michael.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >